**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 13 Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ingawa jana nilitangaza kwamba itakuwa kwa nadra tuwe tunawatangaza Watanzania wenzetu wanaoingia humu, ila kwa sababu maalum. Lakini leo tunao wageni ambao wanaendeleza kile ambacho kingestahili kwa nchi yetu kiendelee kufanyika nayo ni viongozi wa kada mbalimbali kutembelea. Sasa leo kwenye *Gallery* mkono wangu wa kulia wapo madiwani kutoka mikoa mitatu kama ifuatavyo; kutoka mkoa wa Kilimanjaro, Jimbo la Same Mashariki, madiwani 17 wakiongozwa na Diwani ambaye pia Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Same, Ndugu Kesi. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, sasa kundi la pili ni madiwani ambao kwa bahati kutokana na matatizo ya usafiri bado wako njiani walipata matatizo kutokea Mtwara Masasi, sina haja ya kueleza zaidi mnajua hali halisi. Kwa hiyo, wameingia Dar es Salaam saa sita usiku na saa hivi wamefika hapa Kibaigwa wanakuja hapa Bungeni. *(Makofi)*

Nitapenda kuwatambua wakati huo, lakini nawatamka kwa sababu wamekuja kushirikiana na wenzao, hawa wanatoka jimbo la Lulindi Wilaya ya Masasi watakuwa ni madiwani 28. sasa wenyeji wao ni Jimbo la Mtera, ambao ni madiwani wanane, wanaongozwa na Ndugu Nicholas Kibwana, ambaye ni Katibu mwenezi wa CCM Wilaya ya Dodoma vijijini, naomba nao wasimame wenyeji wale pale. Kwa hiyo, mtaona hapa ni ushirikiano baina ya jimbo la Lulindi la mkoa wa Mtwara, Jimbo la Same Mashariki mkoa wa Kilimanjaro na Jimbo la Mtera Mkoa wa Dodoma, wanatembeleana kubadilishana uzoefu. Spika, angefurahi zaidi kama ingekuwa pia na madiwani kutoka Zanzibar tungekuwa tunatembeleana namna hii ingesaidia sana kupunguza baadhi ya hisia ambazo hata katika mjadala zinajitokeza ambazo hazina msingi. Nawapongeza hao na ninawataka wengine Waheshimiwa Wabunge tuwe tunawawezesha Waheshimiwa madiwani katika nchi yetu kuweza kutembeleana. *(Makofi)*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA, UTAWALA BORA, SIASA NA UHUSIANO WA JAMII):**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejiment ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora, Siasa na Uhusiano wa Jamii) kwa mwaka wa Fedha 2006/2007.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA (MHE. RAMADHANI A. MANENO (K.n.y. MHE. GEORGE M. LUBELEJE))**

Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora, Siasa na Uhusiano wa Jamii) kwa mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA (MHE. SHOKA KHAMIS JUMA):**

Moani ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora, Siasa na Uhusiano wa Jamii) kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 195

**Ujenzi wa Barabara Toka kwa Mkocho kwenda Kivinje**

**MHE. HASNAIN G. DEWJI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa awamu ya nne katika kampeni zake za uchaguzi huko Kilwa Kusini mwezi wa nane mwaka 2005 alitoa ahadi kuwa barabara inayotoka kwa Mkocho kwenda Kivinje kwenye Hospitali kuu ya Wilaya yenye urefu wa km. 5 itatengenezwa kwa kiwango cha lami:-

Je, ni lini Serikali itaanza kuitengeneza barabara hiyo kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbasi Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa kutoka Mkoa wa Lindi kuhusu ahadi zote alizotoa Mheshimiwa Rais wakati wa Mikutano ya Kampeni mwaka 2005, ahadi anayozungumzia Mheshimiwa Mbunge kuwa barabara inayotoka kwa Mkocho kwenda Kivinje kwenye Hospitali Kuu ya Wilaya yenye urefu wa km.5 itatengenezwa kwa kiwango cha lami haikuainishwa miongoni mwa ahadi zilizoorodheshwa na Ofisi ya CCM, Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Mkoa wa Lindi kupitia ahadi hizo ili aone kama ahadi anayoizungumzia imesahauliwa. Hii itasaidia Ofisi yangu kuiingiza kwenye mpango wake wa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa mwaka 2005 – 2010 ikiwa ahadi hiyo ilitolewa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imekuwa ikifanyia matengenezo ya muda maalum *(Periodic Maintenance)* barabara ya Mkocho-Kivinje kama ifuatavyo:-

- Mwaka wa fedha 2000/2001, Halmashauri ilitengeneza barabara hiyo kwa kiasi cha sh.42,820,000/= kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara kwa umbali wa km. 5.

- Mwaka wa fedha 2003/2004 barabara hiyo ilifanyiwa matengenezo kwa gharama ya sh.20,951,700/= kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara kwa umbali wa km.1.

- Mchango wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa katika mwaka 2005/2006 kwa matengenezo ya barabara hiyo kwa maeneo korofi ni sh.2,890,000/= kwa kutumia fedha za Mfuko wa Maendeleo.

- Pia katika mwaka wa fedha 2005/2006 Halmashauri ya Wilaya imepanga kuifanyia matengenezo barabara hiyo kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara na fedha za Mfuko wa Maendeleo kuikarabati Barabara hiyo kiwango ambacho itapitika kwa majira yote ya mwaka.

Na. 196

**Wimbi la Ujambazi**

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa, watu wengi kutoka sehemu mbalimbali wanaishi Buchosa kwa lengo la kutafuta riziki kupitia uvuvi wa samaki. Uvunaji wa miti na shughuli nyingine za

maendeleo na kwa kuwa usalama wa wananchi hawa ni mdogo kutokana na wimbi la majambazi katika eneo:-

(a) Je, jukumu la kuhakikisha usalama wa raia ni la Serikali au kuna Chombo kingine?

(b) Kama jukumu ni la Serikali, Je, ni mali za thamani gani ziliporwa na majambazi wakati wa uvuvi na ni watu wangapi waliuawa katika uporaji huo wa kinyama tangu mwaka 2002 hadi leo; na Serikali ilichukua hatua zipi katika kukomesha hali siyo?

(c) Je, Serikali ipo tayari kununua Boti ziendazo kasi na kuwapa askari wa Wilaya ya Sengerema vifaa vya ulinzi vya kutosha yakiwemo magari ili kuwawezesha kupambana na matukio kama hayo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kumjibu Mheshimiwa Chitalilo (Buchosa) swali lake lenye sehemu (a), (b) na ( c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria Na. 322 (*Police Force Ordinance Cap*.322) kifungu Na.5 (1), ni jukumu la jeshi la polisi kuhakikisha usalama wa raia na mali zao hapo nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, takwimu za Jeshi la Polisi katika jimbo la Buchosa zinaonyesha kuwa, kuanzia mwaka 2002 hadi Mei, 2006 mali zenye thamani ya jumla ya shilingi 163,934,900/= ziliporwa na majambazi ambapo jumla ya watu 11 waliuawa katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa operesheni safisha majambazi inaendelea nchi nzima ikiwa ni pamoja na kuwataka wananchi wasalimishe silaha wanazomiliki kinyume cha Sheria. Aidha, Jeshi la Polisi lina hamasisha wananchi kutoa taarifa za wahalifu hao, sambamba na hilo tunawaomba wananchi kuongeza ushirikiano na jeshi la polisi, walinzi wa jadi na mgambo popote walipo katika jitihada za kutokomeza ujambazi nchini.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kununua Boti mpya ziendazo kwa kasi kadri hali ya Bajeti itakavyoruhusu ili kuwawezesha askari wa kikosi cha wanamaji, kufanya doria kukabiliana na tatizo hili la ujambazi katika maeneo ya Ziwa. Aidha, kati ya mwaka 2006/2007 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbalimbali vya ulinzi yakiwemo magari ambayo yatasaidia pia kuimarisha ulinzi eneo la Buchosa. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza napenda niipongeze Serikali kwa jitihada zake

za kupamba na majambazi ambazo zimefanikiwa kwa kiasi kikubwa. Lakini hapo hapo majambazi hao baada ya kufukuzwa Bara, sasa wamehamia Visiwani.

Je, Serikali inampango gani wa kudhibiti ujambazi ambao umeingia Zanzibar hasa sehemu zenye maduka?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ujambazi si lazima utokee bara tu, hata huko Zanzibar wapo, katika tuliowakamata hasa ambao ni *suspect number one,* moja asili yake ni mtu wa Pemba, kwa hiyo popote pale ambapo watu wapo, ujambazi unaweza ukatokea. Lakini hivi sasa Jeshi la Polisi limeanzisha opereshini maalum kule Zanzibar kuwasaka majambazi, nataka niwahakikishie wananchi kwamba kazi hiyo itafanyika vizuri na majambazi mahali popote walipo tutawafuata na tutawakamata na kama alivyosema Rais dhuluma itashindwa na haki, kwa hivyo tutafanikiwa tu.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jimbo la Kichosa ni sehemu ya Wilaya ya Sengerema, na pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu uimarishaji wa ulinzi katika sehemu mbalimbali zikiwemo sehemu za ziwa, na kwa kuwa ujambazi hasa Ziwani katika Jimbo la Sengerema na hasa sehemu za Chifufu, sehemu za Katungulu Kamanga, Busisi na Biangu imekuwa ni kwa kiwango kikubwa sana.

Je, Serikali ingependa kusema kuwaahidi nini wanajimbo wa Sengerema kuhusu uimarishaji wa ulinzi hasa ziwani wakati wa uvuvi kwa kuzingatia taarifa ambazo zimekuwa zikitoka uhalifu umekuwa ni mkubwa sana?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika swali langu la msingi kwamba, Serikali imejipanga vizuri katika operesheni safisha majambazi, pia inampango wa kununua vyombo vipya katika maziwa kwa nia hiyo hiyo ya kuimarisha ulinzi katika maeneo yote ya ziwa. Hata hivyo, kwa hivi sasa tumechukua hatua mbalimbali kukarabati zile boti ambazo ziko katika hali mbaya na nyingi katika hizo sasa hivi zitakuwa zinafanya kazi. Aidha kama Mheshimiwa Mbunge alinisikiliza sana katika masuala yangu ya majibu ya nyuma huko utaona nilisema suala lazima la Mheshimiwa Waziri Mkuu ameunda operesheni maalum inayovishirikisha vyombo vyote vya dola, kwa nia ya kubana na uhalifu hasa katika maeneo ya mipakani. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Ngeleja na wananchi kwamba *operation* hiyo itaendelea na kwa kiasi kikubwa tunafanikiwa, naomba wananchi watupe subira.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nilighafilika kidogo na ili nitende haki, napenda nitambulishe wageni ambao ni Waheshimiwa Madiwani wanawake wanane, kutoka Shinyanga, ambao wanaongozwa na Mstahiki Meya wa Manispaa ya Shinyanga ambaye ni mwanamke. Naomba Mama Moshi Kanji, pamoja na wenzie, niliona ni jambo nzuri kuwatambulisha hawa hasa kwa sababu katika Manispaa chache sana nchini zina mstahiki meya ambaye ni mwanamke, karibuni sana wakina mama na safari njema. (*Makofi*)

Na. 197

**Kituo cha Polisi Lushoto**

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Polisi Lushoto ni kati ya vituo vya Polisi vya zamani nchini Tanzania vilivyoanzishwa wakati wa utawala wa Wajerumani lakini majengo yake ni machakavu sana kiasi cha kuathiri ufanisi wa utendaji wa jeshi la Polisi Wilayani Lushoto.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga majengo mapya ya kituo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kumjibu Mheshimiwa Balozi Mshangama, Mbunge wa Lushoto, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Balozi Mshangama, Mbunge wa Lushoto, kwamba kituo cha Polisi Lushoto ni kichakavu. Aidha, tatizo hili ni la nchi nzima na katika ngazi zote, Kata, Wilaya na Mkoa.

Mheshimiwa Spika, licha ya uchakavu huo, Jeshi la Polisi litahakikisha hauathiri utendaji wake wa kazi wa kulinda raia na mali zao. Aidha, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba katika kipindi cha Bajeti ya mwaka 2006/2007 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya Polisi nchini, kikiwemo kituo cha Polisi Lushoto. Hata hivyo, kupitia mpango wake wa miaka 10 kuanzia mwaka 2003 – 2013, Jeshi la Polisi lina nia ya kujenga kituo cha Polisi cha kisasa Wilayani Lushoto.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza, kwa kuwa Wilaya ya Mbozi ni wilaya ambayo ina vituo vya polisi vya zamani sana na ambacho kimejengwa wakati wa mkoloni na kwa kuwa majengo yake sasa yamekuwa chakavu sana, na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri amesema kwamba wanampango wa kukarabati kituo cha polisi cha Lushoto.

Je, anaweza kutueleza nini wananchi wa Mbozi kuhusu kituo chetu cha polisi ambacho pia ni chakavu sana?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba kituo cha Mbozi ni kimoja katika vituo vichakavu, lakini kama nilivyosema katika mpango wetu wa miaka kumi kuna maeneo mbalimbali ambayo tumekusudia kuyaimarisha. Tuna jumla ya wilaya 65, katika kipindi hicho ambazo tutajenga vituo, kikiwemo kituo cha Mbozi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira asubiri na jitihada zinachukuliwa. *(Makofi)*

Na. 198

**Tatizo la Uraia Katika Mkoa wa Kigoma**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na tatizo kubwa la uraia katika mkoa wa Kigoma kutokana na athari za wakimbizi jambo linaloifanya Serikali kushindwa kutambua raia wa Tanzania na wasio raia na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi kukamatwa kwa kutuhumiwa kuwa sio raia bila sababu za kufaa:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ipo haja sasa ya kutafuta ufumbuzi wa kudumu kwa tatizo hilo ambalo sasa limekuwa sugu na kero kubwa kwa wananchi wa maeneo hayo?

(b) Je, kwa nini wananchi wa mikoa mingine iliyo mipakani na nchi jirani na Tanzania haina usumbufu mkubwa kama huu wanaoupata wananchi wa Kigoma na kuwafanya wajisikie kuwa hawatendewi haki?

(c) Je, Serikali haioni kwamba sasa umefika wakati wa kutengeneza vitambulisho vya uraia mara moja ili kuondoa kero hizo hasa kwa wananchi wa Kigoma?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya (Viti Maalum), lenye sehemu a, b, na c kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji ni mojawapo ya vyombo vya ulinzi na usalama, hivyo inalo jukumu kisheria la kulinda usalama wa nchi yetu kwa kutumia Sheria Na. 6 ya 1995. Kwa mujibu wa Sheria hii Maafisa Uhamiaji wamepewa uwezo wa kumhoji mtu yeyote inayomhisi sio raia wa Tanzania na yupo nchini kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, mahojiano haya sio unyanyasaji bali ni sehemu ya kuhakikisha usalama wa nchi yetu na utaratibu huu wa kuwahoji watu kuhusu uraia, au halali wa kuwa nchini, haufanyiki katika mkoa wa Kigoma pekee bali katika Mikoa yote ya Jamhuri ya Muungano na hasa ile ya mipakani.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuwepo kwa vitambulisho vya uraia vitasaidia sana Maafisa Uhamiaji kuwatambua raia na wageni wasio raia na hivyo kuleta ufanisi katika kazi ya ulinzi na usalama wa nchi yetu. Kwa kutambua umuhimu wa kuwepo kwa vitambulisho, Serikali kupitia Wizara yangu imeanza mchakato wa kutekeleza mradi wa kuchapisha vitambulisho vya uraia. Maelezo zaidi kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa mradi huu yatatolewa katika hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu wiki ijayo.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa Waziri mwenyewe anayotaarifa ya matatizo mbalimbali ambayo yako pale katika Mkoa wa Kigoma.

Je, leo anatoa tamko gani kwa wale maafisa uhamiaji ambao kwa makusudi huwasumbua hata kama wamejua ni raia halali wa Tanzania?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya awali kwamba kuhojiana kama mtu ni raia au si raia, yuko nchini kihalali, au si halali ni utaratibu wa kawaida kabisa ambao maafisa uhamiaji wanaufanya, na wanafanya hivyo kwa madhumuni tu ya kuihakikishia kwamba nchi yetu watu waliomo ndani ni watu wako ndani kisheria na ni watu ambao ni watu salama.

Sasa kama kuna afisa uhamiaji katika kutekeleza jukumu lake, anavuka mipaka anakiuka maadili, naomba Mheshimiwa Mbunge atuletee jina la huyo mtu na kama ni taarifa ya kweli hatutasita kuchukua hatua.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuwa Tanzania inajulikana kwa ukarimu na jinsi ambavyo inawakaribisha wageni hata wale wenye shida. Kumekuwa na tatizo la wakimbizi hasa kutoka Somalia ambao wanaelekea nchi za Afrika Kusini, na wamekuwa wakipita nchi yetu na kwa mila za kiafrika akija kwako anashida unamkaribisha. Lakini sasa kwa sababu ya jinsi hali ya sheria zilivyo, basi wanakamatwa na wale waliowakaribisha wanakamata, lakini wao wanapita.

Je, Serikali ina mipango ya kuweza kuwasaidia kwa sababu ni watu wenye shida wapate *safe passage* kwenda huko wanakoenda, bila kulazimika kujificha ficha na kusababisha wanaowakaribisha vizuri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, kwa mujibu wa kanuni za maswali hilo linakuwa ni swali jipya, pengine liulizwe wakati wake.

**MHE. MANJU SALUM O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Majibu ya Mheshimiwa Waziri yanasema kama mtu anaushahidi wakati nachangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilitoa vielelezo vinavyoonyesha jinsi watu wa uhamiaji Mkoa wa Kigoma ambavyo hawako makini wameweza kuwachukua watu na wanawatambua kwa makabila, wamewapeleka Kongo na Kongo wamerudishwa, hivi Mheshimiwa Waziri anataka ushahidi gani zaidi ya huo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wakati Mheshimiwa Msambya anachangia hoja ya Waziri Mkuu alitoa

malalamiko kuhusu suala na kutoa nyaraka mbalimbali ambazo alimkabidhi Waziri Mkuu, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Msambya kwamba Waziri Mkuu amekwisha kutukabidhi zile hati zako katika Wizara ya Mambo ya Ndani na tunazifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba niongeze tu kwamba baada ya kupokea malalamiko mengi moja kutoka kwa Mheshimiwa Msambya, tumepata malalamiko kutoka kwa Mheshimiwa Zitto, kutoka kwa Mheshimiwa Mporogomyi yanayohusiana na suala hili leo saa tano tunakutana mimi na Wabunge wote wa Mkoa wa Kigoma na nimemwita Mkurugenzi wa Uhamiaji kutoka Dar es Salaam, amekuja hapa, nimemwita Afisa Uhamiaji Mkoa wa Kigoma yuko hapa.

Tutakaa na Wabunge wa Kigoma, watatupa taarifa walizonazo, nimewaambia waje na taarifa zote walizonazo ili tuzifanyie kazi suala hili tuweze kulitafutia ufumbuzi kwa kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa huu ndio ushahidi wa uwajibikaji, awamu ya ari mpya, ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Na. 199

**Mradi wa Maji wa Trunk Main**

**MHE. DR. ABDALLA O. KIGODA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mradi wa Maji wa *Handeni Trunk Main* unasambaza maji katika eneo la zaidi ya asilimia 50 ya Jimbo la Handeni; na kwa kuwa, mradi huo ulianza mwaka 1977 na baadaye ukakabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ukiwa katika hali inayohitaji ukarabati mkubwa; na kwa kuwa, mradi huo unaohudumia vijiji 155 – Handeni umeshindwa kutoa huduma:-

(a) Je, Serikali inaweza kuhuisha maamuzi yaliyotolewa hapo mwanzoni na *HTM* urudishwe Serikalini ili upate huduma nzuri zaidi?

(b) Je, Serikali inatambua kuwa ikiuhudumia mradi huo itakuwa imetimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa katika Jimbo la Handeni hususani kwenye maeneo ya Komsala, Kwamatuku, Sindeni, Misima na Chanika?

(c) Je, Serikali inaweza kuliambia Bunge juu ya ratiba yake ya utekelezaji wa ahadi hiyo ya Rais?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Handeni ulianza kujengwa mwaka 1975 na kufunguliwa rasmi mwaka 1980. Mradi ulilenga kutoa huduma kwa watu wapatao 180,000 waishio katika vijiji 60 vilivyopo Wilayani.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 1980 uendeshaji wa mradi ulikuwa chini ya Mkurugenzi wa Mkoa wa Tanga. Lakini kutokana na mahitaji ya utaalamu wa Kihandisi uliotakiwa katika uendeshaji wa mradi huo; mwaka 1987 mradi ulihamishiwa Wizara ya Maji. Hata hivyo, mwishoni mwa mwaka 2004 mradi ulikabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni chini ya Bodi ya Mamlaka ya Maji *(HTM)* iliyosajiliwa kisheria na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na.29 la tarehe 30 Januari, 2004. Kukabidhiwa kwa mradi huu kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa ni utekelezaji wa Sera ya Maji ya mwaka 2002 ambayo inaelekeza huduma za maji kuendeshwa na vyombo vya watumiaji maji vinavyotambulika kisheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa kuanzia mwaka huu 2006/2007, uendeshaji wa Mradi wa Maji wa *HTM* utasimamiwa na Serikali kupitia Wizara yangu chini ya Bodi ya Maji iliyoundwa kisheria ambayo Mwenyekiti wake ni mkazi wa eneo la mradi.

Wajumbe wa Bodi wanajumuisha wawakilishi wa makundi mbalimbali ya wakazi wa eneo la mradi, viongozi wa Halmashauri ya Wilaya na Serikali Kuu.

Lengo ni kuhakikisha kuwa wananchi wanashirikishwa kikamilifu katika kusimamia mradi huu. Aidha, Serikali itaendelea kulipia gharama za uendeshaji wa mradi huu mkubwa ikiwemo na miradi mingine mikubwa ya Makonde, Wanying'ombe, Maswa, Mugango/Kiabakari na Chalinze.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa ikiuhudumia mradi huo itakuwa imetimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyotoa katika Jimbo la Handeni hususan kwenye maeneo ya Komsala, Kwamatuku, Sindeni, Misima na Chanika. Serikali pia inaendelea kuufanyia matengenezo na ukarabati mradi kulingana na upatikanaji wa fedha.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo niliyoyatoa hapo juu, ni dhahiri kuwa Serikali imeanza kutekeleza ahadi ya Rais na itaendelea kutenga fedha kuboresha huduma ya maji katika maeneo hayo.

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa kuamua mradi huu urudi chini ya uangalizi wao, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa mradi huu umetengewa fedha chache sana katika kipindi hiki cha Bajeti milioni 25 kwa ajili ya madawa na milioni 45 kwa ajili ya ukabarabati.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuja Chanika kama hatua ya dharura ili nimwonyeshe eneo la Kivesa, Mdoe, Kwamgumi, Zizini na Kwaseuta ili atoe uamuzi wa kuchimba visima ili kupunguza tatizo la uhaba wa maji kwa hivi sasa wakati tukisubiri kuendelea na ukarabati kamilifu wa mradi huu muhimu?

(b) Je, Waziri yuko tayari kusaidiana nami katika kutafuta wafadhili wa kukarabati mradi huu hasa katika kupunguza urasimu na ucheleweshaji wa kutoa maamuzi?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, niko tayari kutembelea Handeni ili kujionea hali halisi ya mradi huu. (*Makofi*)

Vile vile kuhusu kwamba tumetenga fedha kidogo ni kutokana na hali halisi ya Bajeti lakini kila mwaka tutakuwa tunatenga fedha ya kuendelea na ukarabati wa mradi huu kwa sababu ni mkubwa. Vile vile iko miradi iliyotajwa katika jibu la msingi ambayo inahitaji fedha za ukarabati ikiwemo Makonde, Kiabakari, Maswa, Chalinze na Wanying'ombe kule Njombe.

Kwa hiyo, tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge katika kutafuta kila namna itakayowezesha kukamilisha kazi hii na kutafuta wahisani sawasawa na *Doctor*. tusaidiane ukimpata haraka mlete tuongee naye. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sikuwa na hakika kama Mheshimiwa Kigoda alitaka atembelewe na Naibu Waziri au na Waziri lakini hata hivyo tunaendelea. *(Kicheko)*

Na. 200

**Barabara kutoka Bunda – Nansio**

**MHE. CHARLES M. KAJEGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika kampeni ya uchaguzi mkuu, Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Kikwete aliahidi kujenga barabara ya Bunda – Nansio kwa kiwango cha lami na kwa kuwa barabara hiyo inahitaji matengenezo makubwa sana kwa hivi sasa ili iweze kupitika kwa urahisi:-Je, ujenzi wa barabara hiyo utaanza lini ili utekelezaji ahadi ya Mheshimiwa Rais uende sambamba na Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya waliyonayo wananchi wa Mwibara?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Bunda – Kisorya hadi Nansio ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *TANROADS* Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikiifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ikiwa ni pamoja na kuimarisha tuta na kukweka changarawe sehemu mbalimbali kadri Bajeti inavyoruhusu. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2005/2006, jumla ya shilingi 159.68 milioni zilitumika kugharamia matengenezo ya kawaida, matengenezo ya sehemu korofi pamoja na ukarabati katika barabara hiyo. Katika mwaka huu wa fedha 2006/2007, jumla ya shilingi milioni 119.42 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ahadi ya Mheshimiwa Rais, ningependa kuthibitisha kuwa, wakati Wizara yangu inaendelea kukarabati barabara hiyo ili iweze kupitika, Serikali ya Awamu ya Nne inaendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya 2005 pamoja na ahadi zote zilizotolewa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na hivyo Serikali itaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hiyo ndani ya miaka mitano ijayo kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hii ndiyo tegemeo pekee ya usafiri kwa wananchi wa Ukerewe na Mwibira. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba wakati muafaka umefika ili iweze kuwa katika Bajeti ya mwaka ujao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Serikali imedhamiria kutekeleza ahadi hiyo ya Rais. Kuhusu Bajeti hiyo kuwekwa katika mwaka ujao wa fedha itategemea mikakati na mipango ambayo itakuwepo katika Bajeti ya mwaka kesho.

Lakini napenda kumuahidi kwamba barabara hiyo Serikali inajua ni muhimu sana inaunganisha Mikoa miwili ya Mara na Mwanza upande wa Bunda na Ukerewe na hivyo juhudi zote zitafanyika kuhakikisha kwamba barabara hiyo inatengenezwa katika kiwango ambacho kitaridhisha.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa hivi karibuni kidogo meli ya *MV Clarias* izamishe watu na kwa Ukerewe huwa inategemea barabara hii tunapopata matatizo, Serikali haioni ni jambo la dharura kwa Wilaya anakotoka Rais wa Bunge la Afrika kupewa barabara hii katika Bajeti ijayo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, udharura huo umeonekana na katika bajeti ijayo Serikali itazingatia. *(Makofi)*

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, kwa nia njema kabisa Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete amekuwa akitoa ahadi mbalimbali kwa nia ya kutoa maisha bora kwa Watanzania yakiwemo masuala ya barabara katika Wizara hii ya Miundombinu.

Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati sasa kufanya kwa haraka na kuchukulia suala hili kama dharura kwa kuanzisha kitengo maalum cha kushughulikia ahadi zote zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais alitoa ahadi nyingi na nyingi zilikuwa ndani ya Ilani ya Uchaguzi na nyingine kama anavyosema zilikuwa za papo kwa papo.

Lakini niseme kwamba ahadi hizi hazikuwa tu za Wizara ya Miundombinu zilihusisha sekta na Wizara karibu zote na bajeti zimepangwa ili kutekeleza ahadi hizo na kila Wizara na kila asasi inaendelea kutekeleza ahadi hizo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema tulipokuwa pale Chimwaga, hivi karibuni zilitolewa zile ahadi na kila sekta na Wizara inajua ahadi zake imepanga kwenye bajeti na inaendelea kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Miundombinu tumeelekeza nguvu zetu katika kutekeleza ahadi hizo pamoja na zile ambazo ziko kwenye Ilani ya Uchaguzi na asiwe na wasiwasi ahadi zote hizi zitatekelezwa ndani ya miaka mitano kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Na. 201

**Kutengeneza Barabara**

**MHE. JUMA HASSAN KILLIMBAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya Shelui, Ntwike, Tulya, Kidaru, Kisirini na Kasha Kiomboi ni barabara muhimu sana inayotumiwa na wakazi wapatao 80,000; na kwa kuwa, barabara hiyo haipitiki kirahisi wakati wa masika na pia husababisha vifo vya wagonjwa hasa akina mama wajawazito:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuitengeneza barabara hii japo kwa kiwango cha changarawe ili iweze kupitika na kuokoa maisha ya wananchi ili nao waonje raha ya matunda ya Serikali yao waliyoichagua?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, kama ifuatavyo: Barabara ya Shelui – Ntwike, Tulya, Kidaru, Kisiriri hadi Kiomboi ni barabara inayohudumiwa na mamlaka mbili kama ifuatavyo:-

(i) Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Singida inahudumia jumla ya kilometa 21.7 za barabara ya Mkoa kuanzia Shelui (mji mdogo) hadi Ntwike.

(ii) Halmashauri ya Wilaya ya Iramba inahudumia sehemu ya barabara hiyo kuanzia Ntwike hadi Kiomboi.

Mheshimiwa Spika, hali ya barabara kutoka Shelui hadi Ntwike ni ya wastani ambapo kilometa 14.7 hupitika wakati wote na kilomita 7 ziko kwenye hali mbaya kutokana na uharibifu wa mvua za *El-Nino* na hivyo kuhitaji matengenezo makubwa. Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Serikali ilitenga jumla ya shilingi 12.75 milioni kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya kawaida katika sehemu ya Shelui – Ntwike yenye urefu wa kilometa 14.7. Wizara yangu inaendelea kutenga fedha ili kuifanyia ukarabati sehemu ya barabara hiyo, kilometa 7 iliyoharibiwa vibaya kutokana na mvua za *El-Nino.* Kuhusu sehemu ya barabara hiyo inayohudumiwa na Halmashauri ya Wilaya, ninamshauri Mheshimiwa Mbunge kuwasiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ili kupanga kuifanyia matengenezo ama ukarabati barabara hiyo, hivyo kupunguza kero kwa wananchi wa eneo hilo na wale wote waliochagua Serikali hii.

**MHE. JUMA HASSAN KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa amesema barabara hii inahudumiwa na mamlaka mbili tofauti *TANROAD* kutoka Shelui – Ntwike na Halmashauri ya Wilaya kutoka Ntwike – Kiomboi na kwa kuwa eneo la mwisho alilolitaja mamlaka inayohudumia ni Halmashauri ya Wilaya na ndio lenye matatizo makubwa na lina madaraja makubwa. Je, Wizara haioni huruma ikajenga yale madaraja ili kuokoa maisha ya watu kwa sababu Halmashauri haina uwezo wa kujenga eneo lililobakia? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi, sehemu hiyo kwa sasa inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba. Lakini kama ambavyo tumekuwa tukijibu kwamba barabara hizi zinaangaliwa upya ili kujua zipi ziendelee kuwa chini ya Halmashauri za Wilaya na zipi ziwe zinahudumiwa na Wizara ya Miundombinu.

Kwa sasa kwa sababu bado barabara hii iko chini ya Wilaya hiyo, naendelea kumshauri waangalie vyanzo vya kupata hela za kumalizia sehemu hiyo lakini pale ambapo ushauri utatakiwa kutoka katika Wizara yetu, tutakuwa tayari kuangalia namna gani tunaweza kusaidia. Kama kuna maombi maalum, tutayapokea na tutayafanyia kazi kama ambavyo tumekuwa tukisaidia maeneo mbalimbali hata yale yanayohudumiwa na Wilaya.

Na. 202

**Mawasiliano ya Simu za Mkononi**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mawasiliano ya uhakika ni nyenzo mojawapo muhimu katika kusaidia uchumi wa nchi na wananchi kwa ujumla; na kwa kuwa, mtandao wa huduma ya simu za mkononi unaendelea kupanuka hapa nchini katika maeneo mengi ya mijini na vijijini:-

(a) Je, ni vigezo gani vya msingi hutumiwa na kampuni ya simu za mkononi katika kuamua kupeleka huduma katika maeneo ya vijijini?

(b) Kwa kuwa, wananchi wa Tarafa za Dakama na Mweli za Wilaya ya Kahama ni wazalishaji wakubwa wa mazao ya biashara kama pamba na tumbaku.

Je, Serikali itakuwa tayari kuzishawishi kampuni za simu za mkononi hususan *Celtel* kupeleka huduma zake katika maeneo ya Tarafa hizo ili kuwapunguzia adha ya kwenda masafa marefu kutafuta mawasiliano au kupanda juu ya miti ili kupata mwelekeo wa mtandao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Makampuni ya huduma za simu hususani za mkononi huwekeza katika biashara hiyo kwa misingi ya kibiashara, hivyo kipaumbele cha uwekezaji ni katika maeneo yenye *potentials* za biashara na ni lazima maeneo hayo yakidhi pia vigezo vifuatavyo:-

Idadi ya wakazi katika eneo/maeneo yanayolengwa, upatikanaji wa miundombinu mingine kama umeme, mkonga wa mawasiliano, barabara, aina ya shughuli zinazofanywa na wakazi wa maeneo husika na maeneo ambayo Serikali ina mipango ya kupeleka miradi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa mawasiliano ya simu kwa wananchi wake. Hivyo, imekuwa ikiyashawishi makampuni ya simu kupeleka huduma zake maeneo yote ya nchi hii.

Napenda nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kuwa Kampuni ya Simu ya *Tigo* inategemea kufikisha mawasiliano ya simu kwenye Tarafa za Dakama na Mweli ifikapo mwezi Aprili, 2007.

Aidha, kampuni ya simu ya *Vodacom* inategemea kuongezea minara katika maeneo yanayozunguka mji wa Kahama. Kama maeneo aliyotaja Mheshimiwa Mbunge yako umbali usiozidi kilomita 30 kutoka Kahama mjini, yatapata mawasiliano. Vinginevyo watatuma wataalamu kuona namna ya kufikisha mawasiliano kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuyahimiza makampuni mengine ya simu ili yafikishe mawasiliano ya simu kwenye maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa Wilaya ya Kahama ina Majimbo mawili Kahama na Msalala yenye jumla ya takriban wananchi 650,000 na kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Kahama wana uwezo wa kiuchumi hususan kutokana na mazao ya tumbaku, pamba, mpunga na madini ya dhahabu na almasi na kwa kuwa wananchi hawa wametimiza vigezo ambavyo wamevitaja, Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini Serikali itayashawishi zaidi makampuni haya yaone umuhimu wa kuwapatia simu za mkononi wananchi wa Wilaya hii ambayo inachangia kwa kiwango kikubwa pato la uchumi wa nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba tayari Serikali imeshawaomba wawekezaji wa simu za mkononi wafike katika maeneo husika na kama nilivyojibu kwamba tayari *Tigo* imesema itafikisha huduma hizo Aprili mwakani.

Lakini napenda nimhakikishie Mbunge kama atajua *topography* ya Dakama na Mweli ipo baina ya *junction* ya Kahama na Bukombe, Dakama iko kilomita 38 kutoka *junction* hiyo na Mweli iko kilomita 8 kutoka *junction* hiyo lakini ni maeneo ambayo yana milima. Kwa hiyo, kunahitajika kufanya *assissment* ipasavyo ili waone ni *techonogy* gani itafaa katika maeneo yale kwa ajili ya kupeleka huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba juhudi zinafanywa kuona mawasiliano ya simu yanafika vijijini ili yaweze kuchangia uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Tarafa za Mweli na Dakama Wilayani Kahama ni jirani kabisa na Tarafa za Msalala na Nyang'hwale Jimboni Nyang'hwale na kwa kuwa matatizo ya mawasiliano ni yale yale na nilishawasiliana na Mheshimiwa Naibu Waziri awasukume *Celtel* waje wajenge mnara pale Kulumwa Msalala ambapo wameshapata *plot.* Je, Waziri anaweza kuwaambia wananchi wa Msalala, Nyang'hwale ni lini *Celtel* sasa watakuja kujenga mnara huo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba nia ya Serikali ni kuona mawasiliano ya simu yanafika vijijini lakini nimkubushe Mheshimiwa Mbunge kwamba kila kampuni ina *business plan* yake kama *business plan* inasema mwaka huu huduma za mawasiliano ya simu wamepanga kwenda maeneo fulani kutokana na hela walizonazo ndivyo watakavyofanya. Sisi tutaendelea tu kuwasukuma wanaohusika na mawasiliano ya simu waone umuhimu wa kwenda katika maeneo hayo na kama *business plan* za makampuni hayo zinasema Msalala na sehemu nyingine hizo alizozitaja zimo basi watafikisha mawasiliano hayo kwa sababu makampuni ya simu yako hapa kufanya biashara wao wafaidike na sisi tufaidike.

**SPIKA:** Nashauri wengine sasa baadaye muonane na Mheshimiwa Naibu Waziri ili muone *business plan* zao zinasemaje. Tunaendelea.

Na. 203

**Mradi wa Ufungaji Mita za Luku**

**MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa mradi wa ufungaji wa mita za LUKU kwenye Jimbo la Ilala haukukamilika kwenye Kata 5 za Kariakoo, Gerezani, Mchikichi, Ilala na Jangwani; na kwa kuwa, wananchi wengi kwenye maeneo hayo wanalalamika kupewa bili kubwa zinazotokana na mita za zamani:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya kero kubwa wanayopata wananchi wa Jimbo hilo?

(b) Kama Serikali kupitia Shirika lake la umeme *TANESCO* haina uwezo wa kuleta mita hizo za *LUKU* kwa wananchi wa maeneo niliyoyataja. Je, kwa nini Serikali isitoe kibali kwa wafanyabiashara binafsi kuleta *LUKU* hizo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Shirika la Umeme *(TANESCO)* linafunga mita za *LUKU* kwa mteja yeyote anayetaka ili mradi alipe ada ya kubadilisha mita ya shilingi 60,000/= kwa mita ya njia moja (*single phase*) na shilingi 160,000/= kwa mita ya njia tatu (*three phase*). Kwa maelezo zaidi, wananchi hao wafike ofisi za *TANESCO* Ilala.

(b) Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa ushauri wa Mheshimiwa Zungu unaolenga kuipunguzia *TANESCO* mzigo wa kununua mita za *LUKU. TANESCO* huagiza mita hizo kwa njia ya tenda za ushindani *(Competitive Tendering)* ambapo hutangaza zabuni hiyo na mfanyabiashara anayeshinda ndiye anayepewa kazi ya kuleta mita hizo kwa viwango vilivyoainishwa. Tunashauri kama Mheshimiwa Mbunge anawafahamu wafanyabiashara wenye uwezo wa kushiriki kwenye biashara hii awaelekeza *TANESCO* ili wapate taarifa za tenda husika.

**MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, ufungaji wa *LUKU* katika maeneo mengi ya Jimbo la Ilala bado ni matatizo. Kuna visima vya wananchi ambavyo vimechimbwa Kata ya Ilala, Mtaa wa Sharifu Shamba eneo la Mivinjeni mpaka leo hawapati maji kutokana na umeme kutofungwa wakati *TANESCO* imelipwa kipindi kirefu sana.

Je, Serikali itachukua hatua zipi kuhakikisha wananchi hawa wanapata maji upesi sana ili kuhakikisha hawapati maradhi mbalimbali ambayo yanawasibu?

Mheshimiwa Spika, baadhi ya watendaji wa *TANESCO* wanachelewesha kwa makusudi kufunga umeme kwa vigezo kuwa vifaa vya umeme hakuna, je, Serikali itachukua hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kweli kuna maeneo ambako kuna matatizo katika uunganishaji wa umeme.

Ninaomba tushirikiane naye ili kuhakikisha kwamba maeneo hayo ya Ilala ambayo yanapata matatizo ya ufungaji wa umeme yanapatiwa umeme katika kipindi kinachostahili. Naomba tuwasiliane naye ofisini ili tupate majina ya hayo maeneo ili tuyafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watendaji ambao wanachelewesha ufungaji wa mita za umeme na vifaa vingine kutokana na visingizio kwamba vifaa havipo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli baadhi ya maeneo kuna matatizo ya vifaa kutokana na Bajeti ya Kampuni ya *TANESCO.* Lakini kama ikitokea kwamba watendaji wa *TANESCO* wanachelewesha kufunga sio kutokana na suala la kutokuwepo kwa vifaa na kutokana na masuala mengine, naomba atufahamishe majina ya hao watendaji ili tuwashughulikie ipasavyo.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri katika jibu lake la msingi amesema kwamba mtu yeyote anayehitaji *LUKU* aombe kwenye vituo vya *TANESCO* na kwa kuwa matumizi ya *LUKU* yameonyesha kwamba yana manufaa na yameondoa ugomvi kati ya wananchi na *TANESCO* katika kulimbikiziwa bili.

Je, Serikali au *TANESCO* wataleta lini *LUKU* katika Mji wa Singida?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Missanga kwamba ufungaji wa *LUKU* unaondoa manung'uniko, malalamiko na balaa la mabishano ambalo hutokea kuhusiana na bili ambazo wananchi wanaona si sahihi.

Kimsingi, upo mradi wa kufunga *LUKU* nchi nzima kadri fedha zitakavyopatikana. Ndio maana Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anajibu swali, amejibu vizuri sana, amezungumzia utaratibu huu ambapo kama wapo wafanyabiashara ambao wanaweza pia kuingia katika kazi hii ya kuagiza *LUKU* basi wanakaribishwa.

Tatizo ni nini? Tatizo ni kwamba *TANESCO* yenyewe pamoja na kwamba kisera ndiyo mwelekeo ulivyo kuhakikisha kwamba tunaondoa tatizo hili la kutokuwa na bili za uhakika kwa kufunga Luku tatizo ni kwamba fedha hazitoshi na kwa sababu fedha hazitoshi nadhani ni muafaka kwamba sasa milango ifunguliwe kwa watu ambao wanaweza wakaagiza Luku waweze kuagiza Luku inakuwa ni nafuu kwa *TANESCO* lakini pia inakuwa ni nafuu kwa wateja.

Kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Missanga kwamba kwa mji wa Singida tutajitahidi kadri iwezekanavyo tuhakikishie kwa njia hii ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameitaja na pia kwa kupitia *TANESCO* waweze kufunga Luku kwa wakati muafaka.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Swali linalofuata ni Wizara hiyo hiyo, anayefuata ni Mheshimiwa Anastazia Wambura Viti Maalimu.

Na. 204

**Nishati Mbadala**

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Kwa kuwa, yapo machimbo ya gesi ya *Mnazi Bay* huko Mtwara, na kwa kuwa, kuna kasi ya uharibifu wa mazingira hususan misitu kutokana na uchomaji wa mkaa.

Je, Serikali itawezesha lini wananchi wa maeneo ya Kusini kutumia Nishati mbadala ili kupunguza tatizo la ukataji miti?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kuna uharibifu mkubwa wa mazingira katika maeneo mengi ya nchi yetu yanayosababishwa na ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa. Hii inatokana na ukosefu wa nishati mbadala ambayo ni nafuu ukilinganisha na kipato cha wananchi. Aidha, upungufu wa umeme umekua vileivle ni tatizo katika maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza gesi ya *Mnazi Bay,* kama nilivyojibu swali namba 152 la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, katika kikao cha tarehe 5 Julai, 2006 Serikali imeshakamilisha majadiliano na mwekezaji na sasa Wizara inakamilisha kulifikisha suala hili kwenye Baraza la Mawaziri ili kupata ridhaa ya Serikali ya utekelezaji wa mradi wa kutumia gesi ya *Mnazi Bay* katika uzalishaji wa umeme kwa ajili ya Mikoa ya Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, vilevile *TPDC* inafanya utafiti juu ya namna ya kuanzisha miradi mingine kwa ajili ya kuitumia gesi kama nishati kwa matumizi ya nyumbani. Juhudi hizo ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kutumia teknolojia rahisi katika kuwafikishia karibu wananchi wengi gesi kwa ajili ya matumizi yao ya kila siku mfano kupikia, kwa kuanzisha vituo vya kuuzia gesi sawa na vile vya kuuza mafuta ya petroli na vituo vya kupikia hususan kwa kina Mama Lishe.

Aidha, Serikali ya China imeonyesha nia ya kutaka kutupatia mafunzo katika miradi mbalimbali inayotumia gesi asilia kama mali ghafi. Taratibu zitakapokamilika tunategemea kwamba wananchi wengi watafaidika kutokana na miradi hiyo.

**MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, tukitaka kufahamu tu kwamba mradi huu wa gesi wa *Mnazi Bay* ambao utatumika Mtwara na Lindi sasa hivi umefikia hatua gani ya matengenezo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, kama ifuatavyo.

Kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi mradi huu umeshakamilika na kimsingi kinachosubiriwa ni kupeleka waraka kwenye Baraza la Mawaziri ili kupata ridhaa ya Baraza.

**MHE. COL. SALEH ALI FARRAH :** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Je, kuna mipango gani ya kupeleka gesi hii upande wa pili wa Muungano?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kuhusu gesi ya *Mnazi Bay* mradi ule umebuniwa kimsingi kwa ajili ya umeme ya Mikoa ya Kusini na kutegemeana na ongezeko la kiwango cha gesi ile pia gesi ile inaweza kutumika kwa uzalishaji wa umeme kwa nchi nzima kwa maana ya kuunganisha na gridi ya Taifa, na kwa maana ya kuunganisha na gridi ya Taifa basi na kwa sababu Zanzibar inapata umeme kutoka kwenye gridi ya Taifa ni dhahiri kwamba Ndugu zetu wa Zanzibar watanufaika kama ambavyo hivi sasa wananufaika na gesi ya Songosongo katika uzalishaji wa umeme unaopelekwa Zanzibar na hasa tukitilia maanani hivi karibuni Pemba nao wana mradi wa kupeleka umeme kutokea Tanga. Kwa hiyo, kadri Gridi ya Taifa inavyopata umeme mwingi na ndiyo Ndugu Zetu wa Zanzibar watakavyonufaika. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda wa maswali umepitiliza kidogo, na hilo ndilo linanifanya nisimame pia nitoe maelezo kwa sababu kuna Mbunge mmoja ameandika ku-*challenge* kwa nini mara nyingine Spika anaruhusu muda wa maswali unapita anavyoona yeye kwamba tunavunja Kanuni.

Kanuni ya 35(2) inasema swali lolote halitauliza Bungeni baada ya kupita muda wa Saa moja tangu Bunge lilipoanza shughuli za maswali katika mikutano mingine yote baada ya kupita saa moja na nusu.

Waheshimiwa Wabunge Kanuni hii haisemi kwamba muda wa maswali mwisho ni saa nne au saa nne na nusu, inasema ni saa moja au saa moja na nusu. Kwa hiyo, Spika, Naibu Spika au Mwenyekiti wanatumia hekima kama muda wa maswali ambao ni saa moja au saa moja na nusu umemegwa kutoa matangazo ya shughuli nyingine.

Hekima inasema kwamba tafsiri ya Kanuni hapo iwezeshe muda wa saa moja au saa moja na nunu uwe wa maswali. (*Makofi*)

Kwa hiyo, zikipita kama hivi sasa dakika nne siyo kwamba tumevunja Kanuni, tunatumia hekima kuwezesha Kanuni ilivyotaka kwamba maswali kutokana na umuhimu wake na jinsi yanavyowagusa wananchi kwa sababu Waheshimiwa mnauliza kwa niaba ya wananchi hapa basi tusimege muda wa matangazo kwa mfano dakika tano au kumi halafu maswali ndiyo ikabaki dakika 40 au 50 hiyo ndiyo maana ya Kanuni hiyo. (*Makofi*)

Matangazo mengine Kikao cha Kamati ndogo ya Ulinzi na Usalama, naona hawakukutana jana kutakuwepo na Kikao. Mheshimiwa Col. Feteh Saad Mgeni Mwenyekiti wa Kamati ndogo ya Ulinzi na Usalama, anawatangazia Wajumbe kwamba Kamati ndogo ya Ulinzi na Usalama mnaombwa kukutana leo tarehe 13 Julai, 2006 saa 5.00 asubuhi katika Ukumbi Namba 133 ghorofa ya kwanza, Jengo la Utawala. Saa 5.00 asubuhi Ukumbi Namba 133 Kamati ndogo ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Katibu wa Wabunge wa CCM Wanawake. Wabunge Wanawake wa CCM anaomba Wabunge wote Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi, mkutane nje ya Ukumbi kwa maelezo mafupi ya safari ya Dar es Salaam mara baada ya Maswali. Kwa hiyo, mara baada ya maswali Wabunge Wanawake wa CCM wakutane hapo nje ya UKumbi kwa mkutano mfupi sana wa kuelekezana kuhusu safari ya Dar es Salaam.

Waheshimiwa Wabunge nimeendelea kupata maombi haya naona leo niseme, kuna Wabunge nadhani hawa ni Wabunge Vijana wanasema katika kipindi chote cha Bunge la Bajeti *Week end* hapa Dodoma zinakuwa zimedorora, wanaomba tuandae *disco* na dansi siku za *week end* maana yangu ya kulisoma hili siyo kwamba nalikubali nalisoma kwa sababu mambo haya siku hizi yanatawaliwa na uchumi wa soko huria.

Sasa kwa kulisoma hivi vijana wa Dodoma na Vikundi mbalimbali wachangamke ili waweze kuwasaidia Wabunge kupata huduma hii. Huduma hii haiwezi kuandaliwa na Serikali wala haiwezi kuandaliwa na Bunge ni wajasiria mali ndiyo wanatakiwa wachangamkie, ahsante. (*Makofi*)

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Matukio ya Milipuko Kutokana na Matumizi ya Mafuta ya Taa Majumbani

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa ya kuhuzunisha inayohusu matukio ya milipuko katika matumizi ya mafuta ya taa majumbani ambayo yamepelekea baadhi ya Watanzania wenzetu ama kujeruhiwa au kupoteza maisha kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika mwezi Januri na Aprili mwaka 2006 katika maeneo kadhaa ya nchi hususan katika Mikoa ya Arusha, Morogoro na Tanga, Wizara ilipata taarifa za matukio ya watu kufariki dunia na wengine kujeruhiwa vibaya kutokana na kulipukiwa na matufa ya taa wakati wanawasha majiko au taa.

Baada ya kupata taarifa kuhusu milipuko hiyo Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini iliitisha mkutano wa dharura ulioshirikisha wajumbe kutoka Shirika la Maendeleo la Petroli Nchini yaani *TPDC*, Shirika la Viwango *TBS* na Jeshi la Polisi ili kujadili suala hili.

Aidha, kufuatia mkutano huo iliundwa timu ya wataalam kutoka Wizara ya Nishati na Madini, *TPDC*, *TBS* na Polisi ili kufanya uchunguzi wa kina katika maeneo ya matukio na kutoa taarifa pamoja na mapendekezo ya kuzuia matukio kama hayo yasitokee tena.

Mheshimiwa Spika, bada ya uchunguzi kufanyika katika mikoa ya Arusha, Morogoro na Tanga ilibanika kuwa matukio mengi ya milipuko yalitokana na mafuta ya taa ambayo hayakuchanganywa na aina nyingine za mafuta.

Baada ya *TBS* kupima sampuli mbili zilizochukuliwa kutoka Arusha ilionekana kwamba baadhi ya matukio inawezekana yalikuwa na mchanganyiko mdogo wa mafuta aina ya petroli, uchunguzi wa *TBS* umefafanua kuwa inawezekana kuwepo kwa petroli ndani ya mafuta hakukuwa kwa makusudi bali ni kwa bahati mbaya inayotokana na kutumia chombo kimoja kubebea mafuta ya aina mbili kwa nyakati tofauti.

Pia uchunguzi ulionyesha kuwa matukio mengi ya milipuko yalisababishwa na uzembe katika matumizi ya mafuta ya taa kwa maana kwamba mafuta yanayoongezwa kwenye taa au yanayoongezwa kwenye taa bila tahadhari ya kuzima kwanza na vilevile mafuta ambayo hayakuhifadhiwa vizuri.Kufuatia taarifa ya uchunguzi ya timu ya wataalam hatua zifuatazo zinakusudiwa kuchukuliwa na Serikali na kama sulihisho la muda mfupi na muda mrefu wa suala hili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni suala zima la elimu kwa wananchi, Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na Kampuni za Mafuta inaandaa utaratibu wa kuelimisha wananchi na wamiliki wa maduka ya rejareja kuhusu matumizi ya mafuta ya taa na mafuta mengine ya petroli. Elimu hii itatolewa kwa njia ya vyombo vya habari yaani magazeti, redio na televisheni pamoja na vipeperushi.

Pili kupima viwango vya mafuta yanayoingizwa nchini, *TBS* itaendelea kuhakikisha kuwa mafuta yote yanayoingizwa nchini yanapimwa ubora wake na kuthibitishwa kwamba yanafaa kutumika kama yalivyokusudiwa. Aidha, *TBS* wanarekebisha hivi sasa viwango vya mafuta ili kungiza ndani ya vipimo vyao au ndani ya mitambo yao ya kupimia mafuta aina ya rangi au alama za kutambua mafuta katika viwango hivyo, utaratibu huu utaiwezesha *TBS* kufanya ukaguzi wa haraka wa ubora wa mafuta katika maeneo mengi nchini. La tatu ni kudhibiti vyombo vya kusafirishia mafuta. Wizara itashirikiana na wakala wa vipimo pamoja na *TBS* ili kudhibiti ubora wa

meli na magari ya kusafirishia mafuta na kuhakikisha kwamba vyombo hivyo vina ubora ili kuepuka mafuta kuchanganyika yenyewe kwa yenyewe au na maji wakati wa kusafirisha.

Aidha, Serikali inawataka wananchi kuwa waangalifu na kuepuka kutumia chombo kimoja cha mafuta tofauti ili kuondoa uwezekano wa kuchanganya mafuta. La nne ni kudhibiti ubora wa vituo vya mafuta. Serikali inazitaka Halmashauri na Manispaa zote nchini zihakikishe kuwa vituo vyote vinavyopewa leseni za kuuza mafuta ya petroli vina mazingira yanayokidhi masharti ya kufanya biashara hiyo na vituo vilivyo chini ya viwango na hasa vituo vinavyoitwa vituo bubu vivunjwe na wahusika wachukuliwe hatua kwa sababu kwa mazingira yake vituo vya aina hii vinaweza kuhusika katika kuuza mafuta yaliyochini ya viwango. Hatua ya tano ni usajili wa makampuni yenye uwezo. Serikali inafuatilia kwa makini usajili wa kampuni za mafuta ili zile zenye uwezo ndiyo ziweze kusajiliwa kuendelea kufanya biashara ya mafuta na zile ambazo zinatimiza masharti na kanuni zote zinazotakiwa kuzingatiwa katika kuendesha biashara hiyo ndiyo zinafanya biashara hiyo na tunalifanya hili kwa kutilia maanani pia kama kampuni ya Wazalendo pia inashiriki kikamilifu katika biashara hii ya mafuta na haitatolewa kisingizio kwa sababu hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha makampuni makubwa ya mafuta yana wajibu wa kufuatilia na kuhakikisha kwamba vituo vya mafuta vinavyotumia majina yao vina viwango bora vya mafuta yanayouzwa. Seriakali haitasita kuwachukulia hatua au kuyachukulia hatua makampuni makubwa yasiyozingatia ubora wa mafuta. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tayari Serikali inazo taarifa za baadhi ya wananchi wenye magari kupata hasara kutokana na mafuta yasiyo bora yanayouzwa kwenye baadhi ya vituo na hatua tayari zimechukuliwa kwa baadhi ya vituo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa napenda kuchukua fursa hii kuwapa pole wale wote waliofikwa na maafa ama ya kujeruhiwa au kupoteza ndugu zao wakati wakitumia mafuta ya taa. Aidha, naomba pia kutumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Lucy Nkya, Mbunge wa Viti Maalumu, Mkoa wa Morogoro kwa kulifuatilia suala hili kwa umakini na kwa ushirikiano wake kwa Wizara kwenye suala hili. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, mniwie radhi Waheshimiwa Wabunge kuna maonyesho ya kikundi cha akina Mama kinaitwa *Femina Hip* yanafanyika pale katika jengo la Utawala karibu na lango la kuendea Idara ya Habari, pale ambapo tunafanyia shughuli za tafrija. Yatakuwa yanaendelea leo na kesho, inaelekea Waheshimiwa Wabunge hamkuwa na habari. Kwa hiyo, kuna majarida pale ya kuhusu shughuli wanazofanya wanawake hapa Tanzania na yapo machapisho ya kila namna na kwa mujibu wa taarifa hii ni kwamba mambo hayo yote yanaweza kusaidia sana kwa sababu kuna vijarida ambavyo vinaweza kupelekwa hata majimboni, kwenye majimbo ya uchaguzi. Waandalizi wa shughuli hii wanaomba mpite hapo na kuona shughuli zao. *(Makofi)*

Naomba tu nisahihishe Mheshimiwa Kanji niliyemtangaza kwamba ni Meya ya Manispaa sasa nimepata ufafanuzi kwamba ni Naibu Meya, ni pigo kidogo kwa wanaharakati lakini nayo ni hatua. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunmge, ahsante sana. *(Makofi)*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007 Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora, Siasa na Uhusiano wa Jamii.**

**WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, baada ya taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais – Ikulu (Fungu 20 na 30), Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33) na Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94). Naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa lipokee na kujadili mapitio ya shughuli zilizotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2005/2006. Aidha, naliomba pia Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa kazi kwa mwaka 2006/2007 pamoja na Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Rais – Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa uchambuzi wa Bajeti yetu ambao umesaidia sana kuboresha mpango wetu wa kazi kwa mwaka 2006/2007. Naomba pia kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, akisaidiwa na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mbunge wa Igalula, kwa ushirikiano, ushauri na maelekezo mazuri waliyotupatia katika kuboresha Bajeti hii ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Mawaziri ambao wamewasilisha hotuba zao za bajeti kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza kwa ushindi alioupata katika Uchaguzi Mkuu uliopita na kuwa Rais wa Awamu ya Nne ya Serikali ya Muungano wa Tanzania. Pili, kwa kuchaguliwa kwa kauli moja kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Uongozi wake thabiti na imara, umeufanya umma wa Tanzania kujenga imani kubwa kwa Serikali anayoingoza pamoja na kuwapa matumaini ya maisha bora, ushirikiano na umoja wa utaifa wetu.

Kauli mbiu aliyoichagua ya: Ari mpya, Nguvu mpya na Kasi mpya, imekuwa ni kirutubisho na changamoto katika utendaji wa kazi. Tunamwomba Mwenyezi Mungu amjalie afya njema na kumwongezea hekima na maarifa katika kuliongoza Taifa letu.

Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar. Pia, nampongeza Mheshimiwa Edward Ngoyayi Lowassa, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu na hatimaye kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kwa kura nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwapongeza Wajumbe wa Sekeretarieti ya Halmashauri Kuu walioteuliwa hivi karibuni, wakiongozwa na Katibu Mkuu wa CCM, Mheshimiwa Yusuph Makamba, Mheshimiwa Jaka Mwambi, Naibu Katibu Mkuu (Bara), Mheshimiwa Rostam Aziz , Mweka Hazina, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Katibu wa Itikadi na Uenezi, Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro, Katibu wa Siasa na Uhusiano wa Kimataifa na Mheshimiwa Kidawa Hamisi, Katibu wa Oganaizesheni.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukupongeza wewe mwenyewe, kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge hili Tukufu katika Awamu hii ya Nne ya Serikali ya Muungano wa Tanzania. Kuchaguliwa kwako ni ushahidi tosha wa jinsi unavyoaminika na kutambulika kwa Waheshimiwa Wabunge na jamii ya Kitanzania kwa ujumla. Tunakuahidi kukupa ushirikiano wetu wa dhati ili kukuwezesha kutekeleza dhamana uliyopewa ya kusimamia demokrasia ndani ya Bunge hili na kulifanya litukuke ndani na nje ya nchi yetu. Napenda pia, kumpongeza Mheshimiwa Anna Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa na kuteuliwa kuwawakilisha wananchi ndani ya Bunge hili Tukufu.

Aidha, naomba kutumia nafasi hii binafsi na kwa niaba ya Mawaziri wenzangu, Mheshimiwa Philip Sang'ka Marmo na Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, kuwashukuru wananchi wa Majimbo ya Mtwara Vijijini na Mbulu kwa kutuchagua kuwa wawakilishi wao katika Bunge hili, na hatimaye kupata heshima ya kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa za Mawaziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora, Siasa na Uhusiano wa Jamii.

Aidha, kwa namna ya pekee, naomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Mtwara Vijijini, kwa kunichagua na kuniwezesha kuwa Mbunge wa kwanza mwanamke tangu kuanzishwa kwa jimbo hilo, na hivyo kuongeza idadi ya Wabunge Wanawake Bungeni.

Mheshimiwa Spika, tunaomba pia kutumia fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyayi Lowassa, Mbunge wa Monduli, kwa hotuba aliyoitoa, ambayo imetoa dira ya shughuli za Serikali katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007. Maelezo ya Hotuba yake yanalenga kutafsiri ya Kauli Mbiu ya Awamu ya Nne ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: "Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya", katika vitendo na hivyo kuwazidishia wananchi matumaini ya maisha bora na amani nchini. *(Makofi)*

Pia, tunapenda kuwapongeza Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Waziri wa Fedha, na Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kwa hotuba zao ambazo zimetoa maelezo yanayobainisha misingi na mwelekeo wa bajeti na uchumi wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu itazungumzia mapitio ya utekelezaji na mafanikio ya shughuli za Ofisi ya Rais – Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma za mwaka 2005/2006; maelezo ya mpango wetu wa mwaka 2006/2007 pamoja na maombi yetu ya fedha za kuutekelezea mpango huo.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuwasilisha bajeti ya Ofisi ya Rais - Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma mwaka jana tuliahidi kutekeleza mambo kadhaa ambayo ninaomba kuyatolea taarifa ya utekelezaji na mafanikio yaliyopatikana hadi kufikia Juni, 2006 kama ifuatavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 Ofisi ya Rais, Ikulu iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kuongoza, kufuatilia, kuratibu uendeshaji bora wa Serikali na kusimamia utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa na Rais na Baraza la Mawaziri, na ifuatayo ni taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na mafanikio yake kwa kipindi hicho.

(a) Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri 31 na Wakuu wa Idara 19 kutoka Wizara zote walipatiwa mafunzo juu ya uandaaji wa nyaraka za Baraza la Mawaziri. Aidha, watumishi 150 walipatiwa mafunzo ya Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi (*Open Performance Review and Appraisal System*). Watumishi 60 waliwezeshwa kuhudhuria masomo ya sekondari, wengine 50 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi kama sehemu ya mafunzo ya kujiendeleza kazini. *(Makofi)*

(b) Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilijadili nyaraka 54, Kamati ya Makatibu Wakuu (*Inter-Ministerial Technical Committee (IMTC)* nyaraka 56 na nyingine 53 zilijadiliwa na kutolewa maamuzi na Baraza la Mawaziri.

(c) Sera ya Mawasiliano ya Serikali kwa umma ilikamilishwa katika kipindi hicho. Sera hiyo itawezesha kuwepo kwa taratibu na mfumo wa mawasiliano baina ya Serikali na wananchi kwa ujumla.

(d) Jumla ya rufaa na malalamiko 570 yanayohusu watumishi wa umma yaliyowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais na kwa Katibu Mkuu Kiongozi yalishughulikiwa. Aidha, Mkakati wa kuboresha utaratibu wa kushughulikia rufaa na malalamiko ya watumishi wa umma umeandaliwa na umeanza kutekelezwa katika kipindi hiki.

(e) Ujenzi wa nyumba ya makazi ya Rais ulioanza mwezi Februari, 2006 unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2007. Aidha, ukarabati wa jengo la Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, jengo litakalotumika kama Ofisi ya Idara ya Mawasiliano kwa Umma pamoja na jengo la makazi ya Katibu Mkuu Kiongozi umeanza na utakamilika katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2006/2007.

(f) Waratibu thelathini na sita (36) wa Mkakati wa Kuzuia Rushwa katika Wizara na Idara za Serikali wamepatiwa mafunzo juu ya Mkakati wa Kupambana na Rushwa. Aidha, wajumbe wa Kamati za Maadili katika Wizara wamepatiwa mafunzo juu ya wajibu wao kama wajumbe wa Kamati hizo.

(g) Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa umefanyiwa mapitio na mpango wa Awamu ya Pili ya kutekeleza mkakati huo katika kipindi cha 2006-2010 umeandaliwa.

(h) Kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Mkakati dhidi ya Rushwa katika Wizara, Idara na Wakala wa Serikali na kutoa taarifa za kila robo mwaka za utekelezaji huo.

(i) Washiriki 60 kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali wamepatiwa mafunzo kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Kupambana na Rushwa ikiwa ni hatua ya kuwaelimisha waweze kushiriki ipasavyo dhidi ya vita ya rushwa

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria Na 16 ya mwaka 1971, TAKURU ina jukumu la kuelimisha umma maana ya rushwa na athari zake katika jamii na mbinu za kupambana na rushwa, juu ya athari ya kutoa na kupokea rushwa nchini, Kuchunguza tuhuma mbalimbali na kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria wote wanaothibitika kujihusisha na vitendo vya rushwa na kuishauri Serikali na Taasisi mbalimbali juu ya njia sahihi za kuziba mianya ya rushwa katika maeneo yao. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2005/2006 TAKURU ilitekeleza mambo yafuatayo:

(a) Kuendelea na uchunguzi wa tuhuma 3,463 zilizokuwepo pamoja na tuhuma mpya 1,126 zilizopokelewa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2005/2006. Majalada 2,285 ya uchunguzi yalishughulikiwa na kukamilika na hatua mbalimbali kuchukuliwa kulingana na ushahidi uliopatikana. Aidha, mashauri mapya 77 yalifikishwa mahakamani. Jumla ya watumishi wa Serikali 225 walichukuliwa hatua za kinidhamu. Majalada 519 yalishughulikiwa na baadaye kuhamishiwa Idara zingine zikiwemo Polisi, Mahakama na vyombo vingine kwa vile hayakuhusiana na makosa ya rushwa.

(b) Jumla ya kesi 265 ziliendeshwa mahakamani ambapo kesi 70 zilitolewa maamuzi. Kati ya hizo kesi 12 washitakiwa walifungwa, kesi 25 washitakiwa waliachiwa huru, kesi 2 zilihamishiwa Polisi, kesi 25 ziliondolewa mahakamani kwa sababu mbalimbali na kesi 6 Serikali imekata rufaa Mahakama Kuu. Hadi sasa kesi 195 zinaendelea mahakamani. *(Makofi)*

(c) Kuendelea na uchunguzi wa matumizi ya fedha za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na tuhuma zilizohusu mtandao wa watumishi wa

Halmashauri za Wilaya, TAMISEMI, Wizara ya Elimu na Hazina katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Uchunguzi huo katika baadhi ya Mikoa umebaini kuwepo kwa ubadhirifu wa fedha za Serikali hivyo majalada husika yanaendelea kufanyiwa uchambuzi wa kisheria ili kuwafikisha watuhumiwa mahakamani.

(d) Tafiti 11 zilizohusu Taasisi za Umma na Binafsi zilifanyika na maeneo yaliyohusika ni, uchaguzi katika Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu, ajira za wafanyakazi, sekta binafsi, vyeti bandia na ajira za walimu, wawekezaji, udhibiti wa dawa, vipodozi na chakula, hali ya rushwa nchini na tafiti kuhusu zabuni katika sekta ya umma.

(e) Kutoa mafunzo kwa watumishi ambapo watumishi wapya 154 walihudhuria mafunzo ya awali ya uchunguzi, wachunguzi 150 walihudhuria mafunzo ya awali ya wiki mbili na wachunguzi 50 walihudhuria mafunzo ya kati.

(f) Katika kukabiliana na tatizo la vitendea kazi, TAKURU ilinunua magari 120, na jenereta 20 kwa ajili ya maeneo yasiyo na huduma ya umeme. Aidha, majengo manne (4) kwa ajili ya ofisi za TAKURU za Wilaya na matatu (3) kwa ajili ya ofisi za mikoa yalinunuliwa.

(g) Kushiriki katika maonyesho na maadhimisho mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa ambapo wananchi walitembelea banda na kupata maelezo na ufafanuzi kuhusu shughuli za TAKURU. Aidha, TAKURU iliandaa midahalo iliyowashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge.

(h) Kuelimisha umma kupitia vipindi vya redio, televisheni, mikutano ya hadhara, midahalo na machapisho, vyote vikiwa na lengo la kuwashirikisha wananchi kwa karibu katika mapambano dhidi ya rushwa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* ina jukumu la kushirikisha vikundi vya jamii, kuainisha, kuchambua matatizo/mahitaji na kukusanya rasilimali kwa ajili ya maendeleo endelevu katika ngazi za Vijiji, Shehia na Wilaya. Katika mwaka *2005/2006 TASAF* ilitekeleza yafuatayo:

(a) Kuhamasisha umma kuhusu awamu ya pili ya *TASAF* kupitia vipindi vya radio, televisheni, makala katika magazeti na vipeperushi.

(b) Kuandaa miongozo ya utekelezaji wa Awamu ya Pili ya *TASAF* katika ngazi za Halmashauri za vijiji, Wilaya, Manispaa, Jiji na Kamati za Miradi na kuitafsiri miongozo hiyo kwa lugha ya Kiswahili.

(c) Kuandaa utaratibu wa kufanya tathmini ya *TASAF* kupitia Mfumo wa Tathmini ya Hali ya Umaskini ambao pia unatumika katika MKUKUTA

(d) Kununua vifaa/vyombo kama magari, kompyuta na mashine za kutolea vivuli; ambavyo vinaendelea kusambazwa katika Halmashauri zote nchini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi.

(e) Kuendesha mafunzo kuhusu awamu ya pili ya *TASAF* kwa wataalam na viongozi katika mamlaka zote za miji na Wilaya, Tanzania Bara na Visiwa vya Unguja na Pemba kwa lengo la kujenga uelewa wa pamoja juu ya muundo, mfumo wa utekelezaji na majukumu ya kila mhusika katika utekelezaji wa Awamu ya Pili ya *TASAF*. Jumla ya watendaji 1,400 wamenufaika na mafunzo hayo.

(f) Kufanya semina kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, na Naibu Makatibu Wakuu juu ya muundo wa Awamu ya Pili ya *TASAF*.

(g) Kuwawezesha wataalam katika Halmashauri zote kuendesha mafunzo kwenye maeneo yao (Vijiji, Mitaa na Sheria) kwa lengo la kuziwezesha jamii kuibua, kutekeleza na kusimamia miradi.

Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ina jukumu la kuandaa mfumo wa kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji biashara utakaoainisha biashara na kuboresha maisha ya watanzania. Katika mwaka 2005/2006 Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania ulitekeleza kazi mbalimbali kama ifuatavyo.

(a) Kukamilika kwa Tathmini ya sekta isiyo rasmi ambayo taarifa yake ilikabidhiwa rasmi kwa Rais wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, mnamo tarehe 5 Oktoba, 2005. Taarifa ilibainisha mtandao, thamani ya sekta isiyo rasmi, kanuni na taratibu zitumiwazo na wadau kumiliki mali na kufanya biashara nje ya mfumo rasmi wa sheria. Aidha, taarifa ya tathmini iliyofanyika iliainisha vikwazo vya kisheria vinavyowazuia Watanzania walio wengi kuzingatia sheria kikamilifu wafanyapo biashara na katika kumiliki mali hususani ardhi na majengo.

(b) Uhamasishaji wa viongozi katika ngazi mbalimbali juu ya malengo na madhumuni ya MKURABITA wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la 2000 – 2005, Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, na Waheshimiwa Mabalozi wetu nchi za nje.

Aidha, walengwa na watendaji wakuu walihamasishwa kupitia warsha mbalimbali kwa wafanyabiashara ndogondogo na kati juu ya shughuli za MKURABITA. Jumla ya warsha 8 zilizohusisha washiriki 520 zilifanyika. *(Makofi)*

(c) Utaratibu wa kuanzisha Tovuti (*Website*) umeanza na unategemewa kukamilika mapema mwezi Agosti 2006.

(d) Maandalizi ya taratibu za ushirikiano wa Wizara na Taasisi za Serikali zinazoweza kufanya shughuli kwa ushirikiano na MKURABITA umeanza na unategemewa kukamilika mwishoni mwa mwezi Julai.

(e) Mpango Kazi (*work plan*) kwa ajili ya hatua ya pili ya shughuli za Mpango (*Reform Design Stage*) umekamilika na kuidhinishwa. Aidha, hatua ya pili yaani Maandalizi ya Maboresho imeshaanza rasmi na inategemewa kukamilika mwezi Oktoba 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jukumu kubwa la Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni kuimarisha utawala bora katika uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa kubuni Sera, Sheria, Kanuni na taratibu za uendeshaji na usimamizi wa shughuli za utumishi wa umma, kujenga uwezo wa watumishi wa umma ili watoe huduma bora kwa wadau wake. Katika kufanikisha majukumu haya, maeneo yanayopewa kipaumbele ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuhakikisha kwamba watumishi wa umma wanafanya kazi kwa uaminifu, uadilifu na kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.

(b) Kuhakikisha kuwa watumishi wa umma wanaoajiriwa wana ujuzi na vipaji vya hali ya juu, na kwamba ujuzi huo unaendelezwa kukidhi mabadiliko ya kisasa.

(c) Kuhakikisha kuwa watumishi wanapimwa utendaji kazi wao na kutuzwa kufuatana na viwango vya ustadi na ufanisi wao, na kwamba kuna mazingira mazuri ya kazi ambapo sheria na kanuni zinatumiwa kwa haki na usawa.

(d) Kuhakikisha kwamba mifumo ya taarifa na mawasiliano ya habari inaimarishwa Serikalini na inatumiwa kutoa taarifa katika kufanya maamuzi.

(e) Kuhakikisha kwamba Wizara, Idara Zinazojitegemea na Mikoa zinajishughulisha na majukumu mahsusi ya Serikali ambayo yanaendeshwa kwa gharama nafuu.

(f) Kuwa na utumishi wa umma unaojali wateja na kuhakikisha wananchi wanaarifiwa vilivyo kuhusu huduma wanazotarajia kuzipata Serikalini na fursa ya kutoa maoni, ushauri au malalamiko.

(g) Kuweka mifumo ya kuboresha utendaji kazi katika utumishi wa umma ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinalingana na gharama zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kukamilisha uwekaji wa Mifumo ya uboreshaji utendaji kazi *(Performance Management Systems (PMS)* katika Mikoa ishirini na moja (21) ya Tanzania Bara. Kutokana na zoezi hilo Mikoa yote hivi sasa ina Mipango Mkakati na Mikataba ya Huduma kwa Mteja. Matarajio ni kuwa, watumishi wataanza kupimwa utendaji kazi kwa kutumia Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi *(Open Performance Review and Appraisal System (OPRAS).* Aidha, Wizara kumi na tano (15) zilizoundwa katika serikali ya awamu ya nne ziliwezeshwa kuandaa Mipango Mkakati. *(Makofi)*

(b) Wakala wa Serikali tano (5) zimeanzishwa ambazo zinafanya idadi ya Wakala zilizokwishaanzishwa kufikia ishirini na nne (24). Aidha, Wakala hizo zimeendelea kuimarishwa kwa kuziwezesha kuwa na mifumo ya kompyuta kwa ajili ya utunzaji wa kumbukumbu mbalimbali na kuzipatia vitendea kazi kwa lengo la kuboresha mazingira ya utendaji kazi. Katika kipindi hicho, mchakato wa kuziwezesha Idara nyingine sita (6) katika Wizara mbalimbali kuwa Wakala umeanza.

(c) Mafunzo ya Upembuzi Yakinifu, Upatikanaji wa wazabuni *(procurement),* na usimamizi wa mikataba ya huduma kwa Wizara 11, Idara Zinazojitegemea 3, Wakala za Serikali 8, na Mkoa mmoja, pamoja na Hospitali moja ya Mkoa yamekamilika. Hatua hii ni muhimu katika mpango wa kushirikisha Sekta Binafsi kutoa huduma kwa umma.

(d) Miundo ya Wizara na Ofisi kumi na tisa (19) iliandaliwa kwa Wizara zilizoundwa upya katika Serikali ya Awamu ya Nne. Aidha, Wizara, Ofisi na Idara Zinazojitegemea ishirini na moja (21) zimewezeshwa kuandaa orodha ya Nafasi za Kazi kwa lengo la kutambua mahitaji halisi ya watumishi.

(e) Sera ya mafunzo katika utumishi wa umma imeandaliwa na inatarajiwa kuanza kutumika rasmi katika mwaka huu wa fedha. Aidha, viongozi na maofisa waandamizi 2,300 wamepatiwa mafunzo mbali mbali ambayo yamewawezesha kuongeza ujuzi wa kazi na mbinu za uongozi. *(Makofi)*

(f) Kituo cha Tanzania cha Mafunzo ya Maendeleo kwa Mtandao (*Tanzania Global Development Learning Center (TGDLC)* kiliwawezesha viongozi, wanasiasa na wasomi mbali mbali kufaidika na teknolojia ya mawasiliano kwa mtandao ambapo walipata taarifa mbali mbali za maendeleo na mafunzo wakiwa hapa hapa nchini.

(g) Chuo cha Utumishi wa Umma kimeimarishwa kwa kukiongezea majengo, vitendea kazi na watumishi wenye sifa na uwezo mkubwa. Pia kimewezeshwa katika kuanzisha ushirikiano na vyuo vingine ndani na nje ya nchi k.m. *ESAMI, INTAN* cha Malaysia na *CSS* cha Singapore, kwa ajili ya kutoa mafunzo mbali mbali ya Uongozi, Utawala na Menejimenti kwa watumishi wa ngazi zote.

(h) Kuwezesha Wizara kumi kutumia teknolojia mpya katika kusimamia mfumo wa uendeshaji na ulipaji mishahara.

(i) Kuwezesha Wizara na Idara Zinazojitegemea kuandaa Mikakati ya Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji (*Management Information System Strategy*). Hadi kufikia Juni 2006 Wizara tatu zilikuwa zimekamilisha maandalizi ya mikakati yao na kuanza utekelezaji.

(j) Ujenzi wa jengo la Serikali-Mtandao *(Network Management Center)* umeanza na unatarajiwa kukamilika Februari 2007. Jengo hili litatumika kufunga vifaa vya Serikali-Mtandao pamoja na kuwa kitovu cha mawasiliano Serikalini.

(k) Zoezi la kuhuisha kumbukumbu muhimu za kiutumishi kwa kuzihifadhi katika mfumo wa ki-elektroni limekamilika katika Wizara tano (5) na Idara inayojitegemea moja .

(l) Mkakati wa kuongeza idadi ya wanawake katika nafasi za uongozi kutoka asilimia 30 mwaka 2005 hadi kufikia asilimia 50 mwaka 2010 uliandaliwa. Mkakati huu una lengo la kuleta usawa kwa wanawake na wanaume katika nafasi za maamuzi.

(m) Katika mwaka wa fedha 2005/2006 watumishi 194 kutoka Wizara, Idara za Serikali Zinazojitegemea na Taasisi za Serikali walipatiwa mafunzo ya utawala na usawa wa jinsia.

(n) Kuendelea kuhakiki orodha ya malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa malipo yanayofanywa na waajiri mbalimbali kwa nia ya kupunguza ubadhirifu wa fedha za umma.

(o) Kushughulikia malalamiko ya watumishi kuhusiana na utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni na Taratibu kwa madhumuni ya kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika utumishi wa umma.

(p) Kutoa na kuratibu vibali vya ajira mpya, mbadala, uhamisho, likizo bila malipo na watumishi wanaoazimwa kwa madhumuni ya kusimamia matumizi bora ya wataalamu waliopo, kudhibiti ubadhirifu wa malipo ya mishahara hususani ajira hewa na kulinda maslahi ya watumishi mbali mbali wanaohama kuingia katika utumishi tofauti na ule walionao.

(q) Kuendesha warsha kwa ajili ya Wakurugenzi wa Utawala na Utumishi na Makatibu Tawala wa Wilaya kwa madhumuni ya kuwajengea uwezo katika masuala ya utawala na utumishi pamoja na uboreshaji wa utendaji katika utumishi wa umma.

(r) Kuendelea kutoa huduma kwa Viongozi wa Kitaifa Wastaafu pamoja na Wajane wa Viongozi kulingana na Sheria ya Hitimisho la Kazi kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa Namba 3 ya mwaka 1999 ikisomwa kwa pamoja na Sheria ya Marekebisho Namba 11 ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni chombo kikuu kinachohusika na kujenga imani ya wananchi kuhusu uadilifu wa viongozi wa umma, imeendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Namba 13 ya mwaka 1995.

Katika mwaka wa fedha 2005/2006 jumla ya Viongozi wa Umma 6,239 walitumiwa Fomu za Tamko la Mali na Madeni. Hadi kufikia Mei, 2006 ni viongozi 2963 tu walikuwa wametoa tamko la mali na madeni. Aidha, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imefanya uchunguzi wa awali wa malalamiko 78 ya wananchi dhidi ya viongozi wa umma waliotuhumiwa kukiuka maadili ya viongozi.

Mheshimiwa Spika, katika kuelemisha umma kuhusu maadili ya viongozi vipindi 155 vilitangazwa kwenye vyombo vya habari. Aidha, makala, kalenda na vipeperushi yalichapishwa na kusambazwa kwa viongozi wa umma na wananchi.

Mheshimiwa Spika, ofisi sita (6) za Kanda ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Tabora, Mwanza na Mtwara zimefunguliwa. Kukamilika kwa Ofisi hizi kutarahisisha kwa kiwango kikubwa kushughulikia masuala ya maadili ya viongozi wa umma pamoja na malalamiko ya wananchi dhidi ya Viongozi. Aidha, ili kukidhi mahitaji ya Ofisi hizo, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeajiri watumishi wapya 23 na kuwapatia mafunzo ya kazi ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa kazi na majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Umma inao wajibu wa kuhakikisha kwamba masuala yote ya Utumishi yanaendeshwa kwa Mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa Ajira katika Utumishi wa Umma inazingatia sifa, uwezo na ushindani kwa madhumuni ya kufanikisha utendaji wenye malengo na matokeo yanayopimika. Katika kipindi cha 2005/2006 Tume imetekeleza majukumu kama ifuatavyo:

(a) Kutoa Mwongozo kuhusu Mashauri ya Nidhamu, Rufaa, na taarifa za kuwasilisha Tume.

(b) Kutoa mafunzo kwa wadau 10 wa makundi mbalimbali kwa madhumuni ya kuziwezesha Mamlaka za Ajira za Nidhamu kutekeleza Majukumu yake.

(c) Kusajili walimu 5938 ambapo wanaume ni 2937 na wanawake 3001.

(d) Kuthibitisha kazini walimu 2807 ambapo 1470 ni wanawake 1337 ni wanaume.

(e) Kushiriki katika vikao vya Bodi za Ajira za Halmashauri 5, Kamati Maalum za Wizara na Idara Zinazojitegemea 48, na Kamati za Mikoa na Wilaya 10.

(f) Kushughulikia mashauri ya nidhamu 230 katika vikao 4 vilivyofanyika kwenye Idara ya Utumishi wa Walimu.

(g) Kutolea maamuzi rufaa 61 na hatimaye kuwajulisha warufani husika.

(h) Kuitangaza Tume ya Utumishi wa Umma kwa njia ya ziara Mikoani, kusambaza vipeperushi, vijarida, kalenda na fulana kwa waajiri na wadau mbalimbali, na kuelimisha umma kupitia vyombo vya Habari kuhusu Majukumu ya Tume.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Ikulu itaendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za serikali na kufanya uchambuzi wa masuala mbali mbali ya kisera na miswada ya sheria. Kazi nyingine zitakazofanywa ni pamoja na:

(a) Kuandaa Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Mawasiliano ya Serikali kwa Umma na kutoa ufafanuzi wa masuala mbali mbali ya kiserikali kwa wananchi.

(b) Kutoa mafunzo mbali mbali kwa watumishi kwa ajili ya kuboresha utendaji wao wa kazi na kusimamia shughuli za uendeshaji wa ofisi.

(c) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kupambana na UKIMWI mahali pa kazi.

(d) Kuimarisha utaratibu wa kupima matokeo ya utendaji kazi kwa uwazi kwa kuhakikisha kuwa watumishi wote wa Ikulu wamepatiwa mafunzo ya Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi *(Open Performance Review and Appraisal System).*

(e) Kuendelea kufanya uchambuzi wa nyaraka na kutoa ushauri kwa Wizara juu ya uandishi wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na kuendelea kuhudumia Kamati ya Makatibu Wakuu *(IMTC)* na Baraza la Mawaziri na Kamati zake.

(f) Kushughulikia rufaa za watumishi wa umma zinazoletwa kwa Rais na kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

(g) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Awamu ya pili wa Mkakati wa Kupambana na Rushwa ambao katika kipindi hiki utahusisha Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majiji yote nchini.

(h) Kuratibu utekelezaji wa mradi wa Kuimarisha Uwajibikaji, Uwazi na Uadilifu katika utendaji wa umma (*Accountability, Transparency and Integrity Programme*) wenye lengo la kuziimarisha taasisi zote zinazosimamia masuala ya Maadili na Utawala Bora.

(i) Kuendelea kutoa machapisho yanayohusu taarifa za utekelezaji wa mipango ya Utawala Bora na hatua zinazochukuliwa katika kupambana na rushwa. Machapisho haya hutolewa kila robo mwaka.

(j) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa programu ya Kuimarisha Taratibu na Utawala Bora ili kupambana na rushwa.

(k) Kuhakiki na kufuatilia utekelezaji wa mpango wa pili wa Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa ili kwenda sambamba na utekelezaji wa programu zingine za Utawala Bora kama vile Maboresho katika Sekta ya Fedha, Maboresho katika Sekta ya Umma, Maboresho katika Serikali za Mitaa na MKUKUTA.

(l) Kuendelea kuratibu masuala ya siasa na mahusiano ya jamii.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU) imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo katika kipindi cha mwaka 2006/2007:

(a) Kuendelea na uchunguzi wa tuhuma 2,304 zilizopo na zingine zitakazopokelewa.

(b) Kuendelea na uendeshaji wa kesi 195 zilizopo mahakamani na zingine zitakazofunguliwa kipindi hicho.

(c) Kuendelea na uchunguzi wa matumizi ya fedha za MMEM ambao hadi sasa umebaini kuwepo kwa ubadhirifu wa kiasi cha shilingi 2.6 bilioni kati ya shilingi 241.9 bilioni zilizotolewa na Serikali pamoja na Wafadhili.

(d) Kuongeza kasi ya uchunguzi wa rushwa kubwa katika maeneo yafuatayo:-

(i) Mikataba mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa.

(ii) Taratibu za uingizaji madawa ya binadamu na ya mifugo.

(iii) Ununuzi mkubwa unaofanywa na serikali na Taasisi zake.

(iv) Mazingira na Maliasili;

(v) Matumizi ya fedha za serikali na wafadhili katika miradi mbalimbali nchini.

(vi) Uwekezaji katika sekta mbalimbali.

(vii) Viongozi wa serikali wanaodaiwa kujilimbikizia mali zisizoendana na kipato chao halali pamoja na maeneo mengine yanayoonekana kuiathiri nchi katika rushwa kubwa kubwa.

(e) Kuongeza uwazi zaidi kwa kuwajibu wananchi juu ya malalamiko wanayowasilisha TAKURU ndani ya mwezi mmoja sambamba na kutoa taarifa za kiuchunguzi zinapokamilika kwa vyombo vya habari.

(f) Kutokana na ongezeko la ofisi za TAKURU kutoka ofisi 21 hadi 141, TAKURU itaajiri watumishi wapya 250 kuanzia mwezi Julai 2006 ili kuweza

kumudu wingi wa tuhuma zinazopokelewa na kukisogeza chombo karibu zaidi na wananchi. Aidha, TAKURU itakamilisha ufunguzi wa ofisi 16 za Wilaya zilizobaki.

(g) Kutoa mafunzo kwa watumishi 360 ili watumishi waweze kuendana na mabadiliko ya jamii na mbinu mpya wazitumiazo wala rushwa.

(h) Kuendelea kuelimisha, kufahamisha na kuhamasisha wananchi juu ya haki zao, madhara ya rushwa na jinsi ya kupambana na kujiepusha na vitendo vya rushwa. Aidha, uelimishaji huu utafanyika kwa njia ya radio, televisheni, machapisho mbalimbali na kupitia midahalo ya wazi ili kuwashirikisha wananchi wengi zaidi.

(i) Kufanya tafiti 48 zitakazohusu sekta za umma na binafsi. Lengo likiwa ni kuongeza kasi ya kupambana na rushwa kwa kuziba mianya iliyobainika katika maeneo husika. Vigezo vitakavyotumika katika kuchagua maeneo ya kufanya tafiti ni wingi wa malalamiko yatakayopokelewa.

(j) Ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika tafiti mbalimbali utafanyika. Warsha 24 zitafanyika ili kujadiliana na wadau kuhusu njia bora za kuhakikisha maazimio ya kuziba mianya ya rushwa yanatekelezwa.

(k) Kukamilisha marekebisho ya Sheria Kuzuia Rushwa Namba. 16 ya mwaka 1971.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* awamu ya pili itaendelea kushirikiana na jamii katika kuainisha kero zao, kuweka vipaumbele, kutekeleza, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ili kuboresha hali yao ya maisha.

Hivyo ni matarajio kuwa mafanikio makubwa yatapatikana katika harakati nzima ya kupambana na umaskini kupitia dhana ya ushiriki wa jamii. Ufadhili wa *TASAF* utaelekezwa katika kuboresha huduma za jamii, kutoa ajira kwa kaya zenye upungufu wa chakula, na miradi ya kuongeza kipato kwa watu wa makundi maalum wakiwemo watoto yatima, wazee, walemavu, waishio na virusi vya UKIMWI na wajane.

Mheshimiwa Spika**,** katika mwaka 2006/2007 *TASAF* imepanga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kushirikiana na jamii, Halmashauri na Ofisi ya Waziri Kiongozi kwa upande wa Unguja na Pemba ili kuhakikisha kuwa miradi ambayo haikukamilika katika Awamu ya Kwanza ya *TASAF* inakamilishwa.

(b) Kuwafikia wananchi wote wa Tanzania na kuendelea kutoa mafunzo kuhusu taratibu za utekelezaji wa miradi itakayofadhiliwa na *TASAF.*

(c) Kuimarisha usimamizi ili kuhakikisha kuwa miradi yote inatekelezwa kama ilivyotarajiwa.

(d) Kujenga uwezo na uelewa wa wananchi kuhusu suala zima la utekelezaji wa miradi kwa lengo la kuwa na miradi endelevu, na kuimarisha dhana ya umiliki wa jamii na kuifanya jamii itambue kuwa miradi hiyo ni mali yao na kwa ajili ya maendeleo yao.

(e) Kufadhili jumla ya miradi 1,800 nchi nzima. Aina ya miradi inayotarajiwa kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa barabara, madaraja, madarasa, zahanati, nyumba za walimu na waganga, visima vya maji, masoko, upandaji miti na miradi ya kuongeza kipato kwa watu wa makundi maalum.

(f) Kusimamia utaratibu unaowezesha taasisi mbalimbali kupitishia fedha TASAF kwa ajili ya malengo maalum (*Ring-fenced facility*). Utaratibu huo hadi sasa unanufaisha miradi ya *Marine and Coastal Environmental Management Programme (MACEMP)* na *Participatory Forest Management (PFM).* Aidha, Kamisheni ya UKIMWI Zanzibar *(ZAC)* inapitisha fedha *TASAF* kwa ajili ya miradi ya UKIMWI inayotekelezwa katika visiwa vya Unguja na Pemba, na *OPEC* kwa ajili ya utekelezaji wa miradi inayoibuliwa na wananchi katika mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania utaendelea kutekeleza shughuli za awamu ya Pili ya kuandaa maboresho (*Reform Design Stage*) kama ifuatavyo:-

(a) Kufanya utafiti wa kina katika wilaya 26 za Tanzania Bara na katika visiwa vya Unguja na Pemba na kuandaa mapendekezo ya awali ya maboresho ya sheria na kanuni zitumikazo katika sekta isiyo rasmi ili ziwe sehemu muhimu za mfumo mpya unaokusudiwa. Aidha, mawasiliano na wadau yatafanyika ili kukamilisha rasimu za awali za maboresho.

(b) Kutoa mafunzo kwa wataalamu wa kitanzania takriban ishirini (20) watakaohusika katika mchakato wa kutengeneza sheria ili kuhakikisha umiliki na ushiriki wa Tanzania katika kutengeneza sheria husika. Aidha, MKURABITA itatoa mapendekezo ya marekebisho yanayohitajika katika sheria za sasa za umiliki mali ili ziunganishwe na kanuni za jamii zilizoboreshwa kupata mfumo mpya unaokusudiwa.

(c) Kukamilisha mipango ya utekelezaji wa shughuli ambazo zinaweza kwenda sambamba na maandalizi ya maboresho kwa nia ya kuendeleza nguvu na msukumo wa Watanzania uliotokana na Riporti ya Utafiti kama ifuatavyo:-

(i) Kuandaa na kutekeleza mkakati wa mawasiliano ili kuhakikisha kuwa maboresho yaliyochaguliwa yanamfikia mlengwa.

(ii) Kukamilisha utaratibu wa mkataba na Taasisi ya Takwimu ya Taifa ili kufanya utafiti wa msingi wa sekta isiyo rasmi kwa Zanzibar na Dar es Salaam. Aidha, utafiti huu unalenga kusaidia katika kuratibu ukuaji wa sekta isiyo rasmi.

(iii) Kutengeneza miongozo na taratibu ambazo zitawapa uwezo walengwa na watekelezaji wa kushiriki kikamilifu katika suala zima la urasimishaji.

(iv) Kuyafanyia majaribio maboresho yanayopendekezwa (*piloting of reform packages)* ili kuthibitisha ubora wake.

(v) Kuwawezesha walengwa ambao kwa sasa wameshaanza mchakato wa kurasimisha rasilimali na biashara zao kukamilisha urasimishaji na kuanza kutumia rasilimali na biashara zao kupata mikopo na fursa nyingine katika soko rasmi.

(vi) Kuanzisha mchakato wa kutengeneza taratibu za usajili ambapo rasilimali za majengo, ardhi na biashara, utambuzi wa watu na taarifa nyingine muhimu zinaweza kupatikana kwa urahisi.

(vii) Kukamilisha Dhana ya MKURABITA *(Program Concept Document*) ili litumike kwa ajili ya kuandaa utekelezaji wa awamu zinazofuatia.

(i) Kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kuandaa utaratibu wa muda wa utoaji hati za kumiliki ardhi kimila kwa kasi zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa kazi wa 2006/2007 Menejimenti ya Utumishi wa Umma tumepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(a) Kuendelea kuboresha maslahi ya watumishi kwa kutekeleza Sera ya Muda wa Kati ya Malipo ya Mishahara (*Medium Term Pay Policy*). Katika mwaka wa fedha 2006/2007, jumla ya Shilingi 1,003,882 milioni zimetengwa kwa ajili ya kugharamia mishahara, ajira mpya na upandishwaji vyeo kwa watumishi wa umma. Kiwango hiki ni sawa na ongezeko la Shilingi 321,985 milioni, na pia sawa na ongezeko la asilimia 47.22 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi 681,897 milioni zilizotengwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2005/2006.

Nyongeza hii itasaidia kugharamia ajira mpya 24,689, upandishwaji vyeo kwa watumishi wenye utendaji mzuri na marekebisho ya mishahara ya watumishi ambayo itapanda kwa viwango vya asilimia kati 15.9 hadi 50. Kutokana na maelekezo ya sera viwango vya mishahara kwa watumishi ambao ni wataalam (fani zote) na watumishi walio katika vyombo vya ulinzi na usalama vitapanda zaidi kuliko vile vya watumishi wengine wa kawaida.

(b) Kuhuisha Mipango Mkakati ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mikoa na Wakala wa Serikali ili iendane na Mwongozo mpya wa kuandaa Mipango Mkakati na Bajeti.

(c) Kuhuisha Sheria, Kanuni, Sera na nyaraka mbalimbali zinazosimamia Utumishi wa Umma ambazo zimepitwa na wakati.

(d) Kufanya mapitio ya mifumo na taratibu za uendeshaji kazi ili kizioanisha na Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002.

(e) Kuanzisha mfumo wa uwajibikaji (*Institutional Accountability Framework*) kwa viongozi wa juu kiutendaji na kisiasa katika ngazi mbalimbali za kiutendaji serikalini.

(f) Kubadilisha Idara sita (6) za Serikali kuwa Wakala, kuendelea kuimarisha Wakala ishirini na nne (24) ambazo tayari zimezinduliwa kwa kuziwekea na kuimarisha mifumo ya uwajibikaji.

(g) Kushirikisha Sekta Binafsi katika kutoa huduma kwa Umma katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali kumi na nane (18), Mikoa minne (4), Hospitali za Mikoa Nne (4) na Hospitali za Rufaa mbili (2); na kufanya tathmini *(impact assessment study)* ya mpango huo katika maeneo ambayo umeanza kutekelezwa kwa lengo la kujua mafanikio na mapungufu yake.

(h) Kuendelea kuhuisha miundo ya Wizara na Idara Zinazojitegemea kwa kadri ya mahitaji ili kuimarisha na kuboresha utendaji wa kazi.

(i) Uwekaji wa viwango vya menejimenti katika Wizara na Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

(j) Kuendelea kuziwezesha Wizara na Idara Zinazojitegemea saba (7) kuchambua na kuboresha taratibu za utoaji wa huduma ili kupunguza urasimu, muda na gharama za utoaji wa huduma hizo kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi (*Business Process Improvement*).

(k) Kuandaa na kutekeleza mifumo mipya ya taratibu za kiutumishi na malipo ya mishahara (*Human Resource and Administrative Processes*).

(l) Kupokea na kushughulikia malalamiko ya watumishi hususan yale yanayohusiana na utekelezaji na ukiukwaji wa matakwa ya sera, kanuni, taratibu na miongozo mbali mbali.

(m) Kuendelea na ukaguzi wa orodha ya malipo ya mishahara kwa nia ya kudhibiti matumizi yasiyo sahihi ya fedha za mishahara na bajeti.

(n) Kuandaa taratibu za Utendaji Bora katika kushughulikia masuala ya Upatanishi na Maridhiano (*Arbitration and Reconciliation Code*).

(o) Kuendelea kuimarisha na kuboresha utendaji kazi kwa kutumia teknolojia ya kompyuta katika kusimamia mfumo wa uendeshaji na ulipaji wa mishahara katika Wizara 5, na baadaye kuendelea na zoezi hili katika Wizara nyingine ikiwa ni pamoja na Mikoani. Aidha, kuendelea na zoezi la usimamiaji na uandaaji wa Mkakati wa Mifumo ya Taarifa za Uendeshaji (*Management Information System Strategy*) katika Wizara kumi (10).

(p) Kuendelea na ujenzi wa jengo la Kituo cha Serikali-Mtandao (*Network Management Center*) pamoja na uenezi wa mtandao wa mawasiliano imara Serikalini.

(q) Kuweka mfumo mpya wa utunzaji wa kumbukumbu katika ofisi sita (6) za wakala wa Serikali na katika ofisi kumi na moja (11) za mikoa. Aidha, kuendelea na zoezi la kuhuisha kumbukumbu muhimu za kiutumishi katika wizara kumi na tano (15).

(r) Kutoa mafunzo kwa wanawake 230 ili kuwajengea uwezo wa kiutendaji na kuwawezesha kushika nafasi za uongozi.

(s) Kuandaa miongozo ya kudhibiti kuenea kwa Ukimwi na namna ya kushughulikia watumishi wenye ulemavu katika Utumishi wa Umma.

(t) Kuendelea kukuza na kufuatilia utendaji kazi unaozingatia maadili ya kazi.

(u) Kuanza kutekeleza utaratibu wa kupokea, kushughulikia malalamiko yanayokera wananchi dhidi ya utumishi wa umma katika wizara sita (6) ili kupima ufanisi wake na hatimaye kuendelezwa katika wizara na idara zote za Serikali.

(v) Kuendelea kuratibu mafunzo kwa watumishi wa umma.

(w) Kuendelea kukiimarisha Kituo cha Mafunzo ya Maendeleo ya Dunia *(TGDLC)* ili kiweze kutoa mafunzo mbali mbali kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano.

(x) Kuendelea kukiimarisha Chuo cha Utumishi wa Umma *(TPSC)* ili kiweze kutoa mafunzo kwa watumishi wa Umma na wadau wengine, na kuongeza kasi ya kukibadilisha ili kuwa Chuo cha Uongozi wa Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imepanga kutekeleza kazi zifuatazo katika mwaka wa fedha 2006/2007:-

(a) Kuimarisha Ofisi sita za Kanda kwa kuziongezea watumishi na vitendea kazi ili kuboresha huduma zake kwa Viongozi na wananchi kwa ujumla.

(b) Kuhakiki mali za baadhi ya viongozi walizozitaja katika Tamko la Rasilimali na Madeni kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa mali zilizotajwa katika Tamko ndizo walizo nazo. Aidha, ulinganisho utafanywa kati ya mali zilizotajwa kwenye tamko na maelezo ya kipato ya viongozi husika. *(Makofi)*

(c) Kuandaa mfumo wa benki ya takwimu (*data bank*) ya mali za viongozi wa umma kwa ajili ya kurahisisha rejea na uwekaji kumbukumbu wa mali hizo na taarifa za viongozi kwa usahihi.

(d) Kuandaa, kuchapisha na kusambaza Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma kwa lugha nyepesi ili viongozi na wananchi waweze kuzielewa kanuni hizo kwa urahisi.

(e) Kuipitia Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 1995 na Sheria Ndogo zilizotungwa chini ya Sheria hiyo na kupendekeza marekebisho yanayohitajika.

(f) Kuchunguza kwa haraka malalamiko ya ukiukaji wa maadili ya Viongozi yatakayowasilishwa na wananchi kwenye Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

(g) Kutoa elimu ya maadili kwa viongozi na wananchi kwa njia ya redio, semina na machapisho mbalimbali kwa lengo la kukuza maadili mema na utawala bora nchini.

(h) Kuwapatia watumishi 25 wa Sekretarieti mafunzo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji wao wa kazi.

(i) Kusimamia uendeshaji wa Mfuko (*Facility*) utakaoanzishwa chini ya Mradi wa Kuimarisha Uwajibikaji, Uwazi na Uadilifu katika utendaji wa umma (*Accountability Transparency and Integrity Program (ATIP).*

Lengo la Mfuko huu ni kuziwezesha taasisi za Umma na binafsi zinazojihusisha na uwajibikaji, uwazi na uadilifu *Oversight and Watchdog Institutions (OWI)* kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha Mfuko utavisaidia Vyama vya Kitaaluma (*Professional Associations*) ili viweze kuimarisha maadili ya taaluma miongoni mwa wanachama wake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007 Tume ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

(a) Kushughulikia rufaa za watumishi, waajiri na Mamlaka za Nidhamu na kutoa Miongozo mipya kuhusu masuala mbalimbali ya Utumishi wa Umma.

(b) Kuandaa na kurusha hewani vipindi 52 vya radio kwa lengo la kuwaelimisha watumishi, waajiri na wadau wote kuhusu Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma.

(c) Kuwajengea uwezo watumishi 300 wa Tume kwa kuwapeleka kwenye mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

(d) Kufanya ukaguzi kuhusu uzingatiaji wa Miongozo, Taratibu na Kanuni kwenye Mamlaka 120 za Ajira na Nidhamu.

(e) Kufuatilia ukamilishaji wa taratibu za uendeshaji katika Utumishi Serikalini, Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji, Serikali za Mitaa, Walimu na Afya.

(f) Kushauri na kusaidia Mamlaka za Ajira 120 kuhusu Ajira, kuthibitishwa kazini na kupandishwa vyeo.

(g) Kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa kuhakikisha kuwa watumishi wa Tume wanakuwa na vitendea kazi muhimu.

(h) Kuanzisha ofisi ndogo Zanzibar.

(i) Kuimarisha Kamati za Uchunguzi kwa Idara ya Utumishi wa Walimu.

(j) Kukarabati ofisi 10 za Tume Mikoani na Wilayani, kununua samani za ofisi, pamoja na matengenezo madogo madogo ya ofisi za makao Makuu ya Tume.

Mheshimiwa Spika**,** Utumishi wa Umma ni nguzo ya Taifa lolote duniani. Watumishi wa Umma wanatoa mchango mkubwa katika kulinda na kujenga heshima ya nchi, kudumisha usalama, amani na utulivu na kuiwezesha Serikali kutekeleza shughuli zake ipasavyo. Huu ndiyo msingi wa mpango wa Serikali wa Kuboresha Utumishi wa Umma kwa kuweka mifumo na kanuni nzuri ili kuwa na utendaji kazi mzuri na uwajibikaji katika Serikali nzima.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu hii, nimeeleza kwamba tunaendelea na juhudi kubwa kuboresha utendaji kazi katika utumishi wa umma ili uwe kweli nguzo muhimu inayochangia ukuaji wa uchumi wetu na kuondoa umaskini, kuboresha uwajibikaji, utoaji huduma na utawala bora. *(Makofi)*

Lengo kubwa la kufanya haya yote ni kuendelea na juhudi hizi ambazo matokeo yake mazuri tayari yameshaonekana. Changamoto yetu sote ni kuongeza kasi ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii imewezekana kuandaliwa na kusomwa katika Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano mkubwa nilioupata kutoka kwa Mawaziri wenzangu; Mheshimiwa Kingunge Ngombale Mwiru, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Siasa na

Uhusiano wa Jamii; Mheshimiwa Philip Sang'ka Marmo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora.

Sisi wote kwa pamoja tumekuwa na ushirikiano wa karibu sana katika kusimamia haya yote niliyoyaeleza katika hotuba hii na pia yale yaliyopangwa kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha, 2006/2007.

Aidha, napenda kuwashukuru watumishi wote wa umma na wananchi kwa ujumla kwa ushirikiano waliotupatia katika kutekeleza shughuli za Ofisi ya Rais pamoja na michango yao ya hali na mali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani kwa Wafanyakazi wa Ofisi ya Rais - IKULU, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma kwa ushirikiano na mchango wao uliowezesha maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee tunapenda kuwashukuru Watendaji Wakuu: Bwana Phillemon Lutangilo Luhanjo, ambaye ni Katibu Mkuu Kiongozi. Wengine ni Bibi Rose Lugembe, Katibu Mkuu IKULU, Bibi Ruth Hiyob Mollel, Katibu Mkuu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Bwana George Daniel Yambesi, Naibu Katibu Mkuu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Wenyeviti na Makatibu wa Tume na Taasisi mbali mbali zinazoendeshwa chini ya Ofisi ya Rais kwa uongozi wao thabiti uliowezesha mafanikio haya yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio yetu pia yamechangiwa na nchi, Mashirika na Taasisi mbali mbali za nje. Hivyo basi tunapenda kutambua na kushukuru mchango unaotolewa na Benki ya Dunia, *JICA, DFID, CIDA, GTZ, UNDP, NORAD, DANIDA, ACBF, OPEC* na Jumuiya ya Umoja wa Nchi za Ulaya *(Eropean Union)*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi nilioutoa hapa juu, naomba sasa Bunge lako Tukufu, lipokee maombi yetu ya fedha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa mpango wa mwaka 2006/2007 kama ifuatavyo:-

Ofisi ya Rais, Ikulu - Fungu 20, Sh. 5,550,756,800/=. Fungu 30 - Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri Sh. 125,863,118,000=; Sh. 91,077,278,000/= kwa matumizi ya kawaida na Sh. 34,785,840,000/= kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo.

Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma jumla Sh. 58,430,104,500/=; Matumizi ya Kawaida ni Sh. 9,122,546,000/= na fedha kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo ni Sh. 49,307,558,500/=.

Fungu 33 - Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Matumizi ya Kawaida ni Sh. 1,249,076,000/= na Fungu 94 - Tume ya Utumishi wa Umma jumla ya Sh.

8,069,314,000; Matumizi ya Kawaida ni Sh. 7,929,326,000/= na fedha kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo ni Sh. 139,988,000/=.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru tena wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. TATU M. NTIMIZI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nashukuru nami kwa kupata nafasi na napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia leo kuweza kusimama na kuweza kutoa maelezo kwa niaba ya Kamati yetu ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 81(1), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma) kwa Mafungu: 20 – Ikulu, 30 – Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, 32 – Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma, 33 – Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, na 94 – Tume ya Utumishi wa Umma, kwa mwaka wa Fedha 2006/2007, na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili.

Aidha, Taarifa hii inahusu utekelezaji wa kazi zilizofanywa na Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, tarehe 29 Mei, 2006, Kamati yangu ilitekeleza kazi ya kupitia Bajeti ya Ofisi ya Rais, kwa kupokea maelezo ya Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 na utekelezaji wa kazi zilizofanywa kwa mwaka wa fedha uliopita, yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma).

Mheshimiwa Spika, katika maelezo hayo Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa ushauri uliotolewa na Kamati katika Mwaka wa Fedha wa 2005/2006. Ushauri huo ulihusu Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) kama ifuatavyo:-

(1) Kuishauri Serikali kuweka mkakati maalumu wa kuwamotisha watumishi wanaofanya kazi katika mikoa na Wilaya zenye mazingira magumu hususan Mikoa ya Kusini;

(2) Kuishauri Serikali kushughulikia ulipaji wa malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wote; na

(3) Kuishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuipa mikoa mamlaka ya kuidhinisha ajira mbadala kuliko kuendelea na utaratibu wa sasa ambapo vibali hutolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambayo ndiyo yenye mamlaka ya kuidhinisha ajira mpya na mbadala.

Mheshimiwa Spika, napenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kuwa ushauri wetu ulizingatiwa na kutekelezwa.Mbali na ushauri huo, Kamati yangu ilipokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali zilizopangwa kufanywa katika mwaka wa Fedha 2005/2006. Utekelezaji huu uliainisha majukumu mbalimbali yaliyopo katika Ofisi ya Rais Ikulu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na kiasi cha fedha kilichotumika kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Mipango ya Maendeleo hadi kufikia Aprili, 2006.

Miongoni mwa mafanikio yaliyoelezwa katika kipindi hiki ni pamoja na ukarabati wa jengo la Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ambalo kwa bahati nzuri Kamati yangu ilipata fursa ya kulikagua ilipokuwa na ziara ya siku moja kuzitembelea asasi zilizo chini yake wakati wa vikao vya Kamati vilivyofanyika Dar es Salaam kabla ya kuanza kwa Mkutano wa Tatu wa Bunge. Mafanikio mengine ni kuendelea kwa Awamu ya Pili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)*. Kabla ya kuanza kwa Mkutano huu wa Bunge la Bajeti, Kamati hii ilipata fursa ya kutembelea miradi kadhaa inayosimamiwa na Mfuko huo katika Visiwa vya Pemba na Unguja na Mkoa wa Tanga na kujionea maendeleo yaliyofikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Kamati ilielezwa juu ya utekelezaji wa kazi mbalimbali zilizokusudiwa kutekelezwa na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma katika Mwaka wa Fedha uliopita na maeneo yaliyopewa kipaumbele. Aidha, Kamati ilijulishwa juu ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na kutumika hadi kufikia Aprili, 2006 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Halikadhalika, Kamati ilipata fursa ya kufahamu mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika taasisi hizo katika kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Spika, mbali ya kupokea Taarifa ya Utekelezaji kwa mwaka 2005/2006, Kamati ilielezwa juu ya Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2006/2007 na kuainishiwa shughuli mbalimbali zinazokusudiwa kufanywa na Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma na kiasi cha fedha kinachoombwa ili kuviwezesha vyombo hivyo kutekeleza majukumu yake. Mwisho, Kamati iliombwa kupitisha maombi ya fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Mipango ya Maendeleo.

Baada ya kupokea maelezo hayo, Kamati yangu inapenda kuishauri Serikali katika maeneo kadhaa. Nikianza na Ofisi ya Rais (Ikulu) na Sekretarieti ya Baraza la

Mawaziri, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* katika Awamu yake ya kwanza, kama tulivyoshuhudia katika ziara yetu tuliyofanya hivi karibuni, kama tulivyoshuhudia katika ziara yetu tuliyoifanya hivi karibuni Kamati inapenda kuishauri Serikali kuwa iwahamasishe wananchi waitumie *TASAF* kikamilifu ili iweze kuwaletea maendeleo kwa kushirikisha nguvu zao. Nafurahi kwamba tulipokuwa Pemba kwa kweli pamoja na upinzani uliopo kisiasa lakini wananchi walijitokeza kusaidia kazi ambazo zimeletwa na fedha za *TASAF* kwa moyo mmoja na kwa ushirikiano bila kujali ni nani mwenye chama gani. Kamati inapenda kuishauri Serikali kuwa iwahamasishe wananchi waitumie *TASAF* kikamilifu ili iweze kuwaletea maendeleo kwa kushirikisha nguvu zao.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wakati Awamu ya Kwanza ya *TASAF* ilikwenda vizuri, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa Awamu ya Pili wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii umechelewa mwaka mmoja nyuma na hivyo kuathiri utekelezaji wa baadhi ya miradi katika muda uliopangwa. Kutokana na umuhimu wa Mfuko huu Kamati inashauri kuwa Serikali ifanye uchunguzi wa kina ili kujua sababu za ucheleweshaji huo. Kuhusu Kikosi cha Kuzuia Rushwa, Kamati inaridhika na kazi nzuri inayofanyika hivi sasa ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo chombo hiki kwa kiasi fulani kilikuwa kikionekana kuwa hakina meno hasa kilipokabiliana na tuhuma zilizowahusu watu wenye nyadhifa kubwa Serikalini na katika sekta za umma. Kamati inashauri kuwa chombo hiki kiendelee kuimarishwa na kipewe uwezo zaidi ili kuwakabili watuhumiwa wa aina hiyo ambao Kamati inaamini kuwa bado wapo na ndio wameweka mizizi ya rushwa nchini. Ili chombo hiki kifanikiwe kutahitajika utashi wa kisiasa kutoka kwa viongozi wote na ushirikiano mkubwa kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Kamati inaona kuwa mbali ya jitihada zinazofanyika kuboresha utumishi katika sekta ya umma bado yapo maeneo Mikoani na Wilayani ambayo watumishi wa kada za chini huwa hawasikilizwi na baadhi ya watendaji wanapowasilisha matatizo yao ya kazi. Suala hili limekuwa kero kwa watumishi hao. Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri kuwa Serikali ilifuatilie suala hili na kulipatia ufumbuzi unaostahili. Itakumbukwa kuwa Serikali imejitahidi kujenga shule nyingi za msingi na sekondari. Kwa bahati mbaya pamoja na kazi nzuri iliyofanyika bado kuna uhaba mkubwa sana wa walimu katika shule zetu. Licha ya kwamba azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa kunakuwepo na ubora wa elimu, kuwepo kwa upungufu wa walimu kunaathiri lengo lililokusudiwa. Ili kutatua tatizo hili, Kamati yangu inashauri kuwa Serikali iangalie uwezekano wa kutoa vibali vya muda vya ajira kuwawezesha walimu ambao hawajapata ajira wafundishe katika shule hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi ambayo inasimamia sheria inayowataka viongozi wa umma kuwasilisha taarifa za mali zao baada ya kumaliza vipindi vyao vya uongozi, inawezekana kuwa kuna viongozi wachache ambao hawatekelezi agizo hilo kwa wakati au hawatekelezi kabisa. Kwa hiyo, Kamati inashauri kuwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilifuatilie suala hili. Pia Kamati inaona kuwa ni wakati muafaka kwa Sekretarieti ya Maadili kuitazama tena Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuona kama bado inakidhi matakwa

yaliyokusudiwa. Kama tunavyofahamu wastaafu walio wengi huwa hawajimudu kimaisha, hali ambayo huwafanya baadhi yao kufariki mapema baada ya kustaafu. Kwa kuwa malipo ya pensheni wanayolipwa wastaafu walio wengi hayatoshelezi kulingana na ugumu wa maisha, Kamati inashauri kuwa utaratibu wa kufanya mahesabu ya pensheni ya wastaafu uangaliwe upya na kwamba malipo yafanywe kwa kuzingatia kupanda na kushuka kwa thamani ya shilingi yetu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine linahusu kuingiliana kwa majukumu kati ya Tume iliyoundwa na Serikali kuchunguza maslahi ya watumishi wakati huo huo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ikiendelea na zoezi la kuboresha maslahi ya watumishi. Kamati iliona kuwa maamuzi ya Tume hiyo yataweza kuingiliana na mikakati iliyowekwa na Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika zoezi hilo. Hata hivyo, Kamati iliridhika na maelezo kuwa hatimaye Tume hii itawasilisha mapendekezo yake katika Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) ili yafanyiwe kazi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu, tarehe 14-24 Machi, 2006, Kamati yangu ilitembelea asasi na Wizara kadhaa inazozisimamia kwa ajili ya kujifunza shughuli zinazofanywa na vyombo hivyo. Miongoni mwa asasi hizo ni Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kilichopo Magogoni, Dar es Salaam.

Katika Chuo hiki Kamati ilijulishwa juu ya juhudi zilizofanywa na Serikali kukibadilisha Chuo hicho kuwa Chuo cha Uongozi (*Staff College*) na juhudi zinazoendelea za kupanua huduma za mafunzo katika fani ya Uongozi, Menejimenti na Utawala kwa kushirikiana na vyuo mbalimbali vya kimataifa vya Utumishi wa Umma kama Malaysia, Singapore, Ghana, Uganda, Afrika Kusini na *ESAMI.* Hata hivyo, licha ya jitihada hizo Kamati ilibaini kuwa eneo ambalo linatumiwa na chuo hicho ni finyu sana kwa hivi sasa halitoshi. Pamoja na kuridhishwa na mabadiliko yaliyofanyika Chuoni hapo, Kamati ilijulishwa kuwa Chuo hicho kimetafuta eneo Bagamoyo ili kukidhi mahitaji yake halisi, lakini bado hawajamilikishwa.

Kamati inashauri kuwa, Wizara ya Ardhi na Wizara hii washirikiane wakalione hilo eneo ili waweze kupewa hati ya kumiliki na waanze ujenzi mara moja kusudi maana ya *Staff College* kuwe ni eneo kubwa, lenye maeneo mazuri, mazingira mazuri na waweze kujidai kwa sababu pale wamekuwa na ufinyu kweli kweli ambapo unakuta kuna Ardhi upande na upande mwingine kuna Ikulu, kiasi ambacho kwa kweli nafasi ya kuitwa *Staff College* pale haionekani kwa macho. Kwa hiyo tunasisitiza sana Wizara hii ifanye kila iwezalo ili Wizara ya Ardhi iweze kukubali kutoa hati na kuwapa eneo hili ili chuo kiweze kupanuliwa katika eneo lile ili waweze kutoa mafunzo ambayo yanahitajika na hadhi ya *Staff College* ionekane kwamba kweli kuna mahali pa kujidai na pakubwa pa kufanyia kazi yao.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla haya ndiyo maoni na ushauri wa Kamati yangu ilipopitia na kuchambua Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma) kwa mwaka wa Fedha 2006/2007. Kama yatajitokeza maeneo mengine ambayo sikuyagusia, sina shaka kuwa Wajumbe wa Kamati hii watakapopata

nafasi ya kuchangia wanaweza wakaongeza mjadala wa Ofisi hii. Napenda kukuthibitishia kuwa kutokana na kazi nzuri na maelezo ya ufasaha yaliyowasilishwa mbele ya Kamati, Kamati yangu ilipitisha Bajeti ya Ofisi hii kwa kauli moja.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati. Napenda nimshukuru pia Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) na Mheshimiwa Phillip S. Marmo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora), Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara, Taasisi na Vitengo, kwa ushirikiano waliotupatia na kwa kutoa maelezo yaliyojitosheleza wakati wote tulipokuwa tukijadili Makadirio ya Ofisi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati, kwa kazi kubwa waliyofanya walipochambua Bajeti ya Ofisi hii. Matokeo ya kazi yao ndiyo yametuwezesha tuwasilishe Taarifa hii. Naomba niwatambue kwa dhati kabisa hasa Mheshimiwa Ndugu yangu, Mgogo mwenzangu George Malima Lubeleje, ambaye ni Mwenyekiti; mimi mwenyewe, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati hii ambao ni Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Shoka K. Juma, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohammed, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi, Mheshimiwa Ramadhan A. Maneno, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nawashukuru Makatibu wa Kamati hii: Ndugu Charles Mloka na Ernest Zulu kwa kutoa huduma inayostahili kwa Kamati yetu wakati wote wa vikao na kuandaa Taarifa ya Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kukubali kuidhinisha jumla ya Sh.199,162,369,300/= kwa ajili ya Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma).

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba wiki iliyopita nilimhitaji Mheshimiwa Mbunge wa Bariadi Mashariki Mheshimiwa John Cheyo athibitishe usemi wake, kwa mujibu wa Kanuni ya 50(1) kuhusu kuliwa kwa Mfuko wa Elimu kule Shinyanga na nilimpa muda mpaka saa 11.00 leo ambayo ndiyo sasa.

Napenda kuthibitisha kwamba amewasilisha ndani ya muda, ninao hapa huo uthibitisho. Sasa uthibitisho wake ni mrefu, una kurasa 20 na viambatanisho 15. Kwa hiyo, kwa kutumia mamlaka yangu, chini ya Kanuni ya 90(2), nitaisoma hii ili muifahamu. Pamoja na mambo mengine, inasema:

"Hali kadhalika Spika, anaweza kukabidhi jambo lingine lolote kwa Kamati yoyote kama atakavyoona inafaa kwa ajili ya kushughulikiwa na Kamati hiyo."

Kwa hiyo, napenda kuwatangazia kwamba kwa sababu jambo hili lilizuka wakati wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, leo saa 7.00 nitamkabidhi Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi ambaye naye pia jina lake ni Cheyo, lakini ni Mheshimiwa Gideon Cheyo.

Nataka Kamati yake ilishughulikie jambo hili ndani ya wiki moja na kumshauri Spika. Kwa sababu vielelezo ni vingi sana na ni vizuri walitazame na kwa sababu suala lenyewe ni kutafunwa kwa fedha za wakulima, basi nadhani ni vizuri Kamati hii iweze kulitazama. Halijaiva kufikishwa kwenye Kamati ya Maadili, kwa sababu sijaelewa humu ndani ya uthibitisho kilichomo ni nini.

Kwa hiyo, Kamati ya Kilimo na Ardhi nawapa muda wa wiki moja watazame wampe ushauri Spika, *then* Spika ataliarifu Bunge. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeamua kusema hili kwa wakati huu kwa sababu kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanasubiri kwamba saa 11.00 labda nitamwita Mheshimiwa John Cheyo aongee. Ndiyo maana nimesema hapana, siyo hivyo, inabidi ushahidi utazamwe kwa uangalifu kwa sababu tunataka kutenda haki. Ahsanteni sana.

Sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii. *(Makofi)*

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba upokee shukurani zetu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Hotuba ya Bajeti, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Siasa na Mahusiano ya Jamii kwa mwaka wa fedha 2006/2007 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b)(c) na 81(1) toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wasemaji wenzangu wa Kambi ya Upinazani wa Wizara hizi, Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi - Msemaji wa Upinzani kwa Wizara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Mheshimiwa Said Amour Arfi - Msemaji wa Upinzani kwa Wizara ya Siasa na Mahusiano ya Jamii kwa ushirikiano wao wa kuandaa hadi kukamilisha hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Micheweni kwa imani waliyonayo kwangu, kwa kunipa kura nyingi. Aidha, ninakishukuru Chama changu cha Wananchi *(CUF)* na viongozi wake wote kwa ushirikiano nilioupata katika ushindi huo. Nasema Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuwapongeza wote waliochaguliwa na kuteuliwa kwa nyadhifa zao mbalimbali.

Napenda kuwapongeza Mawaziri wote katika Ofisi ya Rais kwa majukumu waliyokabidhiwa na sisi tupo tayari kushirikiana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Ofisi ya Rais Ikulu ni kumwezesha Mheshimiwa Rais wetu kuwa na mamlaka ya kuangalia utendaji wa jumla wa Serikali, kufanya maamuzi na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi hayo kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na unyeti wa Ofisi hii, ina umuhimu wa kipekee na ni wazi waliopewa dhamana kuiongoza Ofisi hii wanategemewa kuwa waadilifu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, katika kutoa hoja zetu, tunapenda kuigawanya hotuba hii kufuatana na Idara mbalimbali zilizopo chini ya Ofisi hii ya Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Utumishi wa Umma, Kambi ya Upinzani inapongeza jitihada za Serikali katika kupandisha kima cha chini cha mishahara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo watumishi wetu wananyonywa sana, kuelemewa na mzigo wa kodi tunaowabebesha kila mara. Wengi wao wamekuwa wakikatwa karibu nusu ya mishahara yao kwa kodi na malipo mbalimbali na wakati mwengine bila ya ridhaa zao. Kwa hali hii, suala la kuwaongezea mshahara mara nyingi linaishia kuwa kiini macho tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina uhaba mkubwa sana wa Madaktari, Walimu, Wahudumu wa Afya na Watumishi wengineo. Ni ajabu kuona kuwa wakati tumekuwa tukijitahidi kuongeza idadi ya Shule na Vyuo vya kuwasomesha vijana wetu, bado hatujatambua mzizi mkuu wa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuwa na wataalam wa kutosha katika Sekta ya Afya na Elimu, ni wajibu wa Serikali kuboresha hali za watumishi wetu kwa kuwapa mishahara na marupurupu yanayofanana na thamani ya mchango wao kwa jamii yetu. Ili tupate wafanyakazi wenye mapenzi na uwezo wa hali ya juu kwenye Sekta hizo, ni lazima thamani ya taaluma zao ziboreshwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa viongozi wetu na watu maarufu nchini kwenda kutibiwa nje ili kuwafuata Madaktari bingwa wakati inawezekana kufanyika hapa hapa nchini. Tutambue kwamba wengi wa Madaktari hao wanaowafuata huko Afrika ya Kusini na Nairobi ni Watanzania tuliowasomesha kwa kodi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali mbaya kama ya Sekta ya Afya na ya Elimu ipo katika ngazi nyingine za utumishi. Ili kuweza kutatua tatizo hili ambalo limekuwa sugu, hivi sasa ni wajibu wa Serikali kufanya mambo kadhaa kama ifuatavyo:-

- Watumishi wa Serikali kuanzia ngazi ya chini wapewe mishahara, marupurupu na posho zao kwa wakati.

- Suala la kodi wanazokatwa watumishi hao tunaomba liangaliwe upya ili hatua za kuongeza mishahara zisiendelee kuwa kiini macho tu na ziweze kuboresha maisha ya kila siku ya Watumishi wa Serikali.

- Watumishi wa Serikali wapandishwe madaraja, vyeo na mishahara kwa wakati kulingana na taratibu na kanuni zilizowekwa na kwa kupima utendaji wao kwa haki bila ya ubaguzi wowote.

Mheshimiwa Spika, hapa pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri amesema hatua hizi zitachukuliwa, tunasisitiza zifanywe kwa uwazi. Mheshimiwa Waziri kwa sababu yeye kazisoma, lakini sisi tunasisitiza kwamba zifanywe kwa uwazi.

- Watumishi wa Serikali waruhusiwe kujiendeleza kielimu kwa ridhaa zao wenyewe ili mradi tu wanastahili na sio kutegemea mpango wa muda mrefu wa kuendeleza watumishi wa sekta hizo. Kuna malalamiko katika Idara nyingi sana ya watumishi kunyimwa nafasi ya kujiendeleza.

- Mheshimiwa Spika, miaka mitano ya mwanzo watumishi wote wa Sekta ya Elimu kuanzia Elimu ya Msingi hadi Vyuo na wale wa Afya, yaani Madaktari na watumishi wengine wapewe msamaha wa kodi zote wanazokatwa ili waweze kuboresha maisha yao na wawe kivutio kwa wengine zaidi kujiunga na Sekta hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inapongeza nyongeza iliyotolewa, lakini tumepokea nyongeza ilitolewa na Serikali ambayo kwa kima cha chini haitozidi Sh. 120,000/=. Bado tunaona kwamba kiwango cha Sh. 300,000/= kingeweza kulipwa kama Serikali ingelipunguza matumizi mengine kama *employment allowances*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la maadili ya Watendaji wetu kikazi na binafsi ni lazima lipate Jemadari wa kweli kweli kupambana nalo. Mheshimiwa Waziri wa Utumishi ameonyesha nia ya kuchukua jukumu hili, lakini bado hatujaona makali yake kama inavyopaswa. Hatuwezi kuendelea kuwa na watumishi wa wananchi wasio na nidhamu wanaotukanisha fani ya utumishi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kushuka kwa maadili miongoni mwa watumishi wa Serikali ndio chanzo kikuu cha matatizo yanalolikumba Taifa letu kama vile rushwa na ufisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la ushindani wa kuajiri vijana wenye vipaji vya kiuongozi na kiutendaji na wenye vigezo vya kutosha katika Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni lazima liangaliwe kwa umakini. Siku hizi karibu vijana wote wanaomaliza katika Vyuo vyetu ambao wamethibitisha umahiri wa kielimu na kiutendaji wanachukuliwa na Sekta Binafsi. Serikali imeacha kuchukua hatua za kuwafuatilia watumishi tangu wakiwa Vyuoni ili kuwaajiri katika Idara zetu ambazo zinakutana na ushindani mkubwa na nguvu za utandawazi na soko huria.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kufanikiwa kurekebisha mapungufu haya, tunashauri Serikali ifanye yafuatayo:-

- Irudishe mfumo wa kufuatilia watumishi watarajiwa tangu wakiwa Vyuoni na kuwaanda kulitumikia Taifa ndani ya Sekta ya Umma.

- Kuboresha kipato na marupurupu ya watumishi wa umma ili wawavutie wenzao waliopo Vyuoni. *(Makofi)*

- Kufanya maonyesho mbalimbali ya kazi zao kama ilivyofanyika hivi karibuni, katika viwanja vya mnazi mmoja Jijini Dar es Salaam ndani ya Vyuo vyetu hasa vile Vikuu kila mwaka ili kuwaelezea vijana wetu mfumo wa utumishi wa umma ambao wengi wao hawaufahamu. *(Makofi)*

- Zoezi la ajira katika Serikali ni lazima liongeze uwazi na lionekane wazi ni la haki na la umakini ili kuondoa dhana iliyojengeka katika jamii kuwa kazi za utumishi wa umma ni za watu wachache tu.

Mheshimiwa Spika, dhana ya utawala bora ni moja ya dhana zilizoingizwa katika mfumo wetu wa kisiasa katika miaka ya tisini pale tulipoanza kujenga mfumo wa siasa na demokrasia ya Vyama Vingi.

Mheshimiwa Spika, ni miaka zaidi ya ishirini sasa, dhana ya utawala bora imekuwa moja ya kauli mbiu za Serikali. Kwa namna moja ya kimtazamo, utawala bora unahusisha watumishi wa Serikali na wananchi. Hii ina maana kwamba dhana hii inapaswa kuwa kioo cha mwingiliano kati ya wananchi na watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kisheria na kinadharia, nchi yetu inafuata utawala wa sheria na Katiba na Katiba imeweka wazi mgawanyiko rasmi wa madaraka kati ya Bunge, Mahakama na Utendaji .

Mheshimiwa Spika, uzoefu wa miaka zaidi ya ishirini sasa, inaonyesha dhahiri kuwa Serikali yetu ama imeshindwa kujua maana halisi ya utawala bora ama kwa makusudi kabisa imeamua kutofuata dhana hii kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu tumeanza kutumia dhana hii, matendo ya watawala wetu, yaani viongozi wetu wa Sekta mbalimbali nchini wamekuwa wakitumia madaraka yao kinyume kabisa na dhana ya utawala bora. Ni kawaida kushuhudia jinsi Watendaji wetu Serikalini na maeneo mengine ya jamii yetu wakitumia madaraka yao kuvunja sheria za nchi, kuhujumu wananchi, kunyanyasa Watanzania na hata kujilimbikizia utajiri wenye kutia mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na utawala bora, kunahitajika mambo kadhaa yawepo katika jamii. Haya ni kama vile utawala unaofuata sheria, mfumo wa kisiasa

unaotoa nafasi kwa mawazo mbadala, kuwepo kwa vyombo binafsi na huru vya habari, kuwepo kwa utamaduni unaoheshimu haki za binadamu na chaguzi za haki na huru zifanyikazo kila baada ya muda maalum. Haya siyo kwamba yawepo kisheria tu, bali yaonekane wazi yakitendeka na bila ya nguvu zake kisheria kupunguzwa na sheria nyingine za mlango wa nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati umefika wa vyombo vyetu vya dola ambavyo vimepewa majukumu ya kulinda sheria za nchi na maisha na mali za Watanzania kushurutishwa kufanya hivyo kwa umakini na sio kama tunavyoona hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, tumeona mara nyingi pale raia wanapoandamana kudai haki zao kwa kutoa madukuduku yao kwa jamii kwa njia ya amani, vyombo vya dola vimekuwa vikitumia nguvu nyingi sana kuwakandamiza raia. Badala ya vyombo hivi kuwapa ulinzi Watanzania kutekeleza haki yao, vyombo hivi vimekuwa mstari wa mbele kuvunja amani ya nchi kwa kutumia mabavu pale ambapo mabavu hayo hayahitajiki. Historia ya kisiasa Visiwani Zanzibar inabaki kuwa mfano wa wazi kabisa wa ukiukwaji huu wa dhana ya utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na Katiba ya nchi yetu, sheria zetu na tamaduni zetu, dhana ya utawala bora nchini imeundiwa vyombo maalum vya utekelazaji. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni moja ya Idara nyeti zilizo na jukumu la kumsaidia Rais wetu kuhakikisha Watendaji wake hawatumii vibaya madaraka aliyowakabidhi.

Mheshimiwa Spika, kama ugeni wa Tume hii kwa jamii ulikuwa ni sababu za kutoipa nguvu za kisheria kushurutisha watawala wetu kutimiza wajibu wao ipasavyo, chombo hiki sasa kimeshapevuka na hatuoni sababu ya kutokiamini kiutendaji. Wakati umefika kubadilisha sheria ya kuunda Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ili iweze kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika kwa pande zote za Muungano kulichukulia suala la Haki za Binadamu na Utawala Bora kama ni jambo la kiustaarabu ambalo sio tu linapaswa kutoogopwa katika jamii yoyote ya kistaarabu, lakini vilevile ni kiungo muhimu cha mapambano ya kujenga uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utendaji wa vyombo vya dola ikiwemo Idara ya Usalama wa Taifa usiwe umejikita zaidi kwa Chama Tawala dhidi ya Vyama vya Upinzani. Watendaji katika Taasisi hii nyeti ni lazima wachukuliwe hatua kali kutokana na kutumia nafasi zao kutumikia maslahi ya Chama Tawala. Ni ajabu kuona kuwa mtu anatoka katika Idara hii nyeti anakwenda kuvaa joho la ukada wa Chama Tawala kama vile bado tupo katika enzi ya Chama kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa za Maafisa wa Usalama wa Taifa kuingilia shughuli za Vyama vya Kisiasa hasa wakati wa Uchaguzi Mkuu ni lazima zifanyiwe kazi na matokeo yake yakaonekana wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata ndani ya Jeshi letu la Polisi na Tume ya Kuzuia Rushwa, kumejaa Watendaji ambao ni makada wa Chama Tawala kwa historia yao na hata utendaji wao umekuwa ukiangalia zaidi maslahi ya Chama Tawala.

Mheshimiwa Spika, sio mara moja ambapo tumeshuhudia Jeshi la Polisi likisambaratisha Mikutano ya Vyama vya Upinzani, Tanzania Bara na Visiwani, kwa hali inayoonyesha wazi kulinda maslahi ya Chama Tawala au bila sababu yeyote ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutumika katika chaguzi zetu kwa Watendaji kama Wakurugenzi wa Wilaya ambao ajira yao na maslahi yao binafsi yanategemea fadhila za Chama Tawala, ni moja ya mambo ambayo yanavunja misingi ya Siasa ya Vyama vingi. Kwani wakati mwingi wamekuwa wakitoa maamuzi kulinda maslahi ya Chama Tawala na kuwanyima Watanzania haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matumizi ya Vyombo vya Serikali katika shughuli za Chama kama ilivyojionyesha wakati wa uchaguzi uliopita, ni tofauti na dhana ya siasa za demokrasia ya Vyama Vingi. Hili pia limethibitishwa katika ripoti nyingi zikiwemo za *TEMCO* za mwaka 1995, 2000 na hata 2005. Ni lazima hatua za kweli zichukuliwe kukomesha tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kambi ya Upinzani kuwa ili kile kinachoitwa kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya, kiwe cha kweli na sio kauli mbiu tu, suala la utawala bora ni lazima lionekane kimatendo. Mambo yafuatayo yanatakiwa yafanyike:-

- Serikali ni lazima iwawajibishe watumishi wake katika utendaji wao ikiwa ni pamoja na kuchukua sheria kali dhidi ya wale wanaotumia madaraka yao vibaya kwa kutenda tofauti na dhana ya kweli ya Utawala Bora.

- Sheria ya kuunda Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni lazima ipitiwe upya kwa kushirikisha wadau wote, yaani watawala na watawaliwa kupitia makundi yao ya kijamii ili iweze kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

- Suala la uhalali wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika Visiwa vya Zanzibar, ni lazima lielezwe rasmi kwa vyombo rasmi kama Bunge hili na kuachana na matamko ya kisiasa.

- Maamuzi na maagizo ya Serikali kwa kupitia Viongozi wake Wakuu ni lazima yaonekane yakitekelezwa na wahusika kuchukuliwa hatua kali bila ya kuoneana huruma.

- Ripoti za Tume mbalimbali za kuchunguza ukiukwaji wa utawala bora kama lile suala la mauaji ya wafanyabiashara wa madini ya vito kutoka Mahenge na dereva wa teksi ni lazima zitolewe kwa wananchi kwa ukamilifu wake bila ya kuficha kitu chochote ili Watanzania wajue ukweli wa mambo.

- Dhana ya utawala bora inabidi ipitiwe upya kwa ujumla wake ili kuona wapi tumekosea na wapi tunaweza kuongezea. Wakati umefika sasa wa kuondokana na dhana hii na kuongelea Uongozi Bora kwa watu wote, kwani utawala bora umekuwa ukitafsiriwa vibaya na Watendaji wetu hasa Viongozi wa kisiasa.

- Maadili binafsi ya Watendaji wetu ni lazima yawe sehemu ya vipimo vya utawala bora kwa Watendaji wetu, hasa wale wanaopewa majukumu ya kuendeleza dhana hii katika jamii. Kama mtu anashindwa kujitawala yeye mwenyewe katika matendo yake, ni wazi hataweza kufuata maadili ya utawala bora kwenye utendaji wake mbele ya Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la haki za binadamu ni suala lingine ambalo Serikali imeshindwa kuwathibitishia kwa vitendo Watanzania kuwa inalichukulia kwa umakini. Kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu, sheria zetu na Mikataba mbalimbali ya haki za binadamu ambayo nchi yetu imeridhia, wigo wa haki hizi unahusu haki za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, la kushangaza ni kuwa Serikali hii hii na Idara zilizopo chini yake, ndizo zinazoongoza katika ukiukwaji wa haki za binadamu. Matumizi ya nguvu za dola kule Serengeti ambapo wananchi kadhaa waliteswa na kuchomewa mali zao ni mfano hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu katika nchi yetu unatokana na kushindwa kwetu kuliongelea suala hili kinagaubaga na kulifanya liwe ni suala la kiutamaduni. Heshima ya binadamu juu ya haki ya binadamu mwenzake, daima huendana na utamaduni wa kutambua mawazo na utashi wa mwenzie. Serikali yetu imeshindwa kujenga utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu kama wajibu wa kila Mtanzania. Juhudi za kuendeleza haki za binadamu nchini zimekuwa zikichukuliwa kisiasa zaidi, hali ambayo inafanya suala la haki za binadamu kuwa ni la kuchagua masuala machache na kuacha masuala mengine ambayo yanaonekana hayana tija kwa Serikali na Chama Tawala.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Mahakama wa kuondoa takrima unapaswa kupongezwa. Kilichoitwa kisheria kama "takrima" kwa kweli kilikuwa ni adui mkubwa wa haki za raia wa nchi hii. Ni imani yetu kuwa Serikali itaunga mkono uamuzi huu bila ya kuandaa mfumo mwingine utakaorudisha jinamizi la takrima kwa mlango wa nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani vilevile inaridhia maamuzi ya Mahakama ya kuruhusu Mgombea Binafsi. Kipengele hiki kiliwanyima raia wa Tanzania haki yao ya kuchaguliwa kuwa viongozi kwa kuwalazimisha kujiunga na makundi ya kisiasa bila ya utashi wao.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya Watanzania walio wengi ni kuwa, badala ya Serikali kutumia fedha za mlipa kodi kupigania matumizi ya sheria ambayo ni kinyume cha haki za binadamu, ni bora ikawa tayari kuipitia upya Katiba ya nchi yetu kwa

ujumla. Suala hili haliwezi kushughulikiwa kwa Serikali yetu kukimbilia Mahakamani kama vile hawana imani na Majaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matarajio yetu ni kwamba, Serikali ya Rais wa Awamu hii ya Nne iliyoanza shughuli zake kwa umahiri mkubwa, haitakumbwa na uoga usio wa lazima wa kuzuia Watanzania wasiotaka kujiunga na Vyama vya kisiasa, kugombea nafasi za uongozi. Ni wazi Serikali mahiri inapaswa kutoonyesha hali ya kutojiamini mbele ya macho ya wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, wakati tukiangalia uwezekano wa kupitisha Bajeti ya mwaka huu kwa Wizara husika, Serikali inawajibika kuwaelezea Watanzania masuala yafuatayo:-

- Ni wananchi wangapi wameuawa mikononi mwa vyombo vya Serikali vikiwemo majeshi yetu ya ulinzi, Jeshi la Polisi na Idara ya Usalama wa Taifa kwa miaka mitano iliyopita na ni hatua gani zimechukuliwa kwa watuhumiwa wa vifo hivyo? *(Makofi)*

- Ni Watanzania wangapi walioripoti matukio ya kuvunjiwa haki zao na ni matukio mangapi yamepatiwa ufumbuzi na waathirika wamepewa fidia kiasi gani?

- Ni Watanzania wangapi wameuawa mikononi mwa raia kwa tuhuma za wizi, uchawi na kadhalika katika miaka mitano iliyopita? Watanzania wangapi wamechukuliwa hatua kutokana na kuhusika katika mauaji hayo na ni hatua zipi zimechukuliwa?
- Ni hatua gani zilizochukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano dhidi ya Watendaji wake wanaohusika na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu katika Visiwa vya Zanzibar yakiwemo mauaji ya raia wasio na hatia?

Mheshimiwa Spika, kipengele kimojawapo katika kazi za Ofisi ya Rais ni kushughulikia masuala ya siasa na mahusiano ya jamii. Hii ni Ofisi mpya ambayo imeanzishwa na Rais wa Nne wa Serikali. Ni wazi huu ni ushujaa wa hali ya juu, kwani kwa kufanya hivyo, Serikali imekubali rasmi hatari za mgawanyiko kisiasa na kijamii zipo nchini mwetu. Kukubali tatizo ni mwanzo mzuri wa kulitatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, hali ya mahusiano ya kijamii nayo siyo nzuri kwa kweli. Tumekuwa tukijisifia kuwa nchi yetu ina umoja na ushirikiano. Lakini kama ilivyojitokeza nyakati mbalimbali, hata hivi karibuni hapa Bungeni wakati wa mjadala wa Wizara mbalimbali, ni wazi nguzo za umoja wa kijamii nchini zipo hatarini na athari zake zimeanza kujitokeza. Inatisha kuona kwamba, hivi sasa hata miongoni mwetu humu ndani tumeanza kusahau kuwa Tanzania ni moja na watu wake wote wana haki sawa. Serikali imetufikisha mahali nchi yetu sasa hatutambuani kama ni Watanzania tu, lakini dini ya mtu, kabila la mtu, uwezo wa kipato, elimu ya mtu, uasili wa mtu na hata rangi ya mtu vimekuwa ni vigezo katika maamuzi mbalimbali miongoni mwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Ofisi ya Rais, Siasa na Mahusiano ya Kijamii ni moja ya hatua zilizopaswa kuchukuliwa mapema.

Mheshimiwa Spika, ili kutimiza wajibu wa Ofisi hii, ni wazi mfumo wake unahitaji kuendana na hali ya kisiasa ambayo kisheria inatambua kuwepo kwa makundi mbalimbali ya kisiasa na sio kundi moja tu la Chama Tawala. Ofisi hii ikiwa na mfumo unaohusisha Watanzania wa makundi mbalimbali ya kisiasa na kijamii, ni wazi madhumuni yake ndiyo yatafikiwa.

Mheshimiwa Spika, kuacha majukumu haya kwa mtu mmoja tu ambaye ni kada mkubwa wa Chama kimoja tu, ni mwanzo wa kushindwa kwa majukumu ya Ofisi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inapaswa kuzingatia yafuatayo ili siasa ya nchi yetu ya Mfumo wa Vyama Vingi na mahusiano ya kijamii yaimarishwe:-

- Nafasi ya Waziri wa Ofisi ya Rais inapaswa kupewa mtu ambaye atalithibitishia Taifa hili kwamba utendaji wake utalenga maslahi ya makundi yote ya kisiasa na Watanzania wote kwa ujumla.

- Mheshimiwa Rais aunde Baraza la Mahusiano ya Kisiasa na Kijamii chini ya Waziri mhusika ambalo litahusisha makundi yote ya kisiasa na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tunaongelea mahusiano bora ya kisiasa na kijamii nchini, suala la hali ya mpasuko wa kisiasa Zanzibar ni lazima lipewe umuhimu wa hali ya juu. Tumesikia mengi yanasemwa, lakini hadi hivi sasa wananchi wamekuwa wakipata ahadi tu na vitendo havionekani.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kisiasa Zanzibar halihitaji *feasibility study,* bali linahitaji utendaji wa kishupavu wenye nia nzuri kwa Wazanzibari wote na sio malengo ya kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wetu kuuliza na Serikali kutoa majibu kama kweli kuna nia thabiti ya kuondoa matatizo ya kisiasa na kijamii Visiwani Zanzibar. Miezi sita sasa imepita tangu Rais wa Nne aapishwe rasmi na kuahidi kuwa atalishughulikia suala hili. Serikali itoe dira ya kutatua tatizo hili sasa kabla hali haijawa mbaya zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Taasisi ya Kuzuia Rushwa nchini, ni jambo la kupongezwa. Ni wazi jitihada zinafanyika kuhakikisha Taasisi hii inakuwa chini ya vijana wasomi ambao wanaweza kuchanganua mambo kwa kadri ya hali ya sasa inavyokwenda. Lakini kuajiri vijana wenye Elimu ya Juu tu, haitoshi kuifanya Taasisi hii kuwa mfano mbadala wa uozo uliokubuhu katika Asasi nyingine za Serikali kama Jeshi letu la Polisi, Asasi zinazoshughulika na manunuzi ya vifaa vya Serikali na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya rushwa na ufisadi hivi sasa yamekuwa sugu katika Asasi nyingi za Serikali katika nchi yetu. Tusiache hili litokee katika Taasisi ya Kuzuia Rushwa Nchini.

Mheshimiwa Spika, tunaposikia Rais wetu anaishia kutoa muda kwa wala rushwa kujirekebisha badala ya kuwatimua kazini na kuwafikisha katika Vyombo vya Sheria, ni wazi kuwa miaka 45 ya utawala wa Serikali imeligeuza suala la rushwa kuwa utamaduni uliokubalika. Rais wetu hapaswi kuishia kutoa muda kwa wala rushwa kujirekebisha. Sisi kama Wawakilishi wa wananchi, tunamshauri Mheshimiwa Rais abatilishe usemi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka Rais anawajua wala rushwa, chombo chenye mamlaka kinafanya nini? Hii inatuonyesha mapungufu makubwa ya uwajibikaji yaliyomo ndani ya Taasisi hii.

Mheshimiwa Spika, ili uwepo wa Taasisi hii uwe na maana mbele ya Watanzania walipa kodi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ifanye yafuatayo :-

- Ilete mara moja katika Bunge hili, Sheria itakayoipa meno Taasisi ya Kuzuia Rushwa ili ijadiliwe na kupitishwa.

- Serikali ni lazima ilete mbele ya Bunge hili majina ya watu ambao ama walikuwa au wamo katika uongozi wa juu wa nchi yetu ambao wamewahi kulalamikiwa kuhusika na rushwa.

- Serikali ni lazima ieleze hatua zote zilizochukuliwa kushughulikia madai kuhusu viongozi hao wa kisiasa na wa Kiserikali hadi hivi sasa na ni wangapi wamethibitika kuhusika na suala hili na kina nani.

- Serikali itoe taarifa rasmi hapa Bungeni kuhusu suala la Balozi wetu aliyekuwepo kule Italia ambaye tunaambiwa amerudishwa nyumbani kutokana na madai ya ufisadi.

- Serikali itoe idadi ya matukio ya rushwa yaliyoripotiwa wakati wa Uchaguzi Mkuu uliopita na yalihusu Majimbo yapi na hatua gani zilichukuliwa dhidi ya watuhumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa hoja zetu, ni imani yetu kuwa Serikali itatoa majibu ya kina kwa maeneo yote tuliyohoji ili Watanzania waweze kuyafahamu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninawashukuru wote kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ambayo ndani yake ina mwelekeo na ina msukumo mkubwa na mategemeo kwa Watanzania. Lakini nina mambo machache ambayo nataka kuyazungumzia katika Bunge lako hili.

Mheshimiwa Spika, kwanza nazungumzia suala zima la Utumishi, Menejimenti ya Umma. Watumishi katika nchi hii ndiyo wachangiaji wakubwa wa kodi katika Serikali na ndio wachapakazi mpaka tumefikia hapa tulipofikia kwa kutoa nguvu zao, elimu yao, mawazo yao na muda wao.

Mheshimiwa Spika, lakini katika baadhi ya watumishi kuna makundi katika utumishi huu. Kuna makundi ya watumishi wanafaidika katika suala zima la manufaa na mapato ya nchi. Lakini pia kuna fungu la watumishi ambalo wanafanya kazi katika mazingira magumu. Watumishi hawa nitawataja kwa ujumla kwa mfano Watumishi wa Mahakama, Afya, Walimu na baadhi ya watumishi wengine ambao wanafanya kazi kwa kipato cha chini sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Waziri kueleza kwamba wanaongezwa mishahara, lakini tuangalie mshahara huu wanaoongezwa na wakati huu tuliokuwa nao.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa watumishi katika Sekta ya Afya. Watumishi ni wachache sana, kwa hiyo watumishi lazima waajiriwe. Katika Sekta ya Afya, watumishi wanapewa kozi katika Idara zetu mbalimbali, lakini baada ya hapo wanakuwa hawaendi moja kwa moja kwenye ajira. Utakuta katika Hospitali, watumishi wanakuwa wachache sana. Madaktari ni wachache sana, Watanzania tuko wengi.

Ukienda Muhimbili pale, kama wiki mbili hivi Daktari anakwenda kwenye Semina watu wanapewa *appointment* kwamba waende kliniki asubuhi saa mbili. Unaambiwa Daktari amekwenda kwenye Semina, unasubiri mpaka saa 10.00. Hii ni dhahiri kwamba Madaktari ni wachache. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie suala zima la kuongeza kuajiri watumishi pamoja na kuwapatia vitendea kazi na kuboresha maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, maisha yamepanda. Kilo ya mchele Sh. 1,000/= na kilo ya nyama ni Sh.2,000/=. Mtu ana watoto sita wanasoma, wanataka nauli za daladala, watoto hao siku hizi kusoma mpaka ufanye na *tuition* ndio mwanao asome vizuri! Kwa hiyo, naiomba Serikali iwaangalie tena watumishi ione ni jinsi gani itazidi kuwaboreshea maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ambalo nataka kuzungumzia ni suala la walemavu. Naomba walemavu waangaliwe. Serikali lazima iangalie jinsi gani itasaidia walemavu katika kuwaondolea umaskini hasa katika ajira. Kuna sehemu nyingine za ajira, walemavu wanaweza wakafanya kazi hiyo. Mtu ni mlemavu labda wa miguu, lakini mikono yake inafanya kazi, anaweza akawekwa mapokezi. Mapokezi zote za Serikali zikawa zinawekwa walemavu wakawa wanapokea wageni wanaokuja pale na kuwaelekeza sehemu husika. Kuna walemavu ambao wanaweza wakafanya kazi! Mtu anaweza kuwa hasikii, lakini anaweza akaelekezwa kazi akawa anaifanya.

Mheshimiwa Spika, naomba walemavu waajiriwe wengi katika Serikali kwa sababu Serikali ndicho chombo pekee ambacho kinaweza kikasaidia kundi hili la walemavu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu rushwa. Rushwa imekithiri. Mimi naamini kabisa rushwa haiwezi kuondoka katika nchi hii bila ya kuanza kukamatwa wala rushwa wakubwa. Kwa sababu gani nasema hivyo? Akikamatwa mkubwa wadogo wote hao watajirekebisha kwa sababu *King* ameshaondoka.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kitu kimoja kwamba, Mheshimiwa Rais, amekiri kwamba rushwa ipo na walarushwa wapo na orodha ya wala rushwa anayo. Watanzania wanangojea kuona hatua ambazo zitachukuliwa kwa kauli yake hiyo aliyoisema. Kuwapa muda walarushwa ni kwamba wanazidi kuangamiza Watanzania kwa sababu wanajiimarisha zaidi. Wanajua Rais ameshatangaza baada ya mwaka mmoja kitakuwa kimbembe. Kwa hiyo, wala rushwa wakubwa ndio wanamalizia malizia shughuli hiyo kwa nguvu zote.

Kwa hiyo, natoa ombi rasmi kwamba, Mheshimiwa Rais awachukulie hatua walarushwa mara moja. Wanatuumiza sana! Wala rushwa wadogo wanasema, sisi bwana, wakichukuliwa wakubwa sisi hatuna matatizo, tutakunja tu mikono yetu. Kwa hiyo, hili liangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, suala ambalo sasa nataka kulizungumzia la mwisho ni la kisiasa. Rais wetu wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, amekiri na ameiambia jamii ya Watanzania kwamba kuna mpasuko wa kisiasa katika nchi hii kwa upande wa Zanzibar. Kwa hiyo, mpasuko huu nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Rais kwamba upo na Watanzania wamekaa macho kwa moyo wote wanasikiliza kitu gani kitatokea kutokana na kauli yake hiyo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba Mheshimiwa Rais ameshaanza kuchukua hatua ambazo bado Watanzania hatujaziona matunda yake na hatujazisikia. Naomba tuambiwe wazi wazi hatua hizi zinavyoendelea kwamba sasa hivi tumefikia hatua fulani, ili tupate moyo kwa sababu hali hii inatugawanya. Lazima Watanzania wajue kwamba Muungano huu wa Tanzania Bara na Visiwani sio Muungano tu, ni Muungano wa damu, ni Muungano wa kisiasa, ni Muungano wa kiuchumi, kwa hiyo hatupendi kuona Muungano huu unatetereka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakuballiana na mimi katika Bunge lako hili, kunaona jinsi gani Wabunge wanavyotoleana kashfa katika Bunge lako Tukufu, mbele yako wewe mwenyewe. Hali hii hatuitaki itokee tena katika nchi yetu. Watoto wako wanaangalia, wanaona na wao watafuatisha sisi tuliokuwepo hapa, kauli zetu tunazozitoa na kashfa tunazozitoa, kizazi chetu kitakuja kuiga mara mbili zaidi ya hayo tunayoyafanya sisi. Kwa hiyo, hili ni la kuangaliwa kwa makini na sio la kufanyiwa masihara.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la kisiasa linatia uchungu zaidi na linadhalilisha zaidi wakati wa Uchaguzi. Kwa kweli hali inakuwa mbaya sana katika jamii. Watu wengi wanadhalilishwa, wanapigwa, wanatiwa ndani, wananyanyasika na hii Mheshimiwa Mbunge aliyetoa hotuba wa Kambi ya Upinzani ameelezea kwa kirefu. Lakini tunaiomba Serikali hii iliangalie sana. Vyombo vya Usalama kwa kweli visiwe wanasiasa. Itafika mahali Watanzania, ndio maana sasa hivi wamekuwa hawana imani na Vyombo vya Usalama kwa sababu ya mateso ambayo wanayapata bila sababu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, tumekaribisha Vyama Vingi katika nchi hii na kama Vyama Vingi tunavikaribisha, ina maana kuna baadhi ya Watanzania watakuwa katika Chama Tawala na kuna baadhi ya Watanzania watajiunga katika Vyama Vingi. Kwa hiyo, hii iheshimike na mawazo ya watu wengine yaheshimike. Lakini chombo cha usalama kisiwe ndio chombo ambacho kinadhalilisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, haya ninayoyasema, nina ushahidi nayo na yamewahi kutokea. Mtu mmekaa mahali mnafanya kazi yenu ya kisiasa, wanakuja wanausalama wanawapiga mabomu, wanawadhalilisha, wanawapiga! Kwa hiyo, tunaiomba Serikali hii ya Awamu ya Nne, Watanzania wana matumaini nayo, Watanzania wanaamini yale yote yaliyofanyika nyuma yatarekebishwa kutokana na kauli ya Rais kwa Serikali ya Awamu ya Nne. Kwa hiyo, tunaomba Vyama Vingi viheshimike, demokrasia ni yetu wote na nchi hii ni yetu sote na wote tunawawakilisha Watanzania. Kwa hiyo sio vizuri Watanzania wakianza kugawanyika kwa sababu ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, athari ya kisiasa ni kubwa sana kuliko kitu chochote na tumeona mifano katika nchi mbalimbali hapa duniani. Kwa hiyo, tunaomba siasa ichukuliwe kama siasa. Sisi hapa tumeona jinsi gani mlivyotuendesha kama wanasiasa katika Bunge lako hili. Huangalii hiki Chama Tawala, huangalii hiki Chama cha Mapinga au Chama cha Upinzani. Wote unatupa haki katika hili Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Vyombo vya Usalama na vyombo vinavyohusika na wale watu wakubwa ambao wanahusika na kutoa amri za udhalilishaji, sasa Rais wa Awamu ya Nne, amesema mwenyewe kwa kauli mbiu yenu kwamba Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya. Basi sasa itumike katika haki na isitumike katika uonevu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI KHAMIS S. KAGASHEKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kweli nimeona kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nchi, katika Ofisi ya Rais kwa hoja yake aliyoitoa leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, ningependa nizungumzie tu kuhusu suala la Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Ningependa ni-*focus* hapo. Kwanza naomba niseme kwamba, Watumishi wetu wa Umma ni watu ambao kwa kweli tuseme kwamba tuna-*recognize* kazi yao ambayo wanaifanya katika Taifa hili kwa muda mrefu. Nimeona ni vizuri nilizungumzie suala hili na nitaje machache ambayo nadhani ningependa kuchangia,

labda yanaweza yakasaidia katika mjadala huu kwa suala lote la Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, binadamu ana kiwiliwili, lakini pia ana roho. Roho ya Serikali naamini kabisa kwamba ni Mtumishi wa Umma (*Civil Service*). Kwa nini nasema hivi? Ni kwa sababu tumefanya uchaguzi kama Mataifa, Uchaguzi Mkuu, tumemchagua Rais wa Awamu ya Nne akatengeneza Serikali yake, lakini ninaamini kabisa kwamba Rais katika utekelezaji wa shughuli zake za Kitaifa atategemea sana Utumishi wa Umma (*Civil Service).* Vivyo hivyo, naamini kwamba Waziri Mkuu katika kutekeleza majukumu yake, atategemea sana Utumishi wa Umma (*Civil Service*). Naamini kabisa Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri katika shughuli zao wanategemea Utumishi wa Umma (*Civil Service*)

Mheshimiwa Spika, *Civil Service* ni chombo ambacho kimekuwepo. Ni kidogo ukilinganisha na jamii ya Tanzania, lakini kazi kinachofanya chombo hicho ama kazi ambayo wanashughulikia *Civil Servants* wa nchi hii ama popote pale duniani inagusa maisha ya watu wote na hapa Tanzania, tunaweza kusema inagusa maisha yetu ya kila siku. Sasa kwa nini nimeona nizungumzie juu ya suala hili la *Civil Service?*

Mheshimiwa Spika, Mtumishi wa Umma ni kwamba Rais wetu na kauli mbiu yetu sasa hivi tunazungumzia juu ya Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. Lakini nafikiri ipo haja kwa kweli kujiuliza kama *Civil Service* yetu iko *equipped* kwa sababu hii ni Awamu ya Nne na naamini kabisa Awamu ya Nne sio lazima iwe ni *continuation,* lakini yako yale ambayo ni ya Awamu ya Tatu watakwenda nayo, yako ambayo ni mapya ya Awamu ya Nne ambayo wamekuja nayo na katika hayo tuna hii kauli mbiu ya Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya.

Mheshimiwa Spika, sasa je, tunaamini kabisa na Mheshimiwa Waziri anaweza akalizungumzia hili labda. Tunaamini, ama tunayo matumaini kabisa kwamba *Civil Service* yetu tuliyonayo itakwenda na hii Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya na itaweza. Kwa sababu Mheshimiwa Rais hotuba yake aliyoitoa katika Bunge mwanzoni mwa mwaka huu, nafikiri wakati anafungua Bunge hili, kwa kweli ilikuwa kama nilivyosema ni hotuba ambayo iligusa kila kitu. Sasa utekelezaji wa hayo, mimi ndiyo nauliza na ningeomba Mheshimiwa Waziri ambaye anahusika na eneo hili la Utumishi wa Umma, kweli anayo imani hiyo kwamba *Civil Service* yetu imekuwa katika hali ambayo tunaamini kabisa itakwenda na hii Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya.

Mheshimiwa Spika, hii inanipa nguvu zaidi kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa wakati tulipokuwa tunazungumzia juu ya hotuba yake na nakumbuka ingawa sina hotuba yake, lakini kuna mahali ambapo aliposema kwamba Watendaji wa Serikali ambao hawawezi kwenda na mdundo, nafikiri alitumia maneno hayo, kwamba hawawezi kwenda na mdundo watupishe. Mdundo wenyewe ulikuwa ni Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya. Hayo ndiyo yalikuwa maneno yake Waziri Mkuu. Sasa hayo mimi nasema, ningependa tufahamishwe vizuri kama Watendaji wetu tayari tumewaweka katika ari ambayo tunaamini kabisa watakwenda na Ari Mpya, Kasi mpya na Nguvu Mpya ili waweze kwenda na mdundo ambao tunaudunda hivi sasa. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, hili suala la *Civil Service* iko haja ya kulitazama kwa undani zaidi, kwa sababu tunapozungumzia masuala ya kilimo, natoa tu mfano, matatizo ambayo yanajitokeza utakuta kwamba jibu letu sote liko katika *Civil Service,* wataalamu katika maeneo hayo ambao ni watu wa kilimo. Tunapozungumzia Mahospitali, Wagonjwa wetu, Madaktari, Wauguzi wetu, majibu utakuta tunasema tunakwenda katika Utumishi wa Umma. Tunapozungumzia juu ya elimu kama ni mwanafunzi, kama ni Walimu kama ni suala la mashule, madarasa, bado tunazungumzia *Civil Service,* ndiko huko tunakotafuta majibu. Kama tunazungumzia wafanyabiashara vipi watafanya biashara, leseni zao watapata vipi, bado tunarudi katika *Civil Service*. Kwa hiyo, mimi naona ni eneo ambalo kidogo sio kwamba nataka kulipa umuhimu, lakini ni suala muhimu kwa sababu sote tunategemea hapo.

Mheshimiwa Spika, sasa tumemsikiliza Mheshimiwa Waziri, amezungumzia juu ya *review* ambayo inafanyika ili kuweza kuona kwamba mishahara inakwenda juu. Amezungumzia juu ya *conditions of service,* lakini kusema kweli, mimi ninavyojua wafanyakazi wengi ingawaje wanafanya kazi katika *Public Service,* lakini kuna wengi ambao wamekata tamaa, kuna wengi ambao wamevunjika mioyo, kwa hiyo, iko haja nadhani kwamba, Serikali ingelitazama kwa sababu nguvu yetu sisi ni Watendaji. Ni kweli *speed* yoyote ya Serikali yoyote tukubali, tusikubali, *speed governors* ni *Civil Servants* kwa sababu wale ndio wanaoweza kutuwezesha sisi twende kiasi tunachoweza kwenda ama wanaweza wakaweka *break* katika mambo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema kwamba inapokuja katika haki zao, maslahi yao, mishahara yao, pensheni zao, nafikiri ni vitu ambavyo tungevitazama na hapa ningeweza kushauri kwamba mambo haya yangekuwa yanatazamwa mara kwa mara, yawe *reviewed* mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba wanakuwa *motivated,* wanakuwa na moyo na kuona kwamba tunaweza, katika njia ambayo tunakwenda nayo katika utekelezaji wa Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ningependa nitoe mifano midogo wakati tunazungumzia juu ya mambo ya *Service* kwamba, sio vibaya kutazama hata nchi nyingine huko wanafanyaje. Hii natoa tu kama mfano, yaani ya kujaribu kuona kwamba sisi kama Tanzania tusijitazame kama ni Kisiwa na tukajitazama kwamba tumejifungia. Lakini chukua nchi kubwa kama Marekani kwa mfano, utakuta katika maeneo ya *high tech* ambayo wao wanasema kwamba ni *high tech* na mimi nimeweza kupata bahati na nafikiri na wengine humu wamepata bahati ya kwenda *Silicon Valley Saint Francisco* ambako ndiko *software industry* nyingi inakofanyika.

Mheshimiwa Spika, ukifika kule utakuta wanaofanya kazi katika *software industry* kule sio Wamerikani wa pale, wengi ni Wahindi. Wengi ni watu ambao wametoka India, lakini kwa kuwa nchi ile inajua ina mahitaji katika maeneo hayo, kwa hiyo, imeweza hata kufanya urahisi wa mambo ya usafiri, visa na kadhalika kuhakikisha kwamba wanapata watu ambao ni wataalamu wanaoweza kuweka utaalamu katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, eneo lingine juzi juzi tu kiasi cha miezi miwili iliyopita, Marekani wametangaza ulimwengu mzima kwamba wanataka Ma-*nurse* katika hospitali zao za Marekani. Wametoa tangazo katika *Embassies* zao dunia nzima, wameweza ku-*relax* mambo yao ya nauli ya usafiri na *visa*. Sasa mimi nasema ni kwamba hii ni nchi unaona kabisa inaweka mkakati wa kuweza ku-*attract* watu ambao wana uwezo waweze kuja kusaidia katika maeneo ambao wanaona wao hawana utaalamu ama wana upungufu wa watu ambao wanaweza waka-*contribute*.

Sasa mimi nilikuwa naomba Ofisi ya Rais hasa Waziri anayeshughulikia Masuala ya Menejimenti na Utumishi, wangeweza wakatazama mambo kama hayo na kutazama ni maeneo gani, kwa sababu ukitazama tangu tumepata uhuru tumekuwa tunazungumzia suala la mafunzo, tulikuwa tunazungumzia tutakapowapa mafunzo watu wetu katika maeneo, ni suala ambalo limekuwepo kwa muda mrefu. Sasa naomba, kama Mheshimiwa Waziri angetazama tukawa na chombo maalum ambacho ni cha kudumu cha kuweza kutazama masuala haya, kutazama kwanza *interests* za wafanyakazi wao na kuona jinsi tunavyoweza kuboresha mambo yao ili waweze kutufanyia kazi yetu vizuri na waweze kujenga Taifa vizuri na wengi wana moyo kabisa wa kufanya kazi, lakini kiasi cha kuwatia moyo.

Lakini pili, kutafuta njia na mbinu za kupata wataalamu zaidi ambao tunao Watanzania wengi, sio kwamba lazima tupate watu wa Mataifa mengine, wapo Watanzania ambao wapo nchi za nje sasa tusiseme tu kwamba wapo Watanzania waje tu kwa sababu ya uzalendo, lakini tutengeneze *conditions* na njia za kuweza kuwapata waje waweze kuweka mchango wao katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi yangu ni hayo na nasema naunga mkono hoja moja kwa moja bila ya kipingamizi chochote. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, katika suala la Menejimenti na Utumishi wa Umma kuna mambo mawili, matatu ambayo nataka niyazungumzie. Kwanza kukaimu kwa Maafisa mbalimbali katika Idara mbalimbali za Halmashauri na sehemu nyingine za Utumishi wa Umma. Suala la ukaimu limekuwa kubwa sana, kwa hiyo, ningeomba Wizara iangalie upya kwamba Makaimu wamezidi kuwa wengi. Utakuta Kaimu Daktari, Kaimu *DED*, Kaimu Afisa Kilimo, Kaimu Afisa Ardhi, sasa suala la kukaimu na Kaimu juu ya Kaimu kunazorotesha kazi kiasi fulani, kwa sababu kaimu hana maamuzi.

Wakati mwingine ukimwendea kwa ajili ya kufanyia *service* kitu fulani au suala fulani kwa wananchi, anasema mimi Kaimu, sina uamuzi wa mwisho. Suala linalala pembeni.

Kwa hiyo, ningeomba kabisa suala la Makaimu lichunguzwe upya. Kama kuna kaimu anaweza, basi athibitishwe kazini awe Mkuu wa Idara kamili. Kwa hiyo, masuala haya yachunguzwe katika *Council* zetu na maeneo mengine ya kazi nchini kwamba suala la Makaimu sasa liangaliwe ili lipungue.

Suala la pili, ni upungufu wa Madaktari. Madaktari wamepungua sana. Mimi ningeomba mpango maalum ufanywe angalau Madaktari waongezwe katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la Semina kwa Viongozi wetu mbalimbali. Suala la Semina kwa Wakuu wa Idara katika Halmashauri zetu zimezidi sana, kiasi kwamba kazi hazifanyiki. Semina kwa Ma-*DED,* sasa hivi wameanzisha Semina kwa Waganga Wakuu wa Wilaya na wa Mikoa, Semina kwa Maafisa Kilimo, Semina kwa Maafisa Elimu, kwa kweli zimezidi. Mimi ningeshauri Wizara sasa zipange kwamba Semina zitakuwa labda baada ya miezi sita au mwaka mmoja kuwaita kutoka Wilayani kwenda Dodoma au Dar es Salaam. Kwa sababu ukiweka miezi mitatu, mitatu Semina kwa Madaktari kwa mfano, yaani kabla hawajarudi kazini, kwa sababu wengine wanakaa mbali, tayari wanaitwa tena. Kwa hiyo, wanacheza njiani tu. Kwa hiyo, wanaamua hata kutokwenda kwenye Vituo vyao vya Kazi. Kwa hiyo, kama mtu kwao ni Dar es Salaam anaamua kukaa kwanza kusubiri Semina, harudi.

Mheshimiwa Spika, kwa mtindo huo wa Semina na wenzetu hawa niliowataja kwa maana ya Maafisa Kilimo, Maafisa Ardhi, Elimu na *DED* zimezidi. Tungeangalia upya, kwa sababu kazi zinalala Maofisini. Hawa wenzetu hawapo, wanakaimu juu ya kaimu. Sasa ukimweka kaimu mharibifu, basi kazi inaharibika zaidi. Tuangalie suala la Makaimu.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninataka kuzungumzia ni kwenye ukurasa wa 21. Mkakati wa kuongeza idadi ya wanawake toka asilimia 30 mwaka 2005 kufikia asilimia 50, mwaka 2010. Mwisho wa uchaguzi, ndiyo mwanzo wa maandalizi ya uchaguzi. Suala hili lisichukue muda, kama kuna mkakati maalum ambao utawekwa kwa ajili ya kuwafanya wanawake katika ngazi ya uamuzi kufikia asilimia 50 lisichukue muda, tupewe mikakati, maelekezo, tuonyeshwe, tuambiwe tutafanyaje ili kufikia asilimia hii ya 50. Likichukua muda na kutupa karibu na uchaguzi, tutahangaika sana. Ni afadhali sasa hivi mipango ifanywe, wanawake tuelezwe ni mpango gani, ni mkakati gani ambao sisi tutapewa ili kufikia asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kumalizia ni suala la MKURABITA, suala la kurasimisha rasilimali za wananchi. Sasa hivi wananchi baada ya kusikia kwamba tutapewa mikopo kupitia ardhi zetu, kupitia mali tulizokuwanazo, wanangoja itakuaje. Kwa sababu mali wanazo tayari, watu wana ardhi, majumba, watu wana biashara wanazozifanya sasa wanasubiri itakuwaje. Sasa ningeshauri suala hili lisicheleweshwe, lianze kushughulikiwa mara moja ili watu hawa tuwanusuru katika maisha yao. Nimeona kuna Wilaya 26 ambazo zitaanza kushughulikiwa. Sasa ningeomba kati ya Wilaya hizi 26, basi wasisahau Mikoa ile ya pembezoni ambao ndiyo wananchi wanataabika zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nichukue nafasi hii kwa kweli kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kabla ya kuchangia, kwanza ningependa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Wataalam wake kwa kuandaa hotuba hii. *(Makofi)*

Vilevile, napenda niwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Chambani, kwa imani yao kwa kunichagua mimi na Chama changu cha *CUF* kuja hapa Bungeni na nawahakikishia kwamba nitafanya kazi karibu nao siku zote. Naomba imani hii waendelee kuwa nayo ya kuchagua *CUF* daima.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuondoka kwenye Mkutano wa tatu wa Bunge, nilikutana na kiongozi mmoja wa *TASAF*, ambaye alikuwa na shukurani mbili kuhusu *TASAF,* lakini vilevile alikuwa ana maombi ya aina mbili. Kwanza, alishukuru kuwa, kwa kuwa yule sungura ameongezeka mara hii, kwa hiyo, alikuwa anatoa shukrani kubwa kwa Serikali kwa fedha za *TASAF* kwa awamu hii ya pili. Lakini alikuwa anaomba kwamba kutokana na hali ya umaskini uliokithiri, basi kiwango hiki kizidi kuongezeka ili wananchi wengi wanufaike.

Lakini vilevile alikuwa anaomba kuwa mgao huu wa *TASAF* kwa Zanzibar ungefanywa kama vile Tanzania Bara kwa kuwa katika Tanzania Bara kila Mkoa unakuwa unapata *share* yake. Maana pengine kuna makaka wakubwa na wadogo kule. Kwa hiyo, alikuwa analeta ujumbe kwamba kama tunavyofanya huku Bara, basi tufanye vilevile kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nataka kusema kwamba, kwanza nikiri kwamba nimepata shida kuijua hii *TASAF* iko chini ya Wizara gani na nimeuliza Waheshimiwa Wabunge mbalimbali, lakini kila mmoja alikuwa ananipa jibu tofauti na hata jana niliomba msaada wako, nilivyotaka kuchangia kuhusu *TASAF.* Lakini nadhani majibu uliyonipa unayafahamu. Sasa leo nilivyoona imeelezwa katika hotuba ya Waziri wa Nchi, nikaona nijipenyeze hapa hapa nitoe mchango wangu ambao sio mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)*, nafikiri uko katika nchi mbalimbali duniani na lengo lake kubwa ni kupunguza umaskini katika ngazi ya jamii. Hapa Tanzania umeanza katika mwaka 2000 hadi 2004 katika Wilaya 40 za nchi nzima. Lakini baada ya maendeleo na mafanikio ya awamu ya kwanza ya *TASAF*, ndiyo ikaanza awamu ya pili ambayo imenza mwaka 2005 na itaendelea hadi mwaka 2009. Sasa chochote ambacho kina mafanikio, basi vilevile huwa kina matatizo. Matatizo mengi yalijitokeza nafikiri katika awamu ya kwanza na bila shaka katika awamu ya pili, yatafanyiwa kazi ili yasijitokeze tena.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kueleza matatizo ambayo yameshaanza kujitokeza katika Jimbo langu na mfano wangu utajikita kwenye Jimbo langu la Chambani kwa *TASAF* awamu ya pili.

Mheshimiwa Spika, matatizo makubwa ni uelewa duni wa wananchi katika Jimbo langu kuhusu dhana nzima ya madhumuni ya *TASAF* na nasema uelewa kwa sababu kama mtu anaelewa nini lengo la *TASAF,* basi haya ambayo wanayafanya hawawezi kuyafanya. Baada ya taarifa za *TASAF* kufika katika Jimbo na wananchi wakajua kwamba awamu ya pili ya *TASAF* inaanza, basi viongozi wa maeneo, ambao kule sisi tunawaita Masheha, (Jimbo langu limegawanyika katika sehemu nne na kila sehemu inaitwa Shehia na hizi Shehia zinaongozwa na watu wanaoitwa Masheha. Naweza kuwafananisha Masheha labda na Wenyeviti wa Vijiji hapa Tanzania Bara. Hawa ni watu ambao wameteuliwa na Serikali wanawakilisha Serikali katika mambo yote katika utendaji.) baada ya taarifa hiyo kufika baadhi wanaanza kwenda Vijijini kuwafahamisha wananchi kuhusu miradi ambayo wananchi wenyewe wangependa kuiibua. Kwa hiyo, kazi hii waliifanya Masheha.

Lakini baada ya hapo, awamu ya pili ni pale ambapo fomu zilianza kuletwa ili wananchi ama kwa Shehia nzima au kwa Kijiji au kwa makusudi maalum wajaze fomu hizo. Hapa ndipo palipokuwa na matatizo. Ni kwamba, fomu hizo katika baadhi ya Shehia zilikuwa zinatolewa kwa siri kwa wale Masheha wenyewe ambao wanafikiri kama hawa wanaweza au hawa ni watu ambao wanaweza kuibua miradi. Wengine wakienda kudai, fomu hamna. Sasa kwa sababu sisi ni Wawakilishi wa Wananchi, tulipopata taarifa hizi kuwa fomu zilitolewa kwa upendeleo, tulifanya Mikutano katika Shehia zote kukutana na Masheha na Kamati za Maendeleo pamoja na baadhi ya wananchi ambao walikuwa na malalamiko. Tulifanya Mkutano katika Shehia ya Mzingani, Ngwachani kwa pamoja na kuwasikiliza wananchi matatizo yao. Katika Shehia hizi mbili, tuligundua kuwa, wananchi wa Mizingani walishirikiana vizuri na Sheha wao na wakachagua mradi mmoja tu wa kujenga Kituo cha Afya Mizingani. Lakini wananchi wa Shehia ya Ngwachani hawakupata maelekezo mazuri kutoka kwa Sheha wao. Kila mtu au kila kikundi kilikuwa na mradi wake, miradi ambayo kwa kweli haikuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukaa nao pamoja mimi na mwakilishi wangu, tukaongea nao wakakubaliana kufanya marekebisho kwa hilo. Lakini tulipokwenda katika Shehia ya Ukutini na Chambani, Sheha na Kamati yake walifika katika Mkutano huo. Sheha wa Ukutini alikuja lakini Sheha wa Chambani hakufika. Katika shehia ya Ukutini matatizo yalikuwa ni yale yale, kuwa baadhi ya watu tu wamepewa fomu kujaza katika miradi ambayo kwa kweli haikuwa hata ya msingi, lakini wengine ambao walikuwa tayari na miradi wameshaanzisha, wakanyimwa.

Sasa tukaongea nao wakakubaliana kurekebisha, lakini Sheha wa Chambani alikataa kuja katika Mkutano, tulipomwita siku ya pili, akakataa vilevile. Sasa maelezo ambayo tulikuwa tumeyapata hapo ni kwamba, baadhi ya wananchi walidai kuwa fedha za *TASAF* ni fedha ya CCM. Kwa hiyo, wale ambao hawahusiani na CCM, sio wana-CCM, hawakuwa na haki za msingi za kupata fedha kwa ajili ya miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kama hiyo ni kweli, sisi tukajibu kwamba, misingi mikuu ya *TASAF* ni kutokuwa na upendeleo wa kutofungamana na siasa. Wao wana misingi ya kisiasa, watakuwa wamevunja misingi mikuu ya *TASAF*. Lakini la pili, tukawaeleza kwamba, fedha ya *TASAF* ni mkopo wa Benki ya Dunia. Benki ya Dunia imechangia Dola za Kimarekani milioni 150, Dola milioni 129 ni mkopo na Dola milioni 21 ni msaada. Kama ni mkopo, Watanzania wote ndiyo wanaolipa mkopo ule, sio wana CCM tu, walipa kodi wetu, wananchi wote tunachangia mkopo huo.

Lakini vilevile, kuna mchango wa Serikali wa Shilingi bilioni 15, ambao kama ni Serikali, sote tunahusika na hilo. Kwa hiyo, tafsiri hiyo haikuwa sahihi kwamba pesa za *TASAF* ni pesa za CCM na tulifikiri kuwa ni njia moja ya kuleta ubabaishaji kwa sababu tuliona baadhi ya miradi ambayo imechaguliwa ambayo ni miradi endelevu. Kwa sababu mradi endelevu lazima ukubalike, ufikie viwango. Sasa miradi yenyewe hiyo ilikuwa ni ya wasiwasi. Tunatahadharisha kwamba kama hali ndiyo hii, basi madhumuni ya *TASAF* hayawezi kufikiwa kwa sababu kuna Viongozi ambao wamejielekeza katika kujinufaisha wao binafsi. *(Makofi)*

Kwa mfano, wanasema wamechagua mradi katika makundi maalum, wanasema mradi ambao katika kaya ambayo kuna watu wanaoweza kufanya kazi, lakini kuna upungufu chakula. Sasa kama ni *excuse,* unampa mtu mradi kwa sababu ni maskini, lakini ana uwezo wa kufanya kazi, kwanini iwe siri? Kwanini usitangaze kwa wote? Kwanini usitoe fomu kwa watu wote wakapata halafu ikaonekana kwamba *well* mradi huu ni ghali na huu si ghali. Lakini kitendo cha kuficha, unatoa fomu usiku usiku, kwa kweli unapoteza malengo mazima na madhumini mazima ya kumwondolea au kumpunguzi Mtanzania umaskini.

Mheshimiwa Spika, kwa hili nilitaka lifahamike wazi wazi, vyombo vinavyohusika viangalie hilo, haidhuru wenyewe baadaye wanapitia wanaona, wanaangalia. Lakini ilikwishatokea hapo kabla kwamba baadhi ya miradi ambayo imechukuliwa na *TASAF* imekuwa ya ubabaishaji, haifiki popote. Sasa fedha ya Serikali inapotea, lakini malengo kwa kweli hayapatikani. Kwa hiyo, nilikuwa nasisitiza yafuatayo:-

Kwanza taaluma iwe kubwa zaidi, wananchi waelimishwe wajue kwamba hii *TASAF* ni kwa ajili ya wote na sio kwa ajili ya Chama fulani au watu fulani, ukiwa CCM, ukiwa *CUF,* ukiwa CHADEMA unahusika na *TASAF*. Lakini nafikiri vilevile tatizo la kujenga uwezo labda, liangaliwe vilevile. Pengine Watendaji bado hawajajengewa vizuri uwezo na inawezekana wanafanya hili kwa kutojua. Kwa hiyo, Serikali ina wajibu wa kuwafahamisha hili, kulieleza ili kila mwananchi ajue kwamba *TASAF* ni kwa ajili ya wote. *(Makofi)*

Lingine kuhusu *TASAF* ni kwamba, inatakiwa Mfuko wa *TASAF* uwe endelevu. Najua kwamba Mfuko wa *TASAF* una muda wake. Baada ya mwaka 2009 utakuwa umemalizika. Tunategemea labda Serikali itaendelea kuomba msaada au mkopo, lakini tunasema, uwe endelevu, kwa maana ya kwamba, bila kupata mikopo ya Serikali kutoka

*Word Bank* au sehemu nyingine, sijui itakuwaje. Kwa sababu *TASAF* inatoa pesa kwa wananchi. Sasa inawezekana kwamba, miradi inayofanywa inakuwa endelevu, mingine inakuwa ya hujuma. Sasa kama inakuwa ya hujuma hakuna kilichopatikana. Lakini hata kama inakuwa na faida, faida ile inakwenda kwa wananchi katika kuwaondolea umaskini. Kwa hiyo, ili *TASAF* iendelee katika miaka inayofuata, inabidi hizi hatua za kuendelea kuisaidia *TASAF* mfanye mapema ili kufikia mwaka 2009 ambayo ndiyo mwisho, basi tusichelewe kama tulivyochelewa. Mara hii ianze haraka ili wananchi waweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nami naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu na kabla sijasahau, naomba na mimi nianze kwa kuunga mkono hoja hiyo kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Utumishi na Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora, wa Serikali hii ya Awamu ya Nne. Naomba na mimi niwape salamu kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Peramiho, wanasema wana imani sana na nyie katika kutatua matatizo mbalimbali yanayohusiana na utumishi bora katika nchi yetu na masuala ya utawala bora. Kwa hiyo, watawapa ushirikiano wa kutosha na wanawaomba muwape ushirikiano wa kutosha sana katika Jimbo lao la Peramiho na Halmashauri yao ya Wilaya ya Songea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayo machache ya kuchangia. Baada ya kusikiliza hotuba hii, nimeona kabisa kwamba mipango iliyowekwa na viainisho vyote ambavyo viko katika hotuba hii vinatupa mwelekeo wa safari yetu huko mbele.

Mheshimiwa Spika, lakini katika safari hiyo, mimi nilikuwa naomba nizungumze haya yafuatayo:-

La kwanza, bado liko tatizo kubwa sana la Watendaji wetu wa Vijiji na Watendaji wetu wa Kata. Watendaji hawa mpaka sasa hivi haijulikani kama tayari wameshaingizwa katika Utumishi wa Umma kama ilivyoamuliwa na mpaka sasa hivi haijulikani suala lao la mishahara na hatima ya mishahara itakuwaje. Watendaji wengi mpaka sasa hivi, utumishi wanapoleta utaratibu wa mishahara ya watumishi wengine, Watendaji hawa wa Kata na wa Vijiji hawaonekani katika *pay roll* yoyote na hivyo bado wanahangaika sana kujua hatima ya mishahara yao na huku wakiendelea kufanya kazi za utumishi katika Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine kumekuwa na mahangaiko makubwa sana ya Watendaji wetu. Wakati mwingine wanaambiwa lazima wakidhi viwango fulani vya elimu, wakati mwingine wanaambiwa viwango vile vya elimu sio tena suala la msingi katika ajira yao. Basi kwa kweli wamekuwa katika mahangaiko makubwa sana, hawajui wako ndani ama wako nje, hawana mishahara, wakati mwingine wanaweza wakamaliza miezi miwili, miezi mitatu, miezi sita, mwaka, miaka, hawaelewi kabisa mishahara yao iko wapi.

Kipindi kile Watendaji hawa wa Vijiji na wa Kata kutoka katika mikono ya Halmashauri zetu, huko nyuma walikuwa na malimbikizo mengi sana ya mishahara yao. Lakini mpaka leo haijulikani nani hasa anayehusika na malimbikizo hayo na nani ambaye yuko *responsible* kuwalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba sana, kwa Kasi ile ile Mpya, Ari Mpya na Nguvu Mpya, sasa hivi tumeamua miradi mikubwa ya maendeleo ya wananchi inapelekwa kwenye Vijiji na kwenye Kata huko huko pamoja na *extension officers,* lakini Watendaji hao wa Vijiji na Watendaji wa Kata ndio wasimamiaji wakubwa wa maendeleo ya wananchi wetu. Kwa hiyo, tusipoangalia kwa jicho ambalo halina husuda, kwa kweli tutawakatisha tamaa sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri, afuatilie sana suala hili kama ni la kimtambuka kwa maana ya kwamba Wizara ya Fedha, TAMISEMI na wao wanahusika kwa kiwango cha kutosha, basi mimi nadhani ni muda muafaka sasa wa kumaliza kero hii ya Watendaji. Naomba sana suala hili lipewe kipaumbele

Mheshimiwa Spika, lakini yako mambo mengine yanayoendana na suala zima la Utumishi wa Umma. Ninaomba nizungumzie suala la Walimu. Walimu ni Watumishi wa Umma katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kwamba hakuna Watumishi wa Umma wanaohangaika kama vifaranga visivyo na kuku kama Walimu wetu. Walimu wanamaliza mafunzo yao, katika Vyuo vya Diploma, Vyuo vya *Grade A,* wanatakiwa waajiriwe katika Shule mbalimbali, lakini Walimu wanakaa muda mrefu hawana mshahara, huko katika Majimbo yetu unaona huruma! *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sana!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, mabinti wadogo wanakaa miaka, hawana mshahara! Hebu fikiria huyu Mwalimu akapate wapi fedha za kujikimu mwaka mzima, lakini wakati huo anafanya kazi! Kuna hatari kubwa ya maambukizo ya UKIMWI, sasa hivi tuna hatari kubwa ya kila adha ya dunia hii na vishawishi mbalimbali. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo ndiyo!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, sasa ningependa kuona Serikali kwa mtambuka huo huo, Wizara ya Utumishi, Fedha, TAMISEMI, hebu, waje na ajenda ya pamoja ili Walimu hawa waliomaliza mafunzo yao kabla ya kwenda kupata ajira katika Kituo cha kazi, suala la mishahara na mafao liwe limeshakamilika. Tutawapa moyo kabisa wa kufanya kazi walimu wetu. *(Makofi)*

Lakini sio Walimu tu, hata Watumishi wa Sekta nyingine kama Afya, matatizo ni haya haya! Mimi nakumbuka, kuna kipindi wapiga kura na hasa watumishi walisema

Mheshimiwa angalau hata Walimu wanazungumzwa, sisi watumishi wa afya ndio hakuna hata anayetukumbuka, lakini tuna kero kubwa sana. Kwa hiyo, mimi nafikiri wakati muafaka umefika, mimi naamini kabisa kama Wizara hizi zitashirikiana, masuala yao ya kupandishwa mishahara, kupandishwa vyeo hayataweza kuchukua muda na tulishasaini Mikataba ya Huduma Bora kwa Wateja, hivi utekelezaji wa mikataba ile ukoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba utekelezaji wa Mikataba ya Huduma Bora kwa Wateja, isiishie kwenye Mawizara tu, iwe nayo ni Sekta Mtambuka mpaka huko chini kusudi iweze kuendana na utendaji wa Kasi Mpya na Nguvu Mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niendelee kusema kwamba, bado liko tatizo lingine katika suala la Walimu wanapohamishwa taratibu za kuwahamisha kutoka kituo kimoja kwenda kingine, zinatekelezwa kabisa katika ngazi za Wilaya. Mwalimu huyu atamaliza miezi miwili akisubiri kibali kutoka Tume ya Utumishi wa Umma, ama sijui Tume ya Utumishi ya Walimu, kibali kipatikane ndipo waweze kuhama kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine. Miezi ile miwili ana kasi na ari ya kufundisha, kibali hakijafika, Shule inayomuhamisha imepunguza Mwalimu na Shule inayomtegemea haina Mwalimu. Lakini mshahara anaendelea kupokea na yeye kasi ya kufundisha anayo, lakini haruhusiwi na kituo alichotoka, wala haruhusiwi kituo anachokwenda, anabaki tu yuko hewani anasubiri utekelezaji wa majukumu ukamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri kwa nini tusiamue kukasimu madaraka hayo kuyaondoa huko katika utumishi tukawaachia Wizara ya Elimu wenyewe?

**MBUNGE FULANI:** Sawa sawa!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Washirikiane na TAMISEMI kule kwenye Halmashauri, kusudi mambo haya yawe yanakwenda kwa haraka na utekelezaji wa majukumu ya Serikali na masuala mazima ya utendaji yaweze kufanikiwa vizuri. Naomba sana, hilo tuliangalie, tunahamisha Walimu wetu lakini muda mwingi wanapoteza wako njiani, hawahami, hawaripoti, hawafanyi nini na inakuwa ni hasara kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiwango cha pesheni kwa wazee wetu, tunaishukuru sana Serikali, imewarejesha wazee wetu, baba zetu, mama zetu, binamu, shangazi, mjomba na kila mtu, wamerudi kwenye pesheni zao. Lakini mpaka sasa, kiwango hiki cha Sh. 20,000/= mimi nafikiri kwa kasi mpya tunayokwenda nayo, wao tutawaacha nyuma. Nilikuwa naomba, hebu Serikali iwafikirie basi, mambo haya ya makusanyo ya kodi yanavyoongezeka, hebu tuwaongezee kidogo na hawa wazee waendelee kuongeza maisha. Nafikiri kwa kweli kiwango cha pesheni bado ni kidogo, na ninaomba sana tuwafikirie ili tuwaongezee angalau na wao wawe na unafuu sana wa maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeshazungumza suala la upungufu wa watumishi katika sekta mbalimbali, sasa niendelee kutoa mfano katika Sekta ya Maendeleo ya Jamii. Tumeona kabisa, kwa mfano kwenye Jimbo langu nina Kata 14, lakini Maafisa

Maendeleo ya Jamii ninao saba, Kata saba hazina. Kwa hiyo, kama alivyosema mchangiaji aliyepita, basi imekuwa ni suala la kukaimu, kukaimu na mtu anayekaimu unajua ni masuala ya kukaimu tu, sio masuala ya kutenda kazi kwa kadiri ya jukumu alilopewa.

Mheshimiwa Spika, labda nisimalize kuchangia hotuba hii, bila kuishukuru Serikali kwa mpango huu wa *TASAF*. Naomba niseme kwamba, mpango wa *TASAF* ni tishio kabisa kwa maendeleo ambayo yatakaondoka kwa kasi kubwa katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa kweli katika suala la *TASAF,* mtu atakayesimama na kusema *TASAF* haifai, kwa kweli huyo tumwongope sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hafai kabisa!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, *TASAF* imefanya mambo makubwa sana katika kipindi cha majaribio na mimi naamini kabisa mfumo wa *TASAF* kama ulivyoainishwa na unavyofanya kazi katika nchi yetu ya Tanzania, utaleta maendeleo makubwa sana ya kupambana na umaskini.

Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali, uzi ukazwe zaidi, *TASAF* iendelee kung'ara katika nchi yetu na kadri ilivyowafikia wananchi wote wa Tanzania, iendelee kufika na kutekeleza programu na mipango hiyo. Ni ushirikishwaji wa aina yake kabisa wa jamii ya Watanzania wenyewe na hasa walalahoi na wale maskini kabisa katika maeneo hayo. Tunaomba tu utekelezaji wa ratiba ya miradi uendane na kadri ya mipango tunayojiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kugundua umuhimu wa MKURABITA na ninaomba nimpongeze sana Mwenyekiti wetu wa MKURABITA, Mama yetu Mheshimiwa Anne S. Makinda. Toka alipoanza ajenda hii ya MKURABITA, sasa ninaomba niseme kwamba tumeona mwanga wa MKURABITA unakuja kwa kushirikiana na Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunamwambia Mheshimiwa Anne S. Makinda kwamba wananchi tunasubiri utekelezaji wa kutumia MKURABITA ili kujikwamua kwenye umaskini tulionao. Tuna ardhi za kutosha, tuna mashamba ya kutosha, tunasubiri vitambulisho, tunasubiri tukakope hizo fedha huko tununue matrekta, tufungue miradi mikubwa ya kuendeleza jamii ya Watanzania katika mpango huu mzuri sana wa MKURABITA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba niwapongeze sana Makatibu Wakuu wa Wizara hizo, akina Mama Chapakazi, akina Mama Mahiri, tunawafahamu sana kwa matendo yao, kwa tabia zao na kwa uchapakazi wao walionao. Kwa hiyo, kwa kweli mimi naomba kusema kwamba hao akina mama wataongoza vizuri sana Wizara hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niwapongeze Watendaji wote wa *TASAF*, MKURABITA na zile Taasisi zote ambazo zinafanya kazi chini ya Ofisi ya Rais. Kwa

kweli tumeonja matunda yenu na tunawatakia kila la kheri, Mwenyezi Mungu awajalie muwape *support* Mawaziri wetu ili kweli maneno yenu yaweze kutimia na wananchi waweze kufanikiwa kwa kiasi cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nikushukuru tena wewe kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi ya kuchangia na niseme tena kwamba ninaunga mkono hoja hii na ninaomba nimshukuru Mama Anne S. Makinda, hapa ananichekesha kidogo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini nasema, nakushukuru sana. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhagama. Nilibadili kidogo pale, nikamwita Mheshimiwa John M. Cheyo kabla ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa kuzingatia tu mpangilio wa Vyama, kwa sababu aliyemaliza alikuwa *CUF*, halafu CCM, ningerudi tena *CUF*. Sasa, nakwenda *UDP*, halafu ndio nimalizie na *CUF*.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia mawazo juu ya sehemu hii nzuri sana ya Utumishi wa Umma na inahitajika katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kabisa, nataka kwanza kujikita katika Ofisi ya Rais. Katika Ofisi ya Rais, amechaguliwa Waziri ambaye anamshauri Rais kwa mambo ya Siasa ambaye ni Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru. Nataka kusema kwamba katika muda wa miezi sita ambayo Mheshimiwa Jakaya Kikwete amekuwa Rais wetu, ni wazi kwamba ameonyesha uwezo mkubwa sana wa kuweza kuiunganisha nchi hii na kuwa na mtazamo wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni la maana sana kwa sababu bila kuwa na msimamo wa kitaifa, basi mambo mengine tunaweza kuyapoteza kwa mambo ambayo tunakaa tunazungumza kila siku na tunagombana kila siku. Nyumba inayogombana kila siku, haiwezi ikajengeka kuwa na miradi yoyote ile ambayo inaweza ikaendeleza. Hivyo, hivyo nchi. Mimi naona hapa Mheshimiwa Rais anahitaji msaada mkubwa sana ili kuhakikisha kwamba hali ya siasa katika nchi yetu inasaidia maendeleo na siyo inarudisha maendeleo nyuma na zaidi kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, upande wa Zanzibar, mimi nina hakika Wazanzibari kama wakiweza kukaa pamoja zaidi, *CUF* na CCM wakaa pamoja, wakaacha ugomvi wao, mimi nina hakika wanaweza wakawafikisha Wazanzibari mbali sana katika maendeleo na nina hakika kwa rasilimali walionazo, hata sisi upande wa Bara tunaweza kwenda Zanzibar kuomba watuongezee kidogo mchango wa maendeleo katika sehemu hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wito wangu ni kwamba, Wizara hii au Waziri huyu angejihusisha zaidi katika kujaribu kutengeneza Mikutano ya wanasiasa ili tuweze tukakaa pamoja tuzungumze ni jinsi gani tutamsaidia Rais anayeonyesha sasa hivi anataka utaifa, anayeonyesha kwamba anataka *inclusivity,* yaani kila mmoja ashirikishwe, tuweze kumsaidia namna gani ili kuhakikisha kwamba siasa itumike kwa ajili ya kuendeleza watu na isitumike kwa ajili ya kurudisha watu nyuma.

Mheshimiwa Spika, lakini, mimi namuunga mkono kabisa Rais wa sasa kwa kazi nzuri anayoifanya na juzi hapa nimekwenda naye Amerika, nimeona jinsi watu wanavyomkubali Rais wetu, Mashirika ya Kimataifa yanavyomkubali na Mataifa makubwa yanavyomkubali. Basi kama hiyo inawezekana, mimi nina hakika akisaidiwa na Waziri huyu, pia anaweza akatengeneza mambo ya umoja zaidi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hapa ningeshauri kwamba Vyama vyote ambavyo viko ndani ya Bunge, tuna *Tanzania Centre For Democracy* ambapo Wakuu wote wa Vyama tunakaa pamoja, mimi ningeshauri Mheshimiwa Waziri angetazama mkondo huu kiwe chanzo cha sisi wote kuweza kuzungumza namna gani tunaweza kumsaidia Rais kujenga utaifa wa nchi yetu. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, upande wa watumishi. Mimi hapo nafikiri tumekosea kwa muda mrefu tangu tumeanza. Labda kwa ushauri wa Wafadhili wetu, kitu ambacho kinaitwa *Manpower Reform* katika nchi yetu, tumepoteza taswira au mtazamo wa mtumishi wa Umma. Zamani na mimi nakumbuka nilipokuwa kijana, mtu alikuwa akiingia Serikalini kuwa mtumishi kwa sababu alikuwa na uhakika kwamba, kwanza atakuwa ni *permanent employee*, atakuwa na kazi ambayo ni ya kudumu, hata kama ni mshahara ni mdogo, lakini ana uhakika kwamba atakuwa na ajira.

Mheshimiwa Spika, la pili, alikuwa anaingia mle akijua kwamba kuwa mtumishi wa Serikali ni *career,* yaani ni utumishi unaodumu tangu labda una miaka 18, kuna watu wengine wameingia kutoka Shule tu na wameendelea wamekuwa Ma-*Commissioner* ndani ya Serikali. Anajua kwamba akishafika hapa, atafundishwa ndani ya Serikali, atapata *promotion* ndani ya Serikali, ataendelea na mpaka mwisho anaweza akastaafu na hali yake ikiwa nzuri. Huu ndio ulikuwa mtazamo wa watu wengi hapo zamani.

Mheshimiwa Spika, lakini, leo hakuna mtu ambaye anaweza sasa hivi akajivunia kuomba kazi ya Serikali. Hana uhakika kama mtumishi wa kudumu, kama ni mtumishi labda wa muda, kama ni mtumishi ambaye leo ataambiwa kazi yako imekwisha au anakuwa ni mtumishi ambaye ni wa *Contract*. Kwa hiyo, ni shaghala baghala tu, mambo yote yameharibika.

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri tungerudi tena kule ambako tulipoteza njia. Kweli tuanze kuwandaa hao vijana wanaoingia *Civil Service* na wanabaki kuwa *Civil Servants* na wanafundishwa maadili ya ki-*Civil Servant*. Leo hii, hujui nani ni mwanasiasa, hujui nani ni *Civil Servant*. Siku moja mimi nilipokuwa napeleka *Form* yangu pale Bariadi nikigombea Ubunge, napeleka ile *Form*, mtu anasema, aha! Unajua na mimi nilikuwa nataka kugombea sijui Jimbo la x, y, z. Nikasema, wewe! Akasema ndiyo! Wewe ni Chama gani? CCM! Sasa wewe ni mtumishi wa Umma au wewe ni mwanasiasa?

Mheshimiwa Spika, hali hii kusema kweli inaleta wasiwasi hata namna ya watumishi hawa wa Umma kuweza kuwa watu ambao watafanya kazi bila upendeleo wa aina yoyote. Kwa hiyo, turudi kule.

Mimi nashauri kwamba, katika sehemu ya Utumishi wa Umma ambayo Wazungu wanasema kwamba ni *Professional*, kwa mfano Watumishi wa Umma - Mapolisi, hii ni taaluma. Kwa hiyo, wako Polisi na wanajua mtu wao ni *IGP* mpaka chini. Watumishi wa Umma - Jeshi, wanajua wana Kamanda wao tangu juu mpaka chini. Leo pia tungekwenda hata kwa Watumishi wa Afya, wajue kwamba *Principal Sectretary* Wizara ya Afya, ndiye *Boss* wao na akiingia kwenye Kituo cha Mafunzo kama Unesi au kama Daktari, mara moja anajua kwamba mimi nakwenda mkondo huu na kwamba *Permanent Secretary* Wizara ya Afya, yule ndiye atakuwa Mwajiri wangu.

Mheshimiwa Spika, ndivyo tulivyokuwa kwenye kilimo, ndivyo tulivyokuwa katika sehemu nyingine, ndivyo ilivyokuwa kwa Ualimu na mambo kama hayo. Leo hii, mtu anamaliza Ualimu, mtu anamaliza Chuo cha Afya, anambiwa kwanza angoje kazi zitangazwe. Sasa, utangaze nini? Halafu ikianza kutangazwa, kwanza uende kwenye usaili, wale waliyekuwa wakinifundisha Afya wenyewe hawakujua kwamba mimi Afya nime-*qualify*! Watu wanaotoa usaili ukiwaangalia, hata ile *profession* hawaijui. Sasa, wewe utaniuliza maswali gani ambayo yule Mwalimu hakuniuliza? Kwa hiyo, mimi naona tumepotea njia.

Tuanze kuwaanda sasa vijana kwa mtindo ambao tuliujua zamani tangu wakati wa Ukoloni. Sasa hivi, tumejikuta mahali ambapo sasa tuna Serikali iliyozeeka. Ukienda kuangalia Wizara zote, ni zaidi ya nusu ya watumishi wa Serikali wako tayari kustaafu leo. Wengine wana miaka 55, wengine 52, wengine 60. Sasa, tutaendesha Serikali ya namna gani ambayo wote ni vikongwe tu, hatujui tunaelekea wapi! Kwa hiyo, mimi nashauri kwamba turudi nyuma, tuajiri watu kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Spika, lakini la tatu ni mishahara. Mishahara ya Watumishi wa Umma pia imekwenda Hawaii, haijulikani ina *direction* gani. Watu wanamaliza pamoja Shule, Chuo Kikuu, mmoja anakwenda *TRA* anapata mshahara kibao, mwingine anaingia Wizara ya Madini, ndio hivyo anamegewa kidogo, mwingine akienda Afya, ndiyo kabisa, haijulikani yuko mshahara wa namna gani! Hali hii inaleta kutokuwa na motisha kuingia katika Serikali.

Mheshimiwa Spika, mimi naona Serikali inapaswa kuwa na sera ambayo iko wazi. Watu wa *grade* fulani, wanalipwa hiki na kila mmoja anajua na pasiwe na kupishana sana. Sasa, hivi hata kwenye redio wanasema hata ukiwa *Sweeper* Bwana, ukiwa *TRA* mambo ni mazuri. Hali hii haiweki motisha ambayo itaweza kusaidia watumishi wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia jambo la mishahara, leo kweli Waziri ametuambia kwamba atapandisha mishahara ya watumishi wa Serikali, lakini ukiangalia kwenye vitabu unashangaa kwamba *Basic Salary Pensionable and Not Pensionable* iko hivi. Lakini, iliyo kubwa ni *employment allowance*. Hii *employment allowance* ni kitu gani? Inavyoonekena ni kwamba kama *employment allowance* ndiyo wanayolipwa watu wanaosafiri, mimi nina hakika hii haimsaidii mtu wa chini, itakuwa inawasaidia *Directors*, itakuwa inawasaidia Ma-*principal Secretaries* na watu kama hao. Lakini pia

inaleta sura mbaya, hata watu wanaotusaidia kila wakiangalia kwenye *Vote* zetu, *employment allowance* inafanana na mshahara wenyewe na zaidi mara nyingine katika sehemu nyingine ni mara mbili ya mishahara ambayo inalipwa.

Mheshimiwa Spika, kama *employment allowance* ndiyo inasaidia watumishi, kwa nini basi tusikubaliane kwamba yote hii ilimbikizwe katika mishahara ya watumishi na kama kwamba isilipiwe kodi, afadhali tuseme hivyo, kwa sababu hakuna sababu leo unasema unalipa kodi, *income tax*, kesho unasafiri unachukua mara tano ya ile fedha ambayo umelipa *income tax*. Sasa ni faida gani kwa Serikali? Ni afadhali kama ni *employment allowance* ndiyo inawasaidia watumishi, basi tuseme *employment allowance* hii, ndiyo mishahara yao na kama kodi ndiyo matatizo, tuseme watumishi wa Serikali wote hawana kodi. Kwa hiyo, tunajua kabisa kwamba utakakopata kodi ni kwa sehemu nyingine na siyo kwa watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini, baya zaidi, ukimwekea mtu *employment allowance* wakati akiwa kwenye ajira, kweli atapatapata kidogo, kwa sababu anasafiri, lakini wakati anapoacha je! *Employment allowance* haiwekwi kwenye mahesabu ya pensheni yake. Kwa hiyo, ndiyo maana tunashangaa wastaafu, akiona mtu anafikia kustaafu anaanza kumbembeleza *President*, anaanza kumbembeleza *Prime Minister*, jamani naomba *Contract* hata ya miaka miwili. Ndiyo hivi sasa mababu wanafanya kazi na wajukuu kwa sababu ya kukaa kubembeleza. Akiangalia kule ndani ni giza, kwa sababu hatuna sera nzuri ya wastaafu. Ningeshauri kwamba jambo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, lakini, mwisho ningependa kutaja kidogo juu ya jambo hili la Utawala Bora. Utawala Bora ndiyo sifa ya nchi yoyote ile. Haki za binadamu ndiyo sifa ya nchi yoyote ile. Mimi naona hii ni *area* ambayo bado hatujaifanyia kazi. Bado tuna utaratibu wa zamani usiofaa ambao kila mmoja ni *Boss*, kila mmoja ana uwezo wa kuweka mtu ndani na ndiyo maana ukiangalia kwenye Magereza yetu, nusu ya watu ambao wako kwenye Magereza ni watu ambao wamewekwa mahabusu. Wamewekwa ndani kwa sababu ya *DC* hampendi, amewekwa ndani kwa sababu *Ward Executive* hampendi, Mtendaji wa Kijiji na mwenyewe ana ruhusa ya kuweka mtu ndani hata ndani ya gereji, hata ndani ya ghala la pamba. Hiyo ndiyo hali iliyopo katika nchi hii. Mimi naona wakati sasa umefika kuangalia upya hata haya mambo ya kuweka mtu ndani tupunguze, ni nani anaweza kumweka mtu ndani. Kwa nini watu wasipelekwe Mahakamani na kule hakimu aamue kama ukae ndani au ukae nje?

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi ya kufanywa katika Idara hii na hivyo naunga mkono fedha zote zilizowekwa mle kama zitasaidia kuboresha Idara ya Utumishi wa Umma pamoja na Ofisi ya Rais. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa sababu ya muda, naomba nitoe shukrani ya jumla tu. Tunawapongeza nyote kwa kazi nzuri mliofanya.

Mheshimiwa Spika, ninataka kwanza niende kwenye ukurasa wa 64 wa Jedwali la kitabu cha hotuba, Jedwali la tisa. Kuna malimbikizo ya mishahara karibu ya bilioni 21 ambayo bado haijalipwa kwa wafanyakazi mbali mbali au watumishi mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, ninataka nipate maelezo tu kwamba sasa hivi tunatumia utaratibu wa *Cash Budget*, kuna sababu gani ya watumishi kukaa muda mrefu hawajalipwa wakati tunatumia *Cash Budget* na pesa zimekuwa zinarundikana miaka miwili, mitatu na hatimaye ndiyo baadae watu wanalipwa? Ni kwa sababu gani wakati tunatumia utaratibu wa *Cash Budget* na wafanyakazi wengi hawajalipwa karibu Shilingi bilioni 21 kwa mujibu wa takwimu alizoleta Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni? Hilo lilikuwa la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, ninataka kuona kama Serikali imefanya tathmini juu ya utekelezaji wa Mpango wa Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi. Katika Jedwali Namba saba, imeonyesha hapa kuna Wizara chache tu ambazo tayari zimeanza utaratibu huu wa ushirikishwaji wa Sekta Binafsi. Sijui kama kuna tathmni iliyofanywa katika hizi sekta ambazo tayari zimeanzisha na *performance* yake ikoje!

Mheshimiwa Spika, halafu la tatu, ninataka vile vile Mheshimiwa Waziri atuelezee juu ya *performance* ya Serikali. Tatizo moja ambalo lipo katika Serikali ni uwezo wa Serikali katika kutekeleza. Ukitaka kupata uthibitisho wa haya, mara nyingi angalia vifungu vya fedha zinazorudi baada ya Wizara kushindwa kutekeleza au inafika karibu ya Juni, ndiyo Wizara zinapewa fedha haraka haraka angalau watu wamalize tu. Kwa hiyo, hakuna hata programu nzuri ya matumizi yenyewe ya fedha. Sasa, pengine *capacity* ya utekelezaji ni tatizo.

Je, Serikali au Wizara imefanya tathmini ya *capacity* ya Serikali katika kutekeleza toka Serikali Kuu mpaka Serikali zetu za Halmashauri ili tuweze kujua hasa hizi pesa zinazopelekwa kweli zinaweza zikakidhi yale mahitaji yanayotakiwa? Kwa sababu wakati mwingine unaweza kupeleka fedha, lakini uwezo wa kutekeleza ukawa mdogo. Kwa hiyo, ikawa fedha siyo tatizo, tatizo ni uwezo wa kutekeleza. Sasa kama hamfanyi tathimini, kila wakati tatizo mtachukulia ni fedha, lakini kumbe tatizo ni uwezo wa kutekeleza. Sasa, hilo nafikiri linakosekana katika taarifa hii na ningependa kupata ufafanuzi wake.

Mheshimiwa Spika, la nne ni suala la wafanyakazi wetu,watumishi wetu, Watanzania walioko nje. Sina hakika kama Serikali ina utaratibu wa kujua hasa ni watumishi wa aina gani na wako wapi na wana fani gani walioko nje ya nchi ili Serikali iweze kutumia hizi taaluma ambazo wamezipata nje kusaidia katika maeneo ambayo tunahitaji kuyatumia. Mimi nafikiri, hilo lingeweza kusaidia, lakini pia lingeweza kuwasaidia Watanzania ambao wako nje wakaweza kuwekewa utaratibu maalum, wakaweza kuleta mapato yao wanayopata kutoka nje na kusamehewa hata kodi kwa vitu wanavyovileta ili vikasaidia katika kuendeleza uchumi wetu. Mimi nafikiri Serikali ingeweza kulifanya hilo likasaidia.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la rushwa. Lakini kabla sijaingia kwenye rushwa, Waziri hapa amesema kuna ajira kama 20,000 zitapatikana, labda tungeelezwa katika hizi 20,000 zinapunguza kwa kiwango gani upungufu uliopo hivi sasa na pengo lililobaki litajazwa kwa muda gani? Nafikiri hilo nalo lingetusaidia, badala ya kusema tu tunaajiri watu 20,000, hatujui, lakini pengo hasa ni kiasi gani? Ukichukua hao 20,000 tumepunguza kiwango kwa kiasi gani na hasa katika zile *area* muhimu kama za elimu, afya na kadhalika nalo nafikiri lingeweza kutusadia tukapata majibu yake.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la rushwa. Kuna taarifa mbali mbali hasa kutoka *Public Accounts Committee* juu ya mambo ya rushwa ambayo bado hayajashughulikiwa kwa muda mrefu sana. Kwa mfano, kuna suala la *TVT*, *Public Accounts Committee,* ilisema kuna *element* ya rushwa hapo na ichunguzwe. Labda sasa ni mwaka wa pili hatujapata taarifa zake. Kuna suala la Wizara ya Elimu, kulikuwa na *Computer* ambazo zililetwa 400 kwenye maboksi ya sabuni, ikaonekana ndani yake kuna rushwa, ikakabidhiwa Kitengo cha Rushwa kuchunguzwa. Taarifa zake mpaka leo hazijatolewa.

Kwa hiyo, kuna matukio mengi ya rushwa ambayo yametolewa taarifa na hatujapata taarifa zake. Labda tungeweza kusaidiwa hasa kama zile ambazo ushauri unatolewa ndani ya Kamati za Bunge, nafikiri ni vizuri kukawa na utaratibu wa Kamati zile za Bunge kupewa taarifa zake, vinginevyo inakuwa ni kazi ya bure tu, kazi ya Kamati inafanywa lakini hakuna taarifa zinazotolewa. Sasa hilo mimi ningependa vile vile nalo likaletwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni hili suala la siasa. Nashukuru Mheshimiwa John M. Cheyo ameligusia.

Mheshimiwa Spika, hili ni Bunge letu la tatu la Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa. Mimi nafikiri umefika wakati sasa tukae ndani ya Bunge hili tuzungumzie masuala ya nchi, masuala ya matatizo ya Taifa letu, ya kiuchumi na kijamii. Tunakuja kila wakati tunazungumza jambo hilo hilo moja la mgogoro, mpasuko na kadhalika. Mimi nafikiri *Comrade* angetusaidia akaja na programu ya kuonyesha hasa kazi zake anazotaka kuzifanya ni zipi na tuzielewe, maana yuko pale Ofisi ya Rais, lakini hatujapata programu hasa ya kazi zake atakazozifanya.

Mheshimiwa Spika, nafikiri ni *high time* tupate programu na hasa vile Rais alivyosema katika hotuba yake kwamba ameunda Wizara hiyo chini yake kwa maana ya kwamba kuwe na mahusiano na maelewano juu ya vyama vya siasa, lakini vile vile katika kustawisha ustawi wetu wa jamii. Sasa, tungepata programu, tukajua hasa kuna programu gani iliyoandaliwa hasa ya kukamilisha haya.

Mheshimiwa Spika, nyingine ni ile kauli ya Rais aliyosema ya kuhusu suala la mpasuko wa Zanzibar na nafikiri *Comrade* atakapokuja, tunaomba atupe maelezo kama kuna hatua zozote zimechukuliwa mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kulisema, ni suala la wafanyakazi kukatwa makato ambayo hayamo katika utaratibu uliowekwa. Labda nitoe mfano, Polisi kwa mfano wanakatwa fedha wakati mwingine za michezo na kadhalika. Je, zimo ndani ya utaratibu wa utumishi wao au hakuna? Ni nani ana mamlaka ya kusema mfanyakazi akatwe fedha zake? Kuna malalamiko mengi sana kutoka kwa vijana wetu wa Polisi na wengineo, wanakatwa fedha zao za mishahara bila ya utaratibu wa kisheria. Nalo hili nafikiri linahitaji kusimamiwa na kuelezwa kwa uwazi kabisa ili watumishi wapunguze malalamiko.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa nitasema kwa ufupi sana, ni suala la matumizi ya rasilimali watu. Mimi nafikiri bado hatujapanga programu nzuri juu ya rasilimali watu. Hivi sasa tukiangalia nchi za jirani na sisi, kuna tofauti kubwa sana ya matumizi ya rasilimali watu. Rais alipokuwa anatuhutubia Bungeni, alisema, Libya wanahitaji sio chini ya Walimu 1000 wa kufundisha Kiswahili. Tungetegemea katika kipindi hiki cha miezi sita sasa, tunaarifiwa vijana wangapi wameshapelekwa Libya kwenda kufundisha Kiswahili. Hiyo ni ajira, tena ajira nzuri tu, maana ina mshahara mzuri na marupurupu mengi. Kwa hiyo, Watanzania wangeweza kupata nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa, nasema kauli kama hizi zinatolewa na Rais, huoni programu, unaona Bajeti ya Utumishi ipo, haisemi watu wangapi wanapelekwa Libya kwenda kufundisha na kadhalika. Sasa, rasilimali watu haijatumika vizuri katika nchi yetu. Mimi nafikiri kuna haja ya kuitumia rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, kuna Maprofesa wana-*retire* katika nchi yetu, mimi nasema kumwandaa mtu mpaka akafikia Uprofesa, ni gharama kubwa sana. Mtu huyo ata-*retire* vipi! Lakini ni kwa sababu hakuna maandalizi mazuri. Kwa mfano kama ni Mtaalam, ni *Scientist*, hakuna *Facility* za kufanya *Research* ya ile Elimu yake aliyonayo. Wako wengi tu, tulikuwa na Profesa Machunda kama sijasahau, alikuwa Ukerewe, maskini aliishia kule, basi na utaalam wake huko huko Ukerewe mpaka akamalizikia kule.

Mheshimiwa Spika, sasa mtu anaandaliwa kama Profesa, anafikia cheo cha Uprofesa, fani yake hawezi kuiendeleza, paka uishe uhai wake! Wakati kila mtu akikomaa ndio anaweza kufanya utafiti zaidi! Mimi nafikiri katika *area* ambayo bado hatuja-*concentrate* ni hii *area* ya Utafiti kwa kuwatumia watu waliopata taaluma kubwa, badala yake wanastaafu, wanakaa majumbani katika umri ambao wanaweza kufanya kazi, lakini hakuna fursa za kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri rasilimali watu bado hatujaitumia vizuri na nafikiri ni eneo ambalo Serikali ingeweza kulisimamia vizuri.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ni la mshahara. Nashukuru Serikali imetangaza kwamba itapandisha mishahara. Lakini nafikiri siyo utaratibu mzuri tunaujenga kwamba kila wakati Serikali ndiyo itangaze siku ya Sherehe ya *May Day* ama mtegeemee Rais kutangaza kwamba mshahara utaongezwa. Nafikiri siyo utaratibu mzuri. Kuwe na utaratibu ambao mfanyakazi anaelewa kabisa mshahara wake utaongezwa katika kipindi fulani kutokana na matokeo fulani. Wengine wanaangalia *inflation*,

wengine wanaagalia mambo mengi ya kiuchumi, halafu wanapandisha mishahara na sio lazima kila mwaka, kila miezi mitatu, miezi sita, inategemea hali ya uchumi ilivyo.

Lakini nasema, huu uataratibu wa kusema kwamba tungoje Rais kwenye sherehe za *May Day* atangaze kiwango cha mshahara, siyo utaratibu mzuri hata kidogo! Tungekuwa na utaratibu ambao utatusaidia kutangaza mishahara, mfanyakazi akijua kabisa mshahara wake ni kiasi gani na lini atapandishwa cheo na lini atapata nyongeza ya mshahara wake.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine, kwa sababu ya utaratibu huo mbovu, ndio leo tunakuja tunaambiwa kwenye Bunge kwamba kuna asilimia 15 na kuna asilimia 50 bila kujua ni kiwango kipi na kipi kitakachopandishwa asilimia 50. Lakini kama alivyosema Mheshimiwa John M. Cheyo hapa, sisi tulifanya *Computation* ya hii *employment allowance*. *Employment allowance* inazidi mishahara. Sasa, Serikali inachoogopa kupandisha mishahara au kutumia *employment allowance* inakwepa kuja kulipa pensheni kwa wafanyakazi, lakini wakati huo huo Serikali haijui kwamba imejiibia kodi kwa sababu mlipa kodi peke yake anayelipa kodi kwa ukamilifu ni mfanyakazi, sio mtu mwingine yeyote, sio mfanyabiashara yeyote. Mfanyakzi ndiye anayelipa kodi.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nafikiri tungeitumia ile *employment allowance* kuongezea mshahara ili lile *group* ambalo lilikuwa linasamehewa kutozwa kodi, sasa litakuwa lote linalipa kodi. Kwa hiyo, Serikali itajipatia mapato mazuri zaidi. Lakini vile vile ukiweka *employment allowance* unamfanya mtu asikae kazini, aombe nafasi ya kwenda kufanya kazi mahali au kwenda safari ili apate fedha zaidi. Kwa hiyo, kwa upande mwingine unapunguza uwezo wa kufanya kazi wa mtu. Kwa hiyo, mimi nafikiri hiki kishawishi cha kufanya safari nyingi na Semina nyingi, kitapungua kama hii *employment allowance* itaondolewa na itakuwa *paged* kwenye mshahara kwa mujibu wa ngazi yake ya kazi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana! *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyoona ukutani saa imekaribia ya kusitisha shughuli za Bunge. Kwa hiyo, haitoshelezi kumpa nafasi mchangiaji yeyote. Nasema tu kwamba Saa 11.00 jioni, ninayo majina matano. Lakini watakaoweza kuzungumza ni wanne tu. Wapo Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, kumbe alikuwa kwenye Mkutano, nilipomwita mwanzo alikuwa katika Mkutano wa Mkoa ambao uliitishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo na Mheshimiwa Magadalena H. Sakaya. Kama wataaongea kwa muda mfupi, basi ile saa moja ya saa 11.00 hadi saa 12.00, inaweza ikawatosha wote watano. Lakini, isipokuwa hivyo, itabidi mmoja akose.

Kwa hiyo, saa 12.00, nitawaita Waheshimiwa Mawaziri ili kujibu hoja. Kwanza, nitamwita Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utawala Bora - Mheshimiwa Philip S. Marmo, kwa dakika 15, saa 12.00, atafuatiwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mambo ya Siasa

na Uhusiano wa Kijamii, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru na mwisho, Mtoa Hoja mwenyewe, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, kwa nusu saa. Kwa hiyo robo saa, robo saa, halafu nusu saa, itatufikisha saa moja kamili, ndiyo tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi. Kwa uzoefu nadhani dakika 45 zitatutosha kwa Kamati hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, kwa kuzingatia kwamba muda hautoshi, basi nasitisha shughuli za Bunge dakika chache kabla ya muda wake, hadi tutakapokutana hapo Saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.57 mchana, Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotangaza awali katika orodha yangu hapo, wapo wachangiaji watano na nafasi kwa kufika ule muda wa saa kumi na mbili imekuwa wa nne tu. Labda tu ikiwa wahusika wengine watakuwa wametoka, naona Mheshimiwa Magdalena Sakaya hayupo, ni mmojawapo wa wazungumzaji. Watano hao ni Mheshimiwa Peter Serukamba ambaye atatangulia, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi na mwisho Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kama muongeaji wa kwanza mchana huu. Kwanza kama walivyoanza wenzangu na mimi nimpongeze mtoa hoja, kwa kweli ameitoa hoja kwa umahiri mkubwa, mimi ya kwangu ni machache sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaanzisha wakala, tunaanzisha wanasema mpaka sasa hizi nadhani tumefika wakala wa Serikali 24. Nia ya kuanzisha wakala nikuongeza ama kuboresha utendaji wa Serikali. Mimi nilitaka tu kutoa angalizo kidogo, bado hizi wakala baada ya kuzianzisha, tusiwafanye wawe kama wao sio *part* ya Serikali, lazima maendeleo yale ya Serikali kuendeleza wafanyakazi ama watumishi wa umma pia nao wale watu ambao wako kwenye wakala wahusishwe maana inaweza ikaja kuna baadhi ya wakala zimeanzishwa, wakifika nao wanatengeneza *scheme of services* ya kwao na kuna zingine zina *contradict* hata ile ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *training program.* Maendeleo yoyote duniani yanaletwa na *human resources development,* kwa hiyo, niiombe Serikali tujizatiti kuhakikisha tunatoa *training program* ambazo zitakuwa ni endelevu ili uboreshaji katika Serikali uwe mkubwa katika utendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka nitoe mawazo yangu, ni suala la kubadilisha sasa, najua itakuja taratibu, lakini ili utendaji uweze kuboreka lazima *mind set* za wafanyakazi wetu nazo zibadilike kulingana na wakati. Bado tunalo tatizo la watendaji wetu, tatizo ni kubwa unaweza ukafika ofisini, ukaandika barua ukajibiwa

baada ya muda mrefu sana. Mimi nadhani hili nalo litapunguza utendaji. Ni vizuri sasa tuanze programu za kuwafanya watu waone kwamba sasa Serikali iwe *cooperate entity* hapo tutakwenda. Lakini kama *style* ni ile ile ya zamani, hata kama tutaleta *appraisal performance* nyingi tuna *set targets* kama bado *mind set* za watu ni zile zile, bado hatuwezi kufika kule tunakotaka kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niombe sasa watu wa utumishi kuhus walimu. Walimu huwezi kujua wako chini ya nani, kuna TAMISEMI, Utumishi, mambo yao ningeomba sasa imefika wakati tuamue sasa walimu wote wako chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Mambo yao yote yafanyike huko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ni rahisi kufuatilia. Waganga na manesi wanataka kuhama lazima aende Utumishi, watoke Utumishi waende TAMISEMI, sijui Wizara ya Afya na ustawi wa Jamii, inapoteza muda. Kwa hiyo, nadhani sasa imefika wakati sasa tujue kwamba waganga wote, manesi wako chini ya Wizara ya Afya na mambo yao yote yawe yanafanyika huko chini ya Wizara ya Afya. Hapa nina hakika utendaji utakuwa ni rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo mimi hili ndio hasa limenifanya niombe nichangie, kabla ya mwaka 1999 kulikuwa kuna wastaafu, wastaafu wetu hali zao ni mbaya sana hasa wale waliostaafu kabla ya mwaka 1999 hao ndio ninaowaongelea. Wale waliostaafu baada ya mwaka 1999 sheria imebadilishwa angalau ni tofauti. Lakini fikiria Katibu Mkuu, aliyestaafu mwaka 1990 na Katibu Mkuu aliyestaafu mwaka 1980 wanakutana kwenda kuchukua pensheni, huyu anachukua shilingi 20,000 huyu anachukua shilingi 400,000 katika nchi hii hii na hao waliostaafu kabla ya mwaka 1999 hakika hawa ndio walijenga hii nchi, hawa ndio wameanza toka wakati tunapata Uhuru, wamehangaika na nchi hii, wameifikisha hapa ilipo. Lakini leo ukiwakuta, *in fact* una-*accelerate their death,* mtu amemaliza ni Balozi, amefanya kazi Ubalozini, anakuja leo *imagine that status of life* aliyokuwa anaishi, lakini kwa sababu hatukuandaa mambo yetu vizuri, leo ukimkuta huwezi kuambiwa huyu Balozi mstaafu katika nchi hii, tena hawa ndio waliofanya kazi kwa uhadilifu mkubwa kwenye nchi hii.*(Makofi)*

Naomba sana tuangalie namna ya kuwasaidia wastaafu hawa kabla ya mwaka 1999. Tusipoliangalia kwa sababu tulibadilisha sheria mwaka 1999 leo tukadhani mambo ni mazuri kwa kuangalia wale wa baadaye. Lakini tuwaangalie wa nyuma na sio wengi, kama *issue* ni bajeti, sio wengi, kwanza wengi wanakufa, kwa hiyo, bado bajeti inazidi kupungua haraka. Wale ambao bado wako hai fikiria mtu aliyekuwa *IGP* wa nchi hii, leo anakwenda dirishani kuchukua shilingi 20,000, tunawapa *lesson* gani wale wanaokuja baadaye? Kwa hiyo, mimi naomba kabisa tuandae utaratibu, watu hawa ambao walistaafu kabla ya pale narudia hawa ndio walioijenga hii nchi.

Mheshimiwa Spika, tafadhalini sana tutafute utaratibu wa kuwawekea angalau nao hali ya maisha ipande na hawa ninaowaongelea ni Mabalozi waliokuwa ni Makatibu Wakuu, Wakurugenzi Wakuu fikiria sasa wale waliostaafu ambao walikuwa ni walimu wa kada za chini wanalipwa shilingi ngapi. Lakini pia tusisahau kuna *issue* ya *inflation rate* huwezi kuniambia shilingi 20,000 ya mwaka 1999 bado ina maana mpaka leo.

Kwa hiyo, niombe tuyaangalie haya mambo kwa kina sana na watu wenyewe kama suala ni *finances* siyo wengi na wanapungua kwa haraka sana. Kwa hiyo, niombe kabisa Serikali na ningependa Waziri wakati anatoa majawabu anipe jawabu litakalo niridhisha jinsi ya kuwashughulikia hao wastaafu wa kabla ya mwaka 1999. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa kweli hili mimi ndio lilikuwa linanipa taabu, niombe sasa niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. *(Makofi)*

Kwanza kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa na kuzungumza katika kuchangia kwa mdomo huwa nachangia kwa maandishi, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa nchi hii ili kutuongoza sisi Watanzania. Nina imani kubwa kwa mwanzo alioanza nao bila shaka atakuwa mwadilifu na Mungu atamsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nikupongeze wewe mwenyewe binafsi pamoja na Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kwenu kutuongoza katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano. Lakini pia nikishukuru Chama changu kwa kunipa nafasi hii, nami leo nikawa Mbunge kuja hapa katika Bunge hili na nikawajibika kama Wabunge wenzangu. Pia niwapongeze Wabunge wenzangu wale waliochaguliwa na kuteuliwa na wale ambao wamejaaliwa kupata nafasi za Uwaziri, Mungu awasaidie watekeleze majukumu yao ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia hoja hii nianze na masikitiko. Lakini kwanza naomba nianze kwa kunukuu ile *definition* kidogo tu kwamba *management* ya utumishi ni kuimarisha utawala bora. Nakubaliana kwamba ni kuimarisha utawala bora. Utawala bora ni pamoja na kuheshimu haki za binadamu, ni pamoja na kuheshimu sheria na mambo mengine ambayo sitaki niyataje yote kwa sababu yatanipotezea muda.

Mheshimiwa Spika, tukiwepo katika vikao vya aina zote si hapa Bungeni, siyo kwenye semina, si kwenye vikao vya aina yoyote huwa tunajaribu sana kuelimishana suala la utawala bora. Inasikitisha sana tunahubiri utawala bora ndani ya vitabu na ndani ya semina, lakini mara nyingi huwa tunakiuka kutekeleza hayo mambo yanayohusiana na utawala bora. Kuna mmoja hapa asubuhi alichangia akasema kwamba mwisho wa uchaguzi ndio mwanzo wa uchaguzi. Hofu yangu tayari sasa hivi tunajiandaa na uchaguzi, ni kweli kila chama, kila ngazi imo tayari kujiandaa kwa sababu tumemaliza uchaguzi, tunajitayarisha na uchaguzi unaofuata. Vitendo ambavyo vinafanyika wakati mwingi huwa vinakiuka hizo sheria na utawala bora.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi ni chombo muhimu sana kwa nchi zote au niseme kwa Watanzania ndio mlinzi wa raia. Lakini inasikitisha namna chombo hiki tunajaribu kukitumia vibaya hasa wakati wa uchaguzi. Sijui ni kwa bahati mbaya au wanaandaliwa makusudi au ni kutokana na kwamba hawaelewi wajibu wao. Mara nyingi

ninapokuwa nauliza masuala kwa Wizara ya Ulinzi huwa nang'ang'ania sana kumwambia Mheshimiwa Waziri, kwamba atoe semina, atoe taaluma za ziada ili kuwakumbusha wajibu wao na majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchaguzi chombo hiki nguvu zao zote mara nyingi huwa zinaelekezwa kule Visiwani hasa kule kwetu Pemba. Kule inaonekana kwamba ndio kunakofanyiwa majaribio ya kila anayejua kulenga shabaha au kutumia silaha huelekea kule kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi ni Watanzania, Serikali ya Jamhuri ya Muungano ni Serikali yetu, yote ni mama, Serikali ya Zanzibar nasema ni mtoto, baba yetu ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Chombo hiki kinalelewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na ndio maana nikasema ndio baba. Kwa hiyo, chombo hiki kinapoelekezwa kule nguvu zote zikaelekezwa kule wakati wa uchaguzi huwa kuna nini? Nguvu za ziada zinaelekezwa kule huwa kuna nini? Hata magari ya maji, silaha, mabomu huwa tunaelekezewa sisi kule, kuna nini? Hakuna tatizo ni uchaguzi na uchaguzi unafanyika nchi nzima kwani askari si wako kule.

Mheshimiwa Spika, mimi nazungumza na Mheshimiwa Waziri, nazungumza na Spika, sasa kuna mtu ananijibu kwamba kuna tatizo, kazi kwake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, endelea tu Spika anakulinda, una uhuru kamili wa kusema. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa maana hiyo mimi leo ndio nasimama hapa kulia na uongozi kwa sababu sote tuliopo hapa kuna Serikali tunaiangalia hapa. Kwa hiyo, sisi kama tunahubiri utawala bora, tunahubiri uhusiano, tunahubiri siasa, lakini utekelezaji wetu hauji katika suala la utawala bora. Naomba sana Wizara hii ni Wizara nyeti sana, chombo hiki ni muhimu sana, ndio mlinzi wa raia, badala ya kujenga mahusiano mazuri basi tutakuwa tunajenga chuki na fitina baina yetu. Naiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano, iache iliyonayo, iangalie upya suala la utawala bora, iangalie upya suala la demokrasia tunahubiri demokrasia lakini ukifika wakati wa uchaguzi hatutekelezi kwa sababu hatuiheshimu demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwa tunaitana vikao mara nyingi sana, makamanda wa polisi, tunaitana vikao, mimi nakwenda kwenye vikao, tunapanga mikakati mizuri twende hivi, tuelekee hivi, ghafla hugeuka watu wakaelekea mlengo mwingine wakati hawajui wanachokifanya au wanakijua wanafanya *purposely*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kufika popote katika hali hii. Sioni sababu ya nguvu kubwa kuelekezwa kwenye wananchi ambao hawatimii hata laki tatu kule Pemba, nguvu za askari zikaelekezwa kule, mabomu yakipigwa ya moshi, magari ya maji yakamwagwa, risasi zikalia, eti kuna uchaguzi. Jamani huku Bara wenzetu hakuna uchaguzi? Kwa nini tunakwenda hivi Jamhuri ya Muungano ndiyo baba, lazima iangalie watoto katika hali ya usawa, iwalee watoto wake wote katika hali ya usawa kama tunahubiri kweli utawala bora basi tusihubiri, tuutekeleze utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule kwetu Wakuu wa Mikoa, huwa wanateuliwa na Rais wa Zanzibar na Wakuu wa Wilaya na hapa wanateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano. Nasikitika sana wenzetu hapa Wabunge wenzangu naona uchungu kwamba wanashirikiana na Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanafanyakazi kwa pamoja kuleta maendeleo ya wananchi, kule kwetu ni kinyume, ni tofauti kabisa. Hawataki kuwashirikisha hata vijana wetu katika masuala madogo madogo yaani katika miradi midogo midogo inayofadhiliwa na wafadhili. Hata ile miradi basi kama itapitia kwa Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya basi watakaopata hizo nafasi katika ajira ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naambiwa siyo kweli, nataka nitoe ushahidi mdogo. Hivi ninavyokuambia kuna mradi wa dawa huko Pemba wa Malaria basi uajiri wa nafasi hizo umetolewa kwa ubaguzi. Kama mimi naitwa muongo sawa, lakini mimi nasema umetolewa kwa ubaguzi. Nisingeweze kusema hapa, bila shaka nina ushahidi nimeshaona, nimeshafanyakazi sana katika hizo ngazi, hata ukitamka huko ni kazi bure nina shahidi tosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba kama kweli tuna nia ya kujenga Tanzania moja, tuna nia ya kuleta utawala bora katika Tanzania hii kwa maslahi ya Watanzania wote, namuomba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama alivyoona hali halisi ya mambo yanavyokwenda kule Zanzibar, basi namwomba atilie mkazo kwa hali ya juu kuhakiksha kwamba mambo yanakwenda sawa kwa nia ya kuijenga Tanzania iliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine naomba nizungumzie suala la watumishi. Kima cha chini cha mshahara kinasemekana kuongezwa, hakijaongezwa. Tuiangalie hali halisi ya matumizi katika nchi yetu, tuiangalie hali halisi ya umaskini wa wananchi wetu, halafu tuangalie mshahara ambao tumemwekea Mtanzania. *Maximum* ya matumizi ya mwananchi wa kawaida kwa mshahara ambao tumempangia 120,000 ni shilingi 4,000 hata mlo mmoja hautoshi. Labda awe yeye na mke wake tu, lakini akiwa na watoto watatu au wanne basi atakuwa analala na njaa huyu. Naomba Wizara iliangalie tena kwa kina suala hili namwomba Mheshimiwa Rais, kila tunakokwenda basi mwaka ujao tuwatupie jicho la huruma wananchi wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali yetu ni mbaya sana, tujiangalie sisi viongozi ambao *at least* tunapata mshahara kidogo ukifika hapo nje huna shilingi. Tumwangilie mwananchi wa kawaida yuko katika hali gani.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda hautoshi nami ni mwana genzi nitachangia katika Wizara zinazokuja, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipata nafasi hii ya kuchangia hoja ya Ofisi ya Rais. *(Makofi)*

Kabla sijatoa mchango wangu awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kutoa pole kwa familia ya Marehemu Profesa Chachage na jumuiya nzima ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kumpoteza mtumishi wao mahiri, aliyetetea haki za wananchi wa Tanzania na nje ya nchi. Nimetoa salaam hizo za rambirambi kwa sababu Profesa Chachage, alikuwa mwalimu wangu lakini pia tulikuwa naye katika makongamano mbalimbali na pia alikuwa mwanajumuia mwenzangu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, baada ya salaam hizo pia naomba sasa nitoe pongezi nyingi sana kwa mtoa hoja ambaye ni mwanamke na ameonyesha kwa kweli wanawake tunaweza. Pongezi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitoe pongezi kwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa hotuba yake nzuri aliyotoa asubuhi hii. Nitachangia kwenye sehemu mbili kuu kwa sababu ninavyojua Ofisi ya Rais, imegawanyika katika sehemu tatu, lakini nitachangia zaidi kwenye sehemu ya utumishi lakini nitaanza na sehemu ya siasa na uhusiano wa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ofisi hii inatimiza miezi sita sasa. Lakini toka imeanza sijaona Waziri mhusika, namheshimu sana Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, kufanya mikutano na viongozi wa vyama vya upinzani, ili kujenga mahusiano ya kisiasa hapa nchini. Kwa hiyo, ni matazamio yangu kwamba wakati Mheshimiwa Waziri anafanya majumuisho atatueleza basi ni jinsi gani au ni mikakati gani anayo ya kuweza kukutana na viongozi wa upinzani ili waweze kujenga hayo mahusiano ambayo Wizara hiyo imeundwa ili iweze kufanikisha mahusiano mema ya kisiasa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongelea hilo sasa niende kwenye suala zima la utumishi. Katika suala la utumishi inaonyesha kwamba mazingira ya watumishi wa umma kwa kweli ni mabovu sana. Hii imeonyesha hasa wakati ambapo tunaona watumishi wengi wanasomeshwa na Serikali kwa gharama kubwa sana, lakini watumishi hawa wamekuwa nchi za nje. Pia tumeona kwamba katika mazingira hayo hayo mabovu, watumishi hao hawaeleweki wako wapi lakini. Pia Wizara husika naomba itueleze ni jinsi gani wanaweza kuwasaidia wale watu wengi ambao wamesomeshwa na nchi hii kwa kodi kubwa za wakulima na wafanyakazi, ni vipi watashindwa ku-*retain* wanakwenda nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, tuna ushahidi tosha kwamba Madaktari wengi, Maprofesa wengi wako nje na hivyo hata Waheshimiwa Wabunge, viongozi wanapougua kupelekwa nje unakuta wanatibiwa na Watanzania. Kwa hiyo, nilikuwa natoa changamoto kwa Wizara husika iweze kufanya mikakati maalum ya kuweza kuwa-*retain* hawa watumishi ambao kwa kweli tumewasomesha kwa kodi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nielekee kwenye suala la walimu, walimu ni nguzo kuu ya maendeleo ya nchi yetu. Hakuna mmoja wetu ambaye amefika hapa bila kuwa amefundishwa na walimu. Lakini utaona kwamba walimu hasa wa shule za msingi wako

katika mazingira mabovu sana. Mishahara yao ni midogo, lakini zaidi ya hapo ni kwamba walimu hawa hawaruhusiwi kwenda shuleni wakati wa vipindi.

Kwa mfano, utaona shule za sekondari na vyuo vya elimu ya juu walimu huwa wanakwenda wakati wa vipindi. Lakini walimu wa shule za msingi wanapaswa kwenda shuleni toka asubuhi mpaka jioni. Lakini hapo hapo walimu hao wamezuiwa kabisa kufanya *tution* na *tution* ndiyo ingeweza kuongeza pato lao.

Sasa tunajiuliza kama kweli tunataka kuboresha maisha ya wananchi wa Watanzania kama ambavyo Ilani ya CCM inasema, ni kwa nini walimu hao basi wasipewe muda wa kwenda kwenye vipindi vyao wakati wa vipindi tu ili ule muda mwingine waweze kufanya shughuli zao za maendeleo kama ambavyo wanafanya walimu wa sekondari na vyuo vya elimu ya juu? Kwa nini walimu wa shule za msingi wanapangiwa taratibu tofauti na zile za walimu wa sekondari na walimu wa vyuo vya elimu ya juu, wakati mwajiri ni huyo huyo mmoja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie suala zima la mishahara. Ni kweli tumeshukuru kwamba Waziri amesema mishahara imeongezwa. Lakini ukiangalia kima cha chini cha mshahara kwa kweli hakitoshelezi kabisa mahitaji ya mtu kwa mwezi mmoja kama ambavyo ilivyo. Kwa hiyo, tulikuwa tunafikiri, kwanza kuna kodi nyingi sana wanazokatwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi binafsi nafikiri ni haki kabisa ya wafanyakazi hawa pamoja na kwamba kima cha chini kiongezwe na kufika laki mbili na nusu au laki tatu ambayo inaweza ikawasaidia kustahimili maisha yao ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende kwenye suala zima la utawala bora. Suala la utawala bora na haki za binadamu ndio kitu pekee ambacho kinaletea sifa nchi yoyote. Nchi ya Tanzania katika dunia imeonekana kwamba kweli inaheshimu haki za binadamu na ina utawala bora. Lakini hii inaonekana kwa nje, lakini kwa kweli tukiangalia kwa ndani haki za binadamu zimekuwa zikipuuzwa sana na tuna ushahidi siku hizi kila unapofungua redio ukisoma magazeti unasikia wanawake wamebakwa, wanawake wameuwawa na mambo mengi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano wale wanaoonekana na macho mekundu kule Shinyanga na Mikoa Kanda ya Ziwa huwa wanauwawa. Sasa kama kweli tunatetea haki za binadamu na tunaonekana sisi ni nchi yenye haki za binadamu, tulikuwa tunaomba basi Wizara husika pale yanapotokea mauaji watu wanaohusika wawabijike kama polisi. Siyo hilo tu kumezuka mtindo wa makundi ya vijana au watu kujichukulia sheria mkononi kwa kuua wale vibaka wanaoiba na saa nyingine unakuta hata mtu hajaiba ilimradi tu alikuwa kwenye eneo lile.

Sasa nakumbuka kuna siku kulikuwa kuna swali na tukajibiwa kwamba hiyo inatokana na wananchi kukosa imani. Sasa inapofika kwamba wananchi wanakosa imani na Jeshi la Polisi, hii inatia mashaka. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba ifike wakati Wizara husika basi ihakikishe kwamba haki za binadamu zinaheshimiwa, zinalindwa na hivyo tunaenzi utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitajielekeza zaidi kwenye masuala ya siasa. Pamoja na kwamba yameshaongewa, lakini mimi nilikuwa naomba nichangie kwa kiasi kidogo. Tumetoka kwenye uchaguzi na katika chaguzi hizo yamejitokeza mambo mengi ambayo kwa kweli yameonekana na kila mtu hapa anajua kwa mfano, vyama vya upinzani mara nyingi sana walikuwa wakinyimwa haki zao wakiwa na mikutano wanaburuzwa hata kama wakiomba kibali basi hawapewi ilimradi kuwanyima haki zao za kisiasa. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwa sababu ni Wizara zilizowasilisha hotuba zao leo zinahusika, nilikuwa nawaomba sana wahakikishe kwamba haki inatendeka, sisi ni wananchi wa Tanzania, ni wawakilishi wa wananchi wametuchagua kama walivyochaguliwa wa Chama cha Mapinduzi kwa hiyo, nilikuwa naomba haki kwa kweli itendeke, polisi kazi yao ni kulinda amani, lakini pale ambapo polisi ndo wana-*cause* kuvunjika kwa amani sisi tunaona kwamba polisi hapo hawajawabika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nielekee kwenye masuala mazima ya wastaafu. Pamoja na kwamba imeongelewa lakini nilikuwa nafikiri kwamba sasa hivi tunaona marekebisho mengi kwenye mishahara na kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba zile *pension* za wazee wastaafu inabidi ziongezwe pale inapowezekana kwa sababu maisha yamepanda sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara husika walichukulie jambo hili, waone ni jinsi gani basi wanaweza wakawaongezea walau hela kidogo wale wazee kwa sababu kama mmoja alivyosema wazee hawa kwa kweli ndio wametufanya tuwe hapa, ndio wazazi wetu. Lakini inasikitisha kuona wastaafu hawa wanavyodhalilika hasa wanapokwenda kufuata fedha zao, mtu anaondoka mpaka Dar es Salaam lakini anapewa labda *cheque* ya shilingi 50 au shilingi 100. Kwa hiyo, nilikuwa naomba suala hili liangaliwe kwa kina ili wale wazee waweze na wao kufaidi kazi zao walizozifanya katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee sasa suala la walemavu. Kila ninaposimama ninaongelea suala la walemavu kwa sababu walemavu nimeishi nao na nimekuwa mlezi wao. Inasikitisha sana kuona kwamba walemavu kimsingi hata ukifanya utafiti ulemavu na umaskini ni kama watoto mapacha. Kwa hiyo,walemavu wengi wanatoka kwenye familia maskini. Kwa hiyo, walemavu hawa wanakuwa wamesoma hata wale ambao hawajasoma tuchukulie wale waliosoma Vyuo Vikuu. Wamefika Chuo Kikuu wanamaliza lakini ajira inakuwa ni ya matatizo sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara husika iwape kipaumbele walemavu hasa wale wanaomaliza, wanaohitimu kwenye vyuo vya elimu ya juu wapate kazi au ajira bila masharti yoyote, wasiwe na *competition* na wale wengine wazima kwa sababu wao ule ulemavu wao tu unatosha wao kupewa ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna ajira za kila aina, kuna walemavu na kwamba tunajua kwa historia tuliyonayo ya Chuo Kikuu kuanzia mwaka 1972 mpaka leo hakuna mwanafunzi mlemavu ameingia Chuo Kikuu akawa *discontinued* kwa sababu ya kushindwa masomo. Kwa hiyo, hii peke yake inaonyesha walemavu wana uwezo sana kiakili. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani walemavu hao basi wanapomaliza vyuo vikuu tunaomba wapatiwe ajira na wasishindanishwe na watu wazima kwa sababu wao wana soko kubwa zaidi kuliko wale walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niongelee suala la kukaimu kwenye sehemu nyingi za kazi, hicho ni cha kwanza. Suala la kukaimu limeleta matatizo na hili haliko tu kwenye watumishi wa umma, lakini pia kwenye mashirika ya umma. Mimi nina mfano ambapo kuna mtu amekaimu nafasi kwa zaidi ya miaka kumi. Kwa hiyo, kama mtu anakaimu kwa kweli kama inavyoeleweka ni kwamba anakuwa hana *authority,* hana mamlaka ya kutoa maamuzi ya uhakika. Kwa hiyo, mara nyingi mtu yule anakuwa anafanya kazi kwa wasi wasi. Sasa mimi sielewi ni kwa nini mtu akaimu kwa kipindi kirefu namna hiyo halafu baadaye wanakuja kumpa mtu mwingine na wala wasimpe yule yule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nategemea kwamba Ofisi husika itasaidia suala hili ili walau kama mtu anakaimu labda ni kwa miezi au imezidi sana ni mwaka mmoja. Lakini kumfanya mtu akaimu kwa kipindi cha zaidi ya miaka kumi, hii kwa kweli haileti *efficience* katika kazi. Kwa hiyo, naomba Wizara ilishughulikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nilikuwa naomba kuongelea matatizo ya kukosa ulinganisho katika suala zima la mishahara. Utaona kwamba wanafunzi kwa mfano wanamaliza pamoja Chuo Kikuu, wanaajiriwa katika sekta mbalimbali, lakini cha ajabu wengine utakuta wanapata shilingi laki tano, mwingine laki moja na ishirini na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, imeleta hatari kubwa kwa sababu sasa hivi wanafunzi wengi wanaomaliza *Form Six* wameshajua sasa hivi kwamba wasome masomo ya *IT* au masomo ya *Accountancy* ndiyo utapata kazi. Kwa hiyo, unakuta kuna wingu kubwa la watu wanaoenda kwenye masomo hayo halafu yale mengine yanabaki hayana wanafunzi. Kwa sababu wanajua wakimaliza watapata mishahara mikubwa. Wataenda *TRA*.

Kwa hiyo, utakuta wale wa Sayansi au wa *Education* kunakuwa hakuna kabisa *competation* kwa hiyo, nilikuwa naomba kujua ni vigezo gani vinavyotumika kupatiwa watumishi mishahara tofauti wakati wanafanya kazi pamoja na kwamba kazi ni tofauti. Lakini wana elimu sawa, wana viwango sawa vya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba hilo pia nipatiwe ufafanuzi. La mwisho kabisa ambalo ningetaka kulichangia ni kuhusu maadili mabovu ya watumishi wa umma. Suala hili nadhani limezungumziwa lakini tunayaona. Maadili ya watumishi sasa hivi yamekuwa ni mabovu sana. Lakini nadhani hii inachangiwa sana labda mishahara midogo au kutokuwa na *motivation* ya aina yoyote kwa wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mishahara midogo sidhani kama hiyo inakuwa ni sababu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba pia Wizara iangalie ni kwa nini watumishi wamekuwa na maadili mabovu tofauti na siku za nyuma, wakati hata siku za nyuma mishahara ilikuwa ni midogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, na mimi niweze kuchangia katika hii Wizara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Pasipokupoteza muda na mimi naomba kwanza niunge hoja asilimia mia moja hotuba ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga hoja mkono naomba nizungumzie katika maeneo machache na kusema kweli suala la Menejimenti ya Utumishi kwa maana ya utumishi wenyewe ni suala ambalo ni la msingi sana na umuhimu wake unafahamika na nadhani ndiyo maana hata Wizara hii ipo katika Ofisi ya Rais na hii yote ni kwa sababu ya kujitahidi kuipa umuhimu na kwa kweli ni Wizara ambayo inaunganisha Wizara zote za nchi hii. Kwa hiyo basi, tuna kila sababu ya kuendelea kuiangalia na kuhakikisha kwamba inafanya kazi zake katika utaratibu ambao ni mzuri. Kusema kweli kama hii Wizara ya Utumishi kwa maana watumishi wakifanya kazi zao katika utaratibu ambao ni mzuri matokeo yake hapo ndipo tunaweza kuboresha uchumi lakini na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo basi, tuna kila aina ya sababu ya kuhakikisha kwamba watumishi wetu wanaendelea vizuri na wanawezeshwa na wanafanya kazi zao vizuri. Lakini basi kwa upande wangu mimi ningewafananisha watumishi wa Tanzania aidha, niwafananishe na mashamba yetu haya ya wakulima wa kawaida wa kienyeji wa Tanzania. Kwa maana unakuta mtu analima heka tano au eka moja badala ya kuvuna mahindi magunia ya kutosha lakini anajikuta amevuna gunia tano. Sasa unajiuliza ni kwa nini? Kumbe jinsi wanavyopaswa kutunzwa au kuangaliwa na kuendeshwa ni sawa sawa na yule mkulima ambaye anaamua kulima kisasa. Leo mkulima akianza kulima kisasa, lile shamba lake atalilima vizuri, atatia mbolea, kama mahindi, atalima kwa mistari, tena ataacha *space* na yale mazao yakishakua ataendelea kuweka mbolea na hatimaye ataweka maji, ataendelea kumwagilia na matokeo yake sasa unajikuta badala ya kuvuna gunia tano, ataenda atavuna gunia 70 kwa hekta. Kumbe basi, nadhani hili katika mtazamo wangu ndilo tatizo ambalo tunalo katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana siku zote tunasema nchi yetu ni nchi nzuri, ina kila kitu, kwa maana ya mipango yake ni mizuri. Lakini unapokuja katika utekelezaji kwa kweli mambo mengi tunaona hayaendi na kwa kuwa hayaendi sasa tumekuwa tunajiuliza na tena hata wakati mwingine tunatafuta mchawi wetu kwamba hivi tatizo letu ni nini?

Mheshimiwa Spika, kumbe basi ni vizuri sasa tuangalie hii Idara ya Utumishi iangaliwe sawa sawa na mtu kwamba hebu basi tuangalie kwenye upande wa Serikali, kuna mambo ambayo inahitaji kuyafanya lakini hali kadhalika na kwa upande wa wananchi wenyewe kwa maana wale watumishi yako mambo ambayo wanahitaji kuyafanya. Leo ukiangalia katika nafasi mbalimbali za utumishi katika Idara mbalimbali nafasi nyingi ziko wazi. Idara ipo pale, leo mathalani unapokwenda kwenye Halmashauri, ukienda Halmashauri siku zote tunapiga kelele tunasema Halmashauri hazi-*perform* Halmashauri hazifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini leo ukiangalia ukienda Idara ya Uhasibu, kuna Mhasibu mmoja, wengine wote nafasi zote ziko wazi. Lakini wakati huo huo tunasema Hesabu za Serikali za Mitaa si nzuri. Kwa hiyo, unakuta haya yote bado ni mapungufu. Leo unapozungumza labda habari ya Mahakama, ukienda kule Mahakamani, Mahakimu hawapo. Kwa maana wapo wachache, Majaji hawapo kwa maana wapo wachache. Bado tunasema tunataka Mahakama ifanye kazi kwa ufanisi, ni mambo mawili ambayo hayawezi kuwezekana kabisa.

Mheshimiwa Spika, hata unapokwenda kule Hospitali. Hospitali nyingine unakuta ina *specialist* mmoja, unakuta hiyo ni hospitali ya Mkoa. Kumbe sasa basi katika utaratibu huo matokeo yake ni kwamba mambo tunakuta hayaendi na kwa kuwa hayaendi sasa, tunasema watumishi wa Tanzania hawafanyi kazi vizuri, kumbe hapo pote inategemeana na nafasi nyingi ambazo zipo wazi lakini hizo nafasi hazijazwi. Kwa hiyo basi ni vizuri hii Idara ya Utumishi hebu ingejaribu kuhakikisha kwamba kama kuna nafasi ambazo ziko wazi basi wajitahidi kuhakikisha kwamba nafasi hizo zinajazwa hasa tunapozungumzia kule katika zile Halmashauri zetu. Halmashauri zetu nyingi ule utaratibu wa kuomba kibali mpaka kije kipatikane wakati mwingine ni utaratibu unaochukua mlolongo mrefu. Kwa hiyo, utakuta nafasi inakaa bure, inakaa wazi kwa muda mrefu na matokeo yake sasa utendaji kazi unakuwa si nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, lakini hapo hapo tunapozungumza kwamba tuendelee kulima hilo shamba letu kisasa ni pamoja na kuangalia maslahi ya watumishi au watumishi walipwe vizuri. Kusema kweli kipato wanachokipata watumishi wetu ni kidogo sana. Hata sisi tunafahamu kwamba wanalipwa fedha ambazo hata haziwatoshi ku-*sustain* maisha yao. Kwa hiyo, matokeo yake mtumishi anaenda kazini tayari ana *frustration* maana wakati mwingine anakwenda lakini hana uhakika kwamba jioni atakula nini wala ataishije. Kwa hiyo, hili suala la maslahi ya watumishi wakati mwingine linahitaji tuliangalie katika ngazi zote kuanzia ngazi ya chini hadi ngazi ya juu kwa maana kila watu waweze kupata haki zao kwa mujibu wa utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata katika utaratibu wa upandaji wa vyeo. Nadhani mmesikia wenzangu wamezungumza kuna watu wanakaa mahala kwenye cheo cha aina fulani zaidi ya miaka kumi, ana sifa ya kupanda lakini bado hawezi kupanda. Kwa hiyo, hali hiyo matokeo yake ndiyo maana Watanzania wengi wanakatishwa tamaa. Lakini si suala la kukatishwa tamaa tu, wengine wanaamua hata kuhama nchi, anaenda nje ya nchi. Tena Watanzania wengi tunajua kwamba wanafanya kazi katika nchi zingine. Hebu tujaribu kuwawezesha badala ya wao wahame kutafuta kazi katika maeneo mengine, basi waje waendelee kufanya kazi katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile hata baadhi ya watumishi wetu kuna wengine wamekaa mahali wanafanya kazi zaidi ya miaka 20 wala hawezi kuhama. Sasa kama mtumishi anafanya kazi kwa miaka 20 na mwisho anaonekana naye ameshakuwa ni sehemu ya familia kwa maana ni sehemu ya wale wanajamii. Kwa hiyo, hata wakati mwingine anapotaka atekeleze majukumu yake kwa mujibu wa sheria na utaratibu basi vile vile inampa taabu sana.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri haya maeneo yote tukajaribu kuiangalia na tuone namna ya kuyaboresha. Nizungumzie na kipengele kingine cha Utawala Bora. Katika hili suala la Utawala Bora kwa kweli kwa watumishi wetu wengi hasa hao wenye nafasi za juu nalo lenyewe ni eneo lenye matatizo sana. Lina matatizo sana kwa sababu wanashindwa wakati mwingine kukaa na Idara zao, wanashindwa kukaa na watu wao wa chini. Mimi kadri nijuavyo ni kwamba hata kwenye familia, hata kama hali ya uchumi si nzuri, lakini basi mzazi au baba wa familia lazima ukae na familia yako. Maana kama mshahara kidogo sisi tuna *principle* moja tu, maadam napokea shilingi 70,000/= kwa mwezi, hiyo hiyo shilingi 70,000 napokea nampelekea mama. Lakini inapofikia mwisho wa mwezi nampelekea mama. Pale ugomvi hautakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ugomvi hautakuwepo kwa sababu ile shilingi 70,000 ndiyo fedha yote iliyopatikana. Kwa hiyo, ataendelea kuibajeti ataendelea kuhakikisha kwamba basi anai-*balance* vizuri. Lakini pale ambapo unakuta baba mwingine, mama hajui baba anapokea mshahara kiasi gani. Lakini sasa inawezekana fedha anapata nyingi, kwa hiyo, tunapozungumza suala la Utawala Bora hiyo ndiyo maana yake kwamba hebu tukae na wale watendaji wetu wa chini basi wafahamu hali halisi kama hatuna fedha basi ni vizuri na wao wakafahamu kwamba kwa kweli hali halisi ndivyo ilivyo. Lakini vile vile tujitahidi ku-*share* nao haya matatizo, maana tuki-*share* nao matatizo basi nayo itaendelea kuwapa moyo na matokeo yake sasa ufanisi utaendelea kuwepo katika utumishi na kwa kweli watu wetu watafanya kazi vizuri na hatimaye mambo yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ambalo ningependa na mimi kulizungumzia ambalo kwa kweli nalo ni suala muhimu sana. Ni hili suala la pensheni kama walivyozungumza wenzangu, kwamba ile pensheni kwanza ni ndogo sana shilingi 20,000/= kwa wale watumishi wa zamani kwa mwezi. Lakini siyo shilingi 20,000/= tu mpaka asubiri baada ya miezi sita sasa baada ya miezi sita, kama wale wa vijijini ile safari tu ya kwenda kuchukua ile shilingi 120,000/= kila baada ya miezi sita nauli tu ya kwenda na kurudi tayari zile fedha zimeishia huko. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nadhani hiyo nayo Serikali ina kila aina ya sababu ya kuliangalia basi ni kwamba hivi ni kwa namna gani inavyoweza kuwaboreshea na hawa maana shilingi 20,000/= ya wakati ule si 20,000/= ya sasa kwa maana kwa sasa thamani yake imeshuka kabisa. Lakini hata wale wazee wetu wa Mahakama , wale wazee wetu wa Mahakama wakati mwingine wanasingiziwa kwamba hawatendi haki kule, lakini ukija kuangalia kwanza sijui wanalipwa shilingi 1,500/= kwa kesi na kesi hiyo mpaka ije iishe.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna kesi inamaliza zaidi ya miaka mitatu, yeye anasubiri shilingi 1,500/=. Lakini hata hivyo hiyo kesi ikishakamilika kuja kuipata nako ni mbinde. Sasa wakati mwingine ukienda kule na kesi yako, basi anasema hebu zungumza zungumza vizuri ili mambo tuweze kuteteatetea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo baadhi ya mambo machache ambayo nilidhani na mimi niyachangie, lakini Serikali kwa maana kwamba inahitaji ione ni namna gani inaweza kuangalia katika maeneo yote ya utumishi na ione ni kwa kiasi gani inavyoweza

kuyaangalia na baada ya kuboresha na sasa tunaamini Watanzania wote wanaweza wakaenda kwa ari mpya, na mambo yote yakaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo nakushukuru sana na ninarudia kusema naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nakushuru pia kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Naomba nichukue nafasi ya pekee kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na wataalam wake kwa kuweza kuandaa hotuba hii na kuiwasilisha hapa kwetu Bungeni. *(Makofi)*

Naomba niende moja kwa moja kwenye mchango wangu ambao ni kidogo. Naomba kuzungumzia suala la watumishi wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu vijijini. Kumekuwepo na tatizo la watumishi wengi wa sehemu ya vijijini kukataa kwenye vituo vya kazi na wengine inafikia hatua kabisa kuacha kazi kuliko aende vijijini kwa sababu ya mazingiza magumu na wakati huo huo Serikali haijatoa kipaumbele kwa wale wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watumishi wa sehemu ya sekta ya elimu na sekta ya afya ambao ni muhimu sana na sekta nyingine ambayo ni muhimu lakini wamekuwa ni wachache kwa sababu wengi wao wnakataa maeneo hayo. Mimi natoa ushauri kwa Serikali na kwa Wizara husika kwamba waandae utaratibu maalum wa kuwepo na motisha kwa wale watumishi wanaofanya kazi vijijini ili waweze kuvutiwa kufanya kazi maeneo hayo na kuacha kukimbilia mijini. Pengine hii itasaidia kuona kwamba mazingira wanayofanyia kazi ni magumu lakini Serikali inawajali na inawaangalia pamoja na yale mazingira wanayofanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huo ni ushauri wangu, naomba kuwepo kwa motisha kwa watumishi hao ili jamii za vijijini pia waweze huduma kama wanavyopata jamii za mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni tatizo la watumishi kufanya kazi kwa miaka mingi bila kupandishwa vyeo. Kwa kweli hili ni tatizo kubwa, maeneo mengi sana na sekta ambazo watumishi wamefanya kazi *almost* miaka 15 hadi 20 hawajawahi kupanda cheo pale walipo. Mtu anaanza kazi akiwa na *qualification* ya *certificate* anakwenda shule anapata *diploma,* anakwenda shule anapata digrii, lakini cheo chake kipo pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huku si kukatisha tamaa watumishi wetu kufanya kazi na tutawa-*motivate* vipi wale wengine pengine wangependa kwenda shule lakini wanaona hata wale walioenda shule elimu waliyoipata bado wako kwenye cheo kile kile. Hii hapa athari yake ni kwamba wanapostaafu sasa wakati huo ile pensheni wanayopata inakuwa haiendani na hali halisi na huduma waliotoa kwa miaka yote.

Kwa hiyo, naishauri Serikali ihakikishe kwamba sekta zote watumishi wanaangaliwa, wapandishwe vyeo kwa muda unaotakiwa ili waweze kumudu maisha yao

kikamilifu na pia baada ya kustaafu waweze kuendelea na maisha mengine kwa sababu wengi wao wanapata fedha kidogo, wakikaa mwaka mmoja, wa pili pengine wanakufa kwa sababu fedha waliyopata ni kidogo, haiwasogezi popote.

Mheshimiwa Spika, lakini kama hawakujiandaa vizuri, wakiwa kwenye utumishi basi inakuwa ni hatari na inakuwa yeye pamoja na familia yake pamoja wanakuwa katika maisha magumu ambayo huwezi kuamini kwamba aliwahi kufanya kazi Serikalini. Kwa hiyo, suala la watumishi kupandishwa vyeo liangaliwe na Wizara ilitilie umuhimu wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la watumishi wanaofanya kazi kwenye sekta za binafsi yakiwepo mashirika na sehemu mbalimbali. Watumishi hawa ni watumishi wa umma pia, kwa sababu wanatoa huduma kwa jamii ambayo tunaitegemea. Serikali haiwezi kuwa na uwezo wa kuajiri watu wote Serikalini, haiwezi kuwa na uwezo huo.

Kwa hiyo, ni lazima wengine wao wafanye kazi kwenye sekta binafsi ikiwa ni sehemu mojawapo ya ajira. Lakini mazingira wanayofanyia kazi watumishi hawa kwenye sekta binafsi ni magumu kabisa nan yanasikitisha. Wengine unakuta wana mshahara kidogo sana, Serikali imeweka kiwango cha chini cha mshahara sasa hivi lakini kaangalie kwenye sekta binafsi, mishahara ya chini iko shilingi 30,000/=, shilingi 40,000/=, na shilingi 50,000/= fikiria maisha ya sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, maisha ya sasa hivi mfanyakazi anapewa shilingi 40,000/= kwa mwezi, ataishije? Inapelekea watu kuingia kwenye biashara nyingine ambayo watu hawakustahili kuingia, kwa sababu ya hali ngumu na kwa sababu maisha ni magumu, hana la kufanya anasema bora nikae hapa, lakini angalau ijulikane niko kazini, wakati huo huo kweli ile kazi haimsaidii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba Serikali iweke utaratibu wa kuyabana mashirika binafsi, watu wenye sekta binafsi waweze kutoa mishahara inayotakiwa waweze kutoa huduma zinazotakiwa kwa wafanyakazi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wengi wa sekta binafsi kwanza hawana suala la *NSSF*. Siku ukiugua tu ndiyo mwisho wa kazi. Akiugua na akilala nyumbani kwa muda wa wiki moja hajafika kazini, anakuta barua ya kuachishwa kazi.

Mheshimiwa Spika, wananyanyasika, wanaonewa lakini hawana utetezi. Tunaomba sana Serikali iangalie upande wa sekta binafsi ni sekta inayosaidia sana wananchi kujiondoa kwenye umaskini kwa kuwa mwananchi hawawezi kuishi bila kazi. Lakini pia wananchi hawa wanafanyanyanyaje kazi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba kabisa Serikali iliangalie hili kwa makini, iangalie sana kwa makini, wafanyakazi wengi ambao wako kwenye sekta binafsi lakini wanashindwa kumudu maisha kwa sababu wanachokipata ni kidogo na hata baada

ya kumaliza kazi bado hawana *NSSF,* hawana kitu ambacho angalau kitawasaidia kwa maisha ya baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA (MHE. PHILIP S. MARMO):** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, awali ya yote nasimama hapa kuunga hoja hii mkono na kumpongeza sana mwenzangu Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, kwa kuwasilisha hoja yetu hii kwa umahiri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vile hii ni mara yangu ya kwanza kuongea rasmi katika Bunge hili na hususan katika Ukumbi huu mzuri, naomba nichukue fursa hii kwa niaba yangu mwenyewe, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mbulu ambao nawawakilisha katika Bunge hili.

Nampongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana wakati wa uchaguzi uliopita kuwa Rais wa nchi yetu na hivi karibuni kwa kuchaguliwa kwa kauli moja na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa chama chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa tena kuwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi pia naungana na wenzangu labda baada ya kukupongeza wewe, naomba nimpongeze pia Mheshimiwa Edward Lowassa, Mbunge wa Monduli, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, kuwa Waziri Mkuu na Wabunge kuidhinisha uteuzi huo kwa kauli moja. Naamini umakini na umahiri wa utendaji wake utaendelea kuwa hazina kubwa katika Bunge lako na katika nchi yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niungane na wenzangu kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kuwa Spika wetu na Mheshimiwa Anne Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Nawapongeza Wenyeviti wote wawili, Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Jenista Mhagama. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu ama kwa kuchaguliwa au kwa kuteuliwa na kuwa Wabunge wa Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii vile vile kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Luteni Yusuf Makamba, kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa chama chetu. Nawapongeza pia wasaidizi wake. Nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa hizo muhimu kwa Wabunge wote na kwa Naibu Mawaziri wote na Mawaziri wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kuwa mimi nawahakikishia ushirikiano wangu wa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binafsi natoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani yake kwangu na kuniteua kuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi yake hususan kuongoza eneo la Utawala Bora. Naahidi kuwa nitatekeleza majukumu niliyopewa kwa bidii na kwa uwezo wangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatimaye shukrani zangu nyingi ziwaendee wananchi wote wa Jimbo la Wilaya ya Mbulu, kwa vile kwa mara nyingine wameonyesha imani yao kwangu kwa mara ya tano mfululizo wamenichagua kuwa Mbunge wao na mara zote kwa kura nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaahidi kuwa kama ilivyo desturi yangu nitawatumikia kwa uwezo wangu wote na muda wote nitaweka maslahi yao mbele kuliko maslahi yangu, yale tuliyoyafanya kuendeleza Wilaya yetu siku zote si haba, mimi naamini tukijaaliwa katika miaka minne ijayo tutafanya makubwa zaidi *inshallah. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wengi ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge wanafahamu dhana na upana wa dhana ya Utawala Bora. Nisingependa kuwasumbua kwa kutoa ufafanuzi tena.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la Utawala Bora ni eneo linalosemwa sana hapa Bungeni, nje ya Bunge, kwenye vyombo vya habari, kwenye magazeti kila siku, ni eneo la rushwa. Rushwa ni adui wa haki, rushwa mbaya, wengine huita kwamba ni kansa hasa katika jamii na katika Taifa.

Mimi napata faraja kulieleza Bunge lako leo kuhusu jitihada za Serikali kuhusu jinsi tunavyolishughulikia tatizo hili. Baada ya matamshi ya watu mashuhuri wawili duniani katika mapambano dhidi ya rushwa katika juma hili.

Mheshimiwa Spika, hawa sio wengine, mmoja ni John Williams, mgeni wangu, Mwenyekiti wa Mtandao wa Wabunge Wanaopambana na Rushwa Duniani, *Global Organization for Parliamentarians and Anti Corruption* yaani *GOPAC,* ambaye alisema kuwa rushwa ni tatizo la dunia nzima, ni changamoto ya kila Serikali duniani.

Mheshimiwa Spika, wiki hii pia Jaji Lingera, Mwenyekiti wa Tume ya Kupambana na Rushwa ya Kenya yaani *Kenya Anti Corruption Commission* alipoulizwa na waandishi wa habari kuwa kwa nini Tume yake imeshindwa kuwakamata hawa wala rushwa wakubwa?

Mheshimiwa Spika, jibu lake lilikuwa ni kwamba hawa watoa rushwa wakubwa au wala rushwa wakubwa pia wana mifuko mikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ni matamshi mazito yanatoka nje ya mipaka ya nchi yetu. Hivyo naomba nirejee kwamba rushwa kwa hakika ni tatizo la binadamu na limefanyiwa utafiti wa kina kwa karne nyingi na majibu yamepatikana.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba rushwa hasa ni dalili ya uozo fulani katika jamii kwamba kuna matatizo katika uendeshaji wa shughuli zetu za kila siku, iwe Serikali, iwe chama cha Ushirika.

Mheshimiwa Spika, rushwa ni ishara ya utawala ambao siyo bora hata kidogo. Kukosekana kwa nidhamu katika matumizi ya Serikali, huduma mbovu na hafifu, kutokuwepo na udhibiti katika matumizi ya fedha za umma, dhuluma na ukiukwaji wa haki za binadamu, kutawanya fedha kwenye miradi bila mpangilio wowote na sisi kama Taifa tuna bahati kwamba waasisi wetu waliweza kutambua hatari ya rushwa katika jamii. *(Makofi)*

Hatari ya kutokuwa na uadilifu katika jamii. Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alichukia sana rushwa pamoja na mizizi yake. Kwa hakika, Tanzania kwa ajili hiyo, ilikuwa ya kwanza katika Afrika na katika nchi chache sana za dunia ya tatu, ambayo katika miaka ya 1960, 1970 na mwanzoni mwa 1980, ilikuwa imeanzisha taasisi za Serikali za Utawala Bora, kama vile Tume ya Kudumu ya Uchuguzi mwaka 1962, Kikosi cha Kuzuia Rushwa mwaka 1971 na wakati huo huo masuala ya haki za binadamu, yalikuwa Kaskazini na Kusini mwa Ulaya na duniani kote. Sehemu ambapo Utawala Bora ulikuwepo, ulikuwa unazingatiwa na umefanyiwa utafiti, ilikuwa ni Tanzania na ndio maana Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika mwisho wa miaka ya 1970 na mwanzoni wa miaka1980, ikawa ni kitovu cha kutolea elimu kuhusu *Ombudsman,* ambako kwetu tulikuwa tumewaita Tume ya Kudumu ya Uchuguzi.

Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya rushwa na uovu katika enzi hizo kwa kifupi ilikuwa kama hivyo. Lakini katika Karne ya sasa ya 21, mapambano yanabadilika jinsi ambavyo sura ya rushwa inabadilika. Malengo ya Serikali sasa ni kutunga sheria mpya itakayozingatia mazingira ya rushwa ya Karne ya 21. Tutakuwa na Kamati za Maadili katika Idara zote za Serikali ili kutathmini kila wakati, maadili, hali ya rushwa na pia kuziba mianya ya rushwa.

Kutakuwa na programu za kuboresha utawala katika nyanja zote za Serikali. Sote ni mashahidi, kazi hii inaendelea, mfano ni Maboresho katika Utumishi wa Umma *(Public Service Reform Program)*, Uboreshaji katika Sekta ya Fedha *(Public Finance Management Program)*, Maboresho ya Serikali za Mitaa *(Local Government Reform Programs)*, Maboresho katika Sekta ya Sheria *(Legal Sector Reform Programs)*, Programu kadhaa za Kupambana na Umaskini, yaani MKUKUTA, MKURABITA, *TASAF* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hatua hii inaturudisha kwa yale matamshi ya mgeni wetu, Mbunge kutoka Canada, ambaye alikuwa mgeni wako na ni Mwenyekiti wa *GOPAC,* Bwana John Williams na Jaji Ligela kuwa, tatizo hili ni la dunia. Lakini Mheshimiwa Mbunge wa Canada alisema wazi kwamba, Tanzania ni mojawapo ya nchi ambazo

zinatambuliwa katika Jumuiya ya Kimataifa kwamba, inafanya jitihada za kupambana na adha hii ya rushwa na ndio maana mtandao wa Wabunge wanaopambana na rushwa duniani, umeamua kufanya mkutano wao wa pili, mwezi wa tisa huko Arusha, Bunge lako likiwa ni mwenyeji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaliyosemwa na Waheshimiwa Wabunge, mengi yalikuwa matamshi ya jumla na hii hali sio nzuri sana, kwa sababu rushwa ni tatizo kubwa. Unapotoa matamshi ya jumla, inapotosha hali halisi na hili ni Bunge linalotuangalia. Matamshi ya jumla, yanapopotosha hali halisi ya nchi, hatuitendei jamii yetu haki hata kidogo. Sehemu ya rushwa inajulikana, tungekuwa na ushahidi wa kutosha hapa, ambaye atathibitika ni mpokea rushwa au mla rushwa, adhabu yake ni kubwa sana. Wenyewe mnafahamu, Mawaziri na Wabunge wa nchi jirani, sasa hata kama wanaumwa, hawapewi *Visa* ya kwenda kutibiwa nchi za Ulaya. Sababu ni kwamba, wamejiingiza katika matatizo haya ya rushwa, kwa sababu rushwa ni dhuluma hasa kwa nchi changa kama ya kwetu, ambapo unapomdhulumu mnyonge ni kwamba, kwa kweli unahatarisha maisha yake.

Masuala haya madogo madogo ya jumla, yaliletwa hapa kwa mfano na Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, ambaye yeye ni Msemaji wa Upinzani kwa Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo na Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili. Tutajibu kwa maandishi, yale yote waliyotuelezea. Lakini kwa hakika, tusingependa tuwe tunaongelea jambo hili kijuu juu, tunataka tutoe mifano halisi ili hatua za dhati zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, imesemwa hapa kuwa, Mheshimiwa Rais, anawafahamu wapokea rushwa kubwa kubwa, tena kwa majina na wanashangaa kwa nini hawataji na hawapeleki mbele ya sheria. Mimi nataka kusema kwamba, Mheshimiwa Rais ni mtu makini sana, anazingatia Utawala wa Sheria, lakini bila shaka Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana nami kwamba, sio vema hata kidogo, kusambaza majina ya watu kwenda Mahakamani kwenye vyombo vya habari, bila kuwa na ushahidi wa aina yoyote wa kuweza kuthibitisha Mahakamani bila mashaka yoyote. Kila Mheshimiwa Mbunge hapa, anafahamu kuwa, kila Mtanzania, ana haki zote hadi hapo atakapopatikana na hatia mbele ya Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kesi moja moja, nisingependa kuliongelea ndani ya Bunge, kwa sababu wahusika hawataweza kutoa majibu hapa na hatutawatendea haki, lakini hili la Mheshimiwa Balozi Muhalu, niseme tu kwamba, uchunguzi bado unaendelea.

Mheshimiwa Spika, mengi yamesemwa kuhusu vyombo vyetu usalama, tena kwa uchungu, mimi sijui ni kwa nini, kwa sababu watumishi hawa wa umma wanalaumiwa sana badala ya kusifiwa, kazi zao ni saa ishirini na nne, hakuna sikukuu, wakati sisi tukilala wanatulinda, wanalinda mipaka yetu, sasa wafanye nini zaidi ya hapo. Kwa matukio madogo madogo, tuna vyombo vyetu, kuna Mahakama na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kwa upande wa Zanzibar, dosari iliyoko sasa, itarekebishwa baada ya Baraza la Wawakilishi, kuridhia maudhui yaliyo katika Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na itaanza kutumika kule Visiwani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TASAF*, nisingependa kusema mengi kwa sababu wenye macho wameona, hasa Kamati ile iliyotembelea Unguja na Pemba na mikoa kadhaa ya bara. Ni Mradi ambao kwa kweli umeibuliwa na wananchi, sisi si lolote wala si chochote hapa kuongelea mambo haya, kwa sababu Miradi yote ya *TASAF,* inaibuliwa na wananchi katika ngazi ya kijiji. Pili, *TASAF* ni mkopo wa Benki ya Dunia, lakini Benki ya Dunia haileti Mradi huu kama mvua inavyonyesha, inachunguza, tunakuwa na sifa, si nchi zote zenye sifa. Kwa hiyo, tuzisifu Serikali zote za Chama cha Mapinduzi, kwa kuwa na sifa ya kutambuliwa na mashirika makubwa makubwa kama Benki ya Dunia na kupata misaada kama hii ya *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nachukua nafasi hii, kuwashukuru tena Mawaziri wenzangu, Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Makatibu wote Wakuu na Viongozi wote wa Idara zote zilizoko Ofisi ya Rais, kwa kutuwezesha sisi kuwasilisha hotuba hii ya bajeti mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, SIASA NA UHUSIANO WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Napenda awali ya yote, nitamke kuwa naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Nianze kwa kumpongeza kwa dhati, Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa kuandaa na kuwasilisha vizuri sana, Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais ya mwaka 2006/2007. Amefanya hivyo kwa ufasaha, usahihi na kwa kujiamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba, waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi si Wabunge wengi sana, lakini wamejihusisha na masuala mazito na yenye maana kwa jamii yetu. Nichukue nafasi hii vile vile, kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Wajumbe wa Kambi ya Upinzani, kwa taarifa zao na michango yao kwa mawazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ofisi yangu katika Ofisi ya Rais, inahusu mambo ya Siasa na Uhusiano wa Jamii, ambayo kwa kifupi maana yake ni Mambo ya Siasa yote, masuala ya umoja wa taifa, masuala ya amani, utulivu, mshikamano, mambo ya vyama vya siasa na kadhalika. Vilevile pamoja na kujenga uhusiano na kufuatilia maendeleo ya makundi mbalimbali ya kijamii katika nchi yetu, ili Serikali wakati wote iwe karibu na wananchi inaowatumikia na kuwaongoza.

Makundi ya kijamii ni mengi, si lazima niyaorodheshe yote hapa. Naomba nikubaliane na Mheshimiwa John Cheyo, Mbunge wa Bariadi Mashariki, kwa sifa alizompa Mheshimwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa moyo wake wa uzalendo na nia yake ya kuimarisha umoja wa taifa letu. Kwa hakika, Rais Jakaya Mrisho Kikwete, ameonyesha dhamira iliyo wazi ya kuitumikia nchi yetu kwa moyo wake wote. Ndio maana ni muhimu kwa wazalendo wote tumsaidie ili tuweze kufanikisha kazi hiyo

kubwa. Aidha, nakubaliana naye kwa vyama vya siasa vilivyomo Bungeni, ndio kundi la kuanza nalo katika mjadala wa kisiasa ya Kitaifa. Mimi niko tayari na tutashirikiana katika shughuli hiyo, ushirikiano huu ulishajengewa misingi na yeye mwenyewe amehusika sana katika kipindi kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia kidogo suala la mpasuko uliopo kati ya Unguja na Pemba. Suala hili limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge katika hotuba zilizotangulia hasa za Bajeti, Waziri Mkuu na Ofisi ya Makamu wa Rais. Leo limezungumzwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma na pia na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Naomba tukubaliane kuwa, suala hili la mpasuko kati ya Unguja na Pemba, si la mpasuko la kijiogorafia, bali ni la mpasuko baina ya watu wa Unguja na wa Pemba. Linahusu jinsi watu pande mbili hizo wanavyowaona na wanavyowatafsiri, wanavyowahisi wenzao wa upande wa pili.

Jambo la pili ni kuwa, mpasukuo umejengeka kwa kipindi kirefu kwa miaka mingi na enzi mbalimbali. Kwa kweli ni mchakato wa kihistoria. Jambo la tatu, si rahisi kumpata yule aliyeanzisha mpasuko lakini inaelekea kwamba, watawala mbalimbali, wamechangia kwa namna zao katika suala hili.

Jambo la nne ni kwamba, yapo mambo ambayo yanachochea mpasuko na yapo vilevile mambo yanayoweza kusaidia kupunguza mipasuko na hapa ndio maana kuna suala zima na nafasi ya viongozi. Kwa sababu ni suala la watu na mara nyingi masuala kama haya ya Muungano, ama la mpasuko wa Unguja na Pemba, tafiti zinaonyesha mara nyingi kwamba, suala hili mara nyingi ni la viongozi. Linadumishwa na linakuzwa, kwa sababu ya misimamo ya viongozi. Wakati watu wa kawaida wanaendela kuoana, kuzikana na kufanya urafiki, viongozi ndio wanazungumzia matatizo. Kwa hiyo, viongozi wana nafasi kubwa sana katika hili, kwanza lazima viongozi wakili kwamba mpasuko upo. Kwa sababu kutokukiri ukweli ni kukataa kutafuta ufumbuzi. Sawa sawa na mtu mgonjwa, lakini anasema yeye si mgonjwa, haumwi. Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema, mficha ugonjwa, kifo kitamfichua. Sasa si vizuri kungoja mpaka ufe. Kwa hiyo, ni muhimu tukiri kwamba, mpasuko upo.

La pili, tukubali kwamba, mpasuko huu hausaidii maendeleo ya Zanzibar, wala hauleti maslahi kwa wananchi wa Zanzibar na kwamba unaathiri maslahi ya Zanzibar na ya Tanzania. *(Makofi)*

La tatu, haisaidii kutupiana lawama, haisaidii kusema hii ni shauri ya *CUF,* wala haisaidii kusema hii ni shauri ya CCM. Pande zote mbili, zina mchango wake na katika kutafuta suluhisho, itabidi pande zote mbili zikiri kwamba, tuna tatizo halafu pande zote mbili zikubali, tukae tuzungumze, tutafute jawabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na maneno hayo machache na kwa sababu muda wangu ni mfupi, nataka niseme tu kwamba, hatujaanza kazi za wazi wazi za kisiasa, kwa sababu sasa ni miezi sita tu na kipindi hiki baada ya uchaguzi sisi wengine tunafikiria kwamba, kila chama kinatakiwa kikae, kitazame kidogo madonda yake. Tumeumizana

umizana kwenye uchaguzi huko, kwa hiyo, lazima tukae na kuzungumza. Sisi CCM tuna utaratibu wa kukaa na kujikosoa na kujiandaa upya, tunaamini kwamba na wenzetu wa vyama vingine, wana utaratibu huo. Nadhani sasa wakati mzuri umefika, tumeshafanya *criticism* na *self criticism,* sasa tayari tunaweza tukaanza kukaa na kuzungumza ili tuweze kwenda pamoja, kujenga Tanzania iliyo bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuwashukuru sana wote kwa kunisikiliza. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo, ili niweze kuhitimisha hoja yetu, ambayo niliitoa leo asubuhi. Kwanza, napenda kumshukuru tena na kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Awamu ya Nne, lakini pia kwa kuniteua kuwa Waziri katika ofisi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Serikali ya Awamu ya Nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuchaguliwa kwanza, kuwa Mbunge wa Monduli na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, kuwa Waziri Mkuu na kuthibitishwa kwa wingi wa kura nyingi katika Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kwa namna ya pekee, kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mtwara Vijijini, kwa kunichagua kuwa Mbunge wao, nikiwa mwanamke wa kwanza kuchaguliwa katika Jimbo la Mtwara Vijijini tangu lianze. Napenda kuwaahidi kwamba, sitawaangusha, nitakuwa mwakilishi wao mzuri na nitajitahidi kuwatumikia kadiri Mwenyezi Mungu, atakavyokuwa amenijalia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati, Mawaziri wenzangu, tulio katika Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Philip S. Marmo na Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, kwa ushirikiano mzuri, ambao umetuwezesha kutekeleza majukumu yetu ipasavyo. Aidha, napenda niwapongeze kwa kutoa ufafanuzi mzuri wa hoja za Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe mwenyewe, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge, kwa kutuongoza vyema katika Kikao hiki cha Bajeti. Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote, kwa michango yao endelevu, ambayo imesaidia sana na itaendelea kusaidia, kuboresha utendaji wetu wa kazi. Mafanikio haya yanatokana na misingi imara ya utawala, hazina ya busara, uzoefu na ushirikiano tulionao ndani ya chama na haya yanawezekana kutokana na kuendelea kuwepo kwa amani na utulivu katika nchi yetu, pamoja na mazingira mazuri ya kisera, sheria, kanuni na taratibu madhubuti za kusimamia na kuendesha uchumi, kwa kuzingatia Utawala Bora na uwazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia, kuwashukuru na kuishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa G. Malima Lubeleje, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi na Wajumbe wote wa

Kamati, kwa ushauri na maelekezo, yao ambayo yametuwezesha kufika hapa tulipo hii leo. Aidha, nachukua fursa hii, kuishukuru Kambi ya Upinzani, kwa michango yao ambayo itasaidia kuboresha utendaji wetu wa kazi. Michango yao itatuwezesha kufanya kazi kwa juhudi na maarifa na hatimaye kuboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru kwa dhati, Wabunge wote, ambao wamechangia katika hoja hii ya Ofisi ya Rais, Utumishi, Utawala Bora, Siasa na Uhusiano wa Jamii. Napenda kuwahakikishia kwamba, mapendekezo yao, maoni, pamoja na ushauri wao, tutavizingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo Waheshimiwa Wabunge, ambao wamechangia kwa kuzungumza na wengine wamechangia kwa maandishi. Aidha, kuna wengine ambao walichangia wakati wa kujadili hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na pia katika Wizara mbalimbali, ambazo zimetangulia kabla ya Wizara yetu.

Naomba niwataje kama ifuatavyo: Mheshimiwa George M. Lubeleje Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Pindi H. Chana na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis.

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kuzungumza katika hotuba hii ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Balozi Hamisi S. Kagasheki, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi na Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walichangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Dr. James M. Wanyacha, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Celina O. Kombani, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Dr. Batilda S. Buriani, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka na Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika hotuba yetu, sasa napenda kutolea maelezo hoja zao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja nyingi zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, lakini hoja kubwa ambayo imezungumzwa ni suala la kuboresha maslahi ya watumishi wa umma. Azma ya Serikali ya Awamu ya Nne, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ni kuhakikisha tunaboresha maslahi ya watumishi wa umma. Chini ya dhamira hiyo ya dhati, imejidhihirisha kwa kuanzia na mwaka huu wa fedha, ambapo Serikali imetenga kiasi kikubwa cha fedha, kwa ajili ya maslahi ya watumishi wa umma. Pamoja na juhudi hizo, vile vile Mheshimiwa Rais, ameiunda Tume, ambayo itaangalia upya maslahi ya watumishi wa umma nchini, kwa kutambua kwamba, watumishi wa umma ni injini kama vile mmoja wetu alivyosema, ni roho. Kwa hiyo, Serikali imeliona hilo na inaangalia kiungo hiki muhimu katika kukuza uchumi na kuleta maisha bora kwa Mtanzania, kinapewa motisha lakini pia maslahi yake yanaboreshwa.

Mheshimiwa Spika, katika hoja hiyo hiyo ya kuboresha maslahi ya watumishi wa umma, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, alipendekeza kwamba, kima cha chini cha mshahara kiwe Sh.300,000. Kama nilivyosema, Serikali bado inaendelea kuboresha maslahi ya umma, lakini pia uboreshaji wa maslahi ya watumishi wa umma, yanaendana na uwezo wa Serikali, kuweza kulipa na wakati huo huo kutekeleza Miradi mingine ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tukichulia mfano kima cha chini kama kitakuwa Sh.300,000 au tuseme wale ambao wanalipwa chini ya Sh.300,000, basi tukisema tuwalipe Sh.300,000, Serikali itahitaji shilingi trilioni 2.1, sawa na asilimia 12.7 ya Pato la Taifa au sawa na asilimia 88 ya mapato ya ndani ya Serikali. Nimezungumza hivyo ili tuone kwa kiasi gani tunavyosema kwamba, uwezo wa Serikali ndio unaotegemea pia kuboresha maslahi ya watumishi. Ni nia ya Serikali kuboresha maslahi ya watumishi wake lakini pia uwezo wa uchumi nao unategemea, ndio maana tunasema watumishi tukazane kukuza uchumi wetu, tujitume ili pato liongezeke na maslahi yaboreshwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiwango cha pensheni ya watumishi kinategemea na mshahara wake wakati wa kustaafu. Ukweli kiwango cha pensheni kwa watumishi waliostaafu katika miaka ya 1980 hadi 1990, ni kidogo kutokana na ukweli kwamba, mishahara ya wakati huo ilikuwa midogo. Kwa kutambua tatizo hilo, Serikali imekuwa ikihuisha viwango vya pensheni kulingana na uwezo wa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyotolewa ni kuhusu Menejementi ya Utumishi wa Umma, kusimamia malipo ya mishahara katika sekta binafsi hususan kima cha chini cha mshahara. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyacha na Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria Na.6 ya mwaka 2004, kima cha chini cha mshahara, hupangwa na Wizara ya Kazi, baada ya kushauriana na Bodi ya Kima cha Chini (*Minimum Wage Board),* iliyoteuliwa na Waziri wa Kazi. Kama kuna shirika linalolipa chini ya kiwango kilichowekwa na Serikali, linakiuka sheria na linastahili kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuhusu wageni kutoka nchi jirani, wanaochukua nafasi za kazi za Watanzania hasa katika sekta ya hoteli na shule zinazotoa mafunzo kwa lugha ya Kiingereza. Ni utaratibu gani unaotumika katika kutoa vibali vya ajira hizo?

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya hoteli ni za wawekezaji binafsi. Wawekezaji wanapoomba kuwekeza, wanaleta maombi yao Serikalini, ikiwa ni pamoja na mahitaji ya watumishi. Pale ambapo wawekezaji wanahitaji watumishi kutoka nje ya nchi, huwasilisha maombi yao Wizara ya Kazi, Ajira na Vijana, kwa uchambuzi kabla ya kuridhia vibali hivyo. Baada ya uthibitisho wa Wizara ya Kazi, maombi hayo huwasilishwa Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa ajili ya taratibu za uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusu mishahara inayolipwa wataalam wa kigeni kuwa, mikubwa kuliko ile ya wataalam wazalendo. Wataalam wa kigeni walioko nchini, ni wale wanaoajiriwa katika Miradi inayofadhiliwa na mashirika ya nje. Hivyo, mishahara ya wataalam wa aina hiyo, inalipwa na wafadhili wenyewe na hivyo Serikali haina sababu ya kuingilia utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimarisha uwajibikaji wa watumishi wa umma. Namshukuru Mheshimiwa Martha J. Umbulla, kwa ushauri wake, ambao nitauzingatia. Kama nilivyosoma kwenye hotuba yangu, Serikali itaendelea kuweka na kuimarisha mifumo ya uwajibikaji, pamoja na kuboresha maslahi yao. Aidha, katika kutekeleza Sera ya Menejementi ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Serikali inaweka misingi ya kuimarisha utendaji unaojali matokeo.

Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, alizungumzia kuhusu Polisi kukataliwa kurudi kazini baada ya kumaliza mikataba ya kuazimwa. Sera ya Serikali ni kuwaruhusu wafanyakazi kwenye mashirika na taasisi zenye uhusiano na Serikali ili kuwajengea uwezo wao. Ofisi haina taarifa na tatizo hili na naahidi kuwasiliana na Waziri wa Usalama wa Raia, kutatua tatizo hili kama lipo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la upungufu wa watumishi katika Sekta ya Afya, Wakuu wa Idara kukaimu katika Halmashauri kwa muda mrefu, kupeleka madaraka ya kutoa vibali kwa waajiri na pia lilizungumziwa suala la upungufu wa watumishi katika taaluma ya uhasibu hasa katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu ilishatoa vibali vya kuwathibitisha Wakuu wa Idara wenye sifa katika Halmashauri. Waziri mwenye dhamana na Tawala za Mikoa na

Serikali na Mitaa, sasa hivi analifanyia kazi na mpaka sasa hivi ofisi yangu imeshapokea zaidi ya asilimia 90 ya Wakuu wa Idara, ambao walikuwa wanakaimu, ambao wamerekebishiwa mishahara yao, tayari kwa kuanza kuwathibitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu watumishi wa Sekta ya Afya na Elimu, ofisi yangu imetoa kibali kwa Wizara ya Afya, Elimu na Fedha, kuwapangia kazi wahitimu kutoka vyuoni, moja kwa moja bila kutangaza nafasi hizo kwa ushindani. Hivyo, kuna tatizo la upungufu wa idadi ya mahitaji kulingana na mahitaji. Kama tulivyosema, Walimu, Wahasibu na hata Sekta Afya, sasa hivi hatufanyi ushindani. Tatizo ni kwamba, katika soko la ajira, wataalam wa fani hizo ni wachache. Hivyo, natoa raia tuzidi kuwasisitiza vijana wetu, sasa hivi waende wakasome kwenye kozi ambazo sokoni bado wanahitajika badala ya kwenda kusoma kozi ambazo wanajua kabisa, soko limeshajaa, sasa hivi tuko katika utandawazi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa utoaji vibali ulioanzishwa, ulianzishwa ili kudhibiti bajeti ya mishahara, pamoja na ajira za watumishi hewa. Hata hivyo, ofisi yangu imeunda Kamati ya kuangalia taratibu za utendaji, yenye lengo la kuboresha utendaji kazi kwa kupunguza umangi-meza. Aidha, suluhisho la muda mrefu la tatizo la vibali, litapatikana baada ya kupeleka usimamizi wa mfumo wa pamoja wa taarifa za kiutumishi na mishahara kwa waajiri. Hatua hii imeanza kutekelezwa kwa Wizara chache.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la semina kwa viongozi wetu kwamba, zimezidi mno kama afya, ma-*DED* na elimu. Hili lilizungumzwa na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, pamoja na Mheshimiwa Fatuma A. Mikidadi. Lengo la semina kwa viongozi, linakusudia kuwajengea uwezo wao wa uongozi.

Hata hivyo, pamoja na kuwajengea uwezo huo, Waraka kutoka ofisi yangu, ulitoa maelekezo kwamba, watumishi wasiwe nje ya vituo vya kazi kwa zaidi ya siku 60 kwa mwaka. Ofisi yangu itaendelea kufuatilia utekelezaji ili waajiri wazingatie Waraka huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mipango ielekezwe kuhusu kuongeza nafasi za wanawake mpaka asilimia 50. Kulingana na makubaliano ya Kimataifa, Serikali imekuwa ikitekeleza mpango huu wa kufikisha asilimia 30 ya wanawake. Kwa mfano, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu, ofisi yangu tumejiwekea lengo la kutoa mafunzo kwa wanawake 230 ili kuwajengea uwezo wa utendaji ili waweze kushika nafasi za madaraka kwa sababu sio tupewe tu, lakini pia lazima tuonyeshe uwezo na ili tuwe na uwezo basi, tunatakiwa kuwajengea uwezo. Hivyo, ofisi yangu itatoa mafunzo kwa wanawake 230 ili waweze kushindana na wanaume ikiwezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Watendaji wa Kata na Vijiji kuingizwa kwenye *payroll,* napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, hadi kufikia Juni, 2006, Watendaji wa Vijiji na Mitaa wapatao 9,102 walikuwa wameingizwa kwenye orodha ya malipo ya mishahara, kati ya watendaji 12,599 walioidhinishwa kuajiriwa. Idadi ya Watendaji 3,497 waliosalia, wataingizwa kwenye orodha ya malipo ya mishahara, baada ya taarifa zao kupokelewa na ofisi yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watumishi elimu na afya kukaa muda mrefu bila mishahara. Ofisi yangu inachukua hatua za kushughulikia tatizo hili, kwa kuanzisha sehemu moja *(One Stop Center),* ya kushughulikia mishahara ya watumishi hususan Walimu, kuondoa umangi-meza katika taratibu za utendaji katika utumishi wa umma, lakini pia kwa kupeleka kwa waajiri, jukumu la kusimamia mfumo wa pamoja wa taarifa za kuitumishi na mishahara. Mwaka huu tunategemea tuanze haraka iwezekanavyo katika Wizara ya Elimu, kwa kupelekea huu mtandao, tumeshawapelekea lakini kuutumia kikamilifu, tutasimamia kuhakikisha wanautumia ili kuondoa adha kwa Walimu wanaoajiriwa.

Mheshimiwa Spika, nafasi mpya za ajira na mbadala 10,628, ambazo hazijajazwa. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini. Nafasi hizi ambazo hazijajazwa, zinatokana na ukosefu wa watumishi wenye sifa, kwa baadhi ya maeneo. Kwa mfano, Wizara ya Elimu, wana vibali vya kuajiri Walimu mpaka tunakaribia kuufunga mwaka huu walikuwa na kibali cha Walimu zaidi ya 1,500, ambacho hawajakitumia pamoja na kuwachukua wale walioko mashuleni. Kwa hiyo, sio kwamba, hizo nafasi zinaachwa kwa makusudi, zinaachwa kwa sababu watumishi wa kuajiriwa kwa nafasi hizo wanakuwa hawapo. Pia baadhi ya wahitimu kutopendelea kwenda kufanya kazi katika baadhi ya maeneo, hata wakipangiwa wanaacha kwenda, kwa hiyo, ile nafasi unaikuta kwenye Halmashauri imekaa, pamoja na kwamba wamepata kibali.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa kukabiliana na tatizo hilo ni kuruhusu Wizara ya Elimu, Afya na Fedha, kuwapangia wahitimu moja kwa moja bila ushindani, lakini pia waajiri wanaendelea kushauriwa, kuboresha mazingira ya kazi ya maeneo yao ili kuvutia waajiriwa. Kama vile wenzetu wa Mkoa wa Rukwa, lakini pia hata Mkoa wa Mtwara na baadhi ya Mikoa mingi tu, wamejiandaa kuwapokea Walimu ili wakifika wasipate matatizo na hivyo kukimbia. Hivyo, tunawashauri na maeneo mengine waendelee kuwavutia watumishi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze watumishi wa afya hasa Madaktari Bingwa, tatizo hili linatokana na uhaba wa Madaktari Bingwa hapa nchini, wachache waliopo wanajichagulia hospitali za kufanyia kazi. Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kazi, pamoja na mishahara ili kuwavutia watalaam hao, kwa kufanya kazi maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni Serikali iangalie uwezekano wa kutoa vibali vya muda vya ajira, kuwawezesha Walimu ambao hawajapata kazi. Walimu wote wanaohitimu mafunzo yao, wanapangiwa vituo vyao vya kazi na bado nafasi zipo hivyo, hakuna sababu ya kutoa vibali vya muda. Zipo nafasi kwa ajili ya Walimu, lakini pia wameruhusiwa kuwatumia wahitimu wa Vyuo Vikuu na pia kutumia wanafunzi wa Kidato cha Sita.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kutoka kwa Mheshimiwa John M. Cheyo, kuhusu *Employment Allowance,* kwa nini na inafanya nini. *Employment Allowance,* ni posho zinazotumika kumwezesha mtumishi kutekeleza majukumu yake na sio sehemu ya

maslahi ya mtumishi wa umma. Kwa mfano, posho hizi ni kama posho ya kujikimu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kufuatilia wahitimu vyuoni ili wajiunge na utumishi wa umma. Tunapokea pendekezo hili na Serikali itaweka mikakati ya kujitangaza zaidi ili kuwavutia wahitimu wajiunge na utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kufanya tathmini ya ushirikishaji wa Sekta Binafsi, ofisi yangu imepanga kufanya tathmini hii katika mwaka huu wa fedha 2006/2007. Aidha, Wizara na taasisi binafsi, zinazotekeleza mpango huu, zinaonyesha kuridhishwa na ushiriki wa Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tathmini ya uwezo wa Serikali kutekeleza mipango yake, hili tutawasilisha Wizara ya Fedha na kuona kama tathmini inaweza kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwepo na malimbikizo ya mishahara wakati fedha zinarudishwa, tatizo hili linasababishwa na waajiri kuchelewa kuwasilisha fomu za kudhibiti ajira na *data sheet* kwa muda muafaka hivyo, kusababisha watumishi kuchelewa kulipa mishara. Tatizo hili linashughulikiwa na ofisi yangu, kwa kupeleka usimamizi wa taarifa za watumishi na mishahara kwa waajiriwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala kuhusu takwimu za wataalam wa Kitanzania wanaofanya kazi nje, takwimu zitatafutwa na wakati muafaka ukifika, zitawasilishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kwa vijana, Serikali inaweka mazingira ya kuwawezesha vijana kujiajiri na pia kuajiriwa kwa wale wenye sifa.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi kukatwa makato ya mishahara yao bila ridhaa yao. Makato yote katika mshahara wa mfanyakazi lazima yapate ridhaa ya mtumishi mwenyewe, isipokuwa makato yale ambayo yako kisheria mfano, kodi, hii ipo kisheria, kodi hata kwa mfanyabiashara, sidhani kama unahitaji kupata ridhaa yake.

Mheshimiwa Spika, suala la vijana wa Tanzania waliopata ajira nje ya nchi, kama Libya ambazo Mheshimiwa Rais alizitaja, hili nadhani nimeshalijibu, takwimu zitatafutwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la rasilimali watu inatumikaje, watu wanasoma lakini hawatumiki. Kama nilivyosema, Serikali inaboresha mazingira ili wananchi wawaze kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala linasema, je, kwa nini ongezeko la mishahara linasubiri tu mpaka Mei Mosi au Mheshimiwa Rais atangaze, badala ya kuangalia vitu kama *inflation*. Utaratibu wa kuongeza mishahara huzingatia bajeti na uwezo wa Serikali. Ongezeko lolote la mishara, hutekelezwa baada ya kupitishwa bajeti

na Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo, haiwezekani kutamka wakati wowote kwamba, sasa hivi kwa vile *inflation* imependa, basi na mishahara tunapandisha.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala lililoulizwa na Mheshimiwa Peter J. Serukamba kwamba, tubadili fikra katika utendaji wa kazi. Kazi ya kubadili fikra za watumishi katika kuboresha kazi ni kazi endelevu na inatekelezwa katika programu ya kuboresha utendaji kazi katika utumishi wa umma.

Maeneo maalum yanayolenga katika kuwajengea uwezo watumishi utendaji wao wa kazi ni pamoja na mfumo wa kupima utendaji wao wa kazi, mikataba ya huduma kwa wateja, mafunzo kuhusu maadili na pia kuelimisha watumishi kuhusu mipango ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na suala kwamba, Wakala za Serikali na wenyewe wasijione kama si sehemu ya Serikali. Kuhusu miundo ya utumishi, Wakala za Serikali utaratibu ni kwamba, miundo hiyo haiwezi kutekelezwa bila kuchambuliwa na kuidhinishwa na Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma. Lengo ni kuhakikisha kwamba, inazingatia sera, kanuni na taratibu za utumishi wa umma. Hivyo, Wakala za Serikali ni sehemu ya Serikali.

Kuhusu suala la mafunzo, Wakala na Wizara zote, zina mipango ya mafunzo. Aidha, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, katika bajeti yake ya kila mwaka, hutenga fedha za kujenga uwezo wa Wakala kwa kutoa nafasi za mafunzo kwa watumishi wake.

Kulikuwa na suala la Walimu, hawana mwenyewe, wanawajibika kwa nani? Walimu wanawajibika kwa mamlaka zifuatazo kwa mchanganuo ufuatao: Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu na Ufundi kwa Walimu wa Sekondari na Vyuo vya Ufundi na vyuo vya Mafunzo ya Ualimu; Wakurugenzi wa Halmashauri kwa Walimu wa Shule za Msingi na Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa Walimu au Wakufunzi wa Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika Mheshimiwa Suzan A. J. Lyimo alisema, Walimu wa Shule za Msingi hawana muda wa kujiletea maendeleo na hawawezi kufanya *tuition* ili kuboresha maisha yao. Hili tutaliekeleza kwa Wizara ya Elimu na siku ikifika nadhani litajibiwa.

Suala la walemavu kupewa kipaumbele katika ajira. Napenda kulitaarifa Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara ya Kazi na Ajira, ndio inayotoa Sera ya Walemavu na hata hivyo, waajiriwa wanahimizwa kuwapa kipaumbele walemavu katika ajira ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka, alipenda kufahamu utaratibu wa upimaji wa kazi wa wazi wa *OPRAS*. Utaratibu huu ulianza kutekelezwa tangu Septamba, 2004. Ili kuwawezesha watumishi kutekeleza vizuri utaratibu huu wa *OPRAS,* ofisi yangu imekuwa ikiendesha mafunzo kwa awamu. Kwa hiyo, ni kweli utaratibu huu haujaeleweka vizuri, hasa kwa watumishi wa Halmashauri za Wilaya, kwa vile bado haujatekelezwa vizuri kwa baadhi ya Halmashauri. Halmashauri za Wilaya, tumekwishatoa mafunzo katika ngazi za Wizara na Mikoa. Serikali inapanga

kuwaelimisha watumishi Wilayani kuanzia mwaka 2006/2007, pamoja na kuwepo na fomu itakayozingatia mahitaji ya Walimu.

Mheshimiwa Spika, napenda tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, kwa michango yao mizuri, ambayo wametupatia katika utendaji wetu wa kazi. Kama kuna ambayo labda kwa bahati mbaya hayajajibiwa, napenda kuwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutawajibu kwa maandishi na watayapata kabla ya Bunge hili kufungwa hapo mwezi wa nane.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 20 – Ikulu**

Kif.1001 - *Administration and General* ... ... ..... ... Sh. 5,550,756,800/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Kif.1001 - *Administration and General* …… ….. Sh. 89,242,541,400/=

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Niko kwenye *vote 30, subvote 1001, item 261100.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la bajeti ya mwaka huu ni asilimia 17 na ongezeko la mwaka uliopita ilikuwa asilimia sita. Mimi sihoji kiasi hiki, lakini ninachohoji pengine ningepata maelezo kilichoongezeka mwaka huu wa fedha ni nini ambacho kimesababisha ongezeko la bajeti kwa asilimia 17, ambapo ni shilingi bilioni 12, ambayo ni sawasawa na matumizi ya Ikulu, Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya *Vice President, vote* 20, 25 na *vote* 26 kwa pamoja ukijumlisha unapata ongezeko la mwaka huu?

Ningeomba nipate maelezo kwamba, ongezeko la asilimia 17 ni nini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinahusiana na Manunuzi. Naomba kutoa taarifa mbele ya Kamati yako kwamba, kuna idara kadha na vitengo kadhaa, vimeongezeka katika Ofisi ya Rais, Ikulu, lakini pia tufahamu kwamba, bei ya vitu inapanda.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote* hiyo hiyo ambayo ni *vote* 101, ningependa kujielekeza kwa kuwa nimesoma fungu zima katika *section* mbili. *Section* ya kwanza ni ile *subvote 25300 - Employment Allowances,* halafu nitamalizia na *subvote* 26110. Mimi sijaridhika na …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John M. Cheyo, naomba urudie hukusikika vizuri pale mwanzo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Kwa kuwa, imezungumzwa juu ya fungu zima, sasa katika nimechagua vitu viwili katika fungu hili ambalo ningependa kuzungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko pamoja?

**MWENYEKITI:** Siyo fungu zima ni kifungu cha 1001 hicho.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Hilo siyo fungu ni kifungu.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Sawa, Kifungu. *Subvote 1001,* ambayo jumla ni shilingi bilioni 89 na ushee kama alivyosema Katibu.

Sasa katika *subvote* hii nataka kuuliza juu ya kwanza, *employment allowances*, bado mimi sijaridhika na maelezo ya Waziri anaposema kwamba, hizi ni *allowances* za watu mbalimbali. Sasa kwa sababu ya usafiri, ukiangalia hapa mimi sikubali kabisa kwamba, hii *employment allowances* ni usafiri tu, ofisi nzima inasafiri au ni kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nimesema kwamba, hii *employment allowances* mtu akiangalia hapa anaona ni njia moja tu ya kuwapa labda ahueni wafanyakazi, lakini hili haliwasaidii wakati wanapostaafu. Kwa hiyo, kama hili ni jambo la *policy,* labda angetueleza kama kuna mtu analiangalia hili zaidi kuliko linavyokaa hivi. Kwa hiyo, hilo ni swali la kwanza, sijaridhika na hilo.

Halafu kila wakati mimi kwa kweli ni Mwenyekiti wa *PAC,* ukienda kwenye *vote 206*, *subvote* 1100 ukakutana na *figure* kubwa kama shilingi bilioni 80, ambazo zinasema *other goods and services note classified above.* Hii ambayo ni kama karibu asilimia 80 ya *vote* nzima, mtu unaanza kujiuliza tunapitisha hapa kitu gani. Najua hii ni Ofisi nyeti, lakini pia kuna sheria ambayo tumeshatunga, tumetunga sheria ya usalama, tuna sheria juu ya mambo ya rushwa, *PCB* na taasisi nyingine. Kwa nini kama hii ndiyo *lump* ya watu kama hawa, kwa nini isiwe *subdivided,* ikaonyeshwa kabisa kwamba, hizi hela zipo hapa? Kuliko mtu akiangalia namna hii anafikiri labda ni uvivu wa kutoeleza ni kitu gani kilichoko humo. Lakini zaidi baadaye tunapokwenda kwenye mahesabu inaleta tena *queries*, kwa sababu kama ni *lump* kubwa kama hii, haijulikani ni kitu gani inaleta mashaka sana. Mimi napenda maelezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, toa maelezo kwa hizo kasma ndogo mbili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo anayohitaji Mheshimiwa John M. Cheyo, yangekuwa rahisi sana kama tungelikuwa tunaongelea Wizara moja, hii ni ofisi ambayo inaongoza nchi na Wizara zote.

Kwa hiyo, unapoongea juu ya posho ya watu wengi sana; *Pilots*, Maaskari na wageni wanaokuja kila siku, ambao wanakuja bila taarifa, labda tu niseme hapa kwamba, sisi siyo wageni. Tanzania katika muda wote wa historia ni nchi ambayo inakubalika sana katika Kanda na Kimataifa. Kukubalika huku kuna gharama zake, kuna kusuluhisha ugomvi yanayotokea katika Kanda yetu na kuna kuja kuomba ushauri. Lakini pia shughuli zetu hizi ambazo zimetajwa hapa ni kutafuta michango mbalimbali ya wafadhili, ikiwa ni pamoja na wahisani wa nchi mbalimbali na hawa huwezi kuwaomba waje halafu uwaelezee matatizo yale.

Unakwenda unaongea nao kama alivyofanya Mheshimiwa Rais juzi juzi, alipoanzia ziara yake kule Ghuba, akaenda Ufaransa, Amerika, Uingereza na Abdijan, juzi alikuwa *Cape Town*, akakutana na wakubwa akina Bill Gates. Gharama hizi zinaweza kuonekana kuwa ni kubwa, lakini matokeo yake pengine ni makubwa zaidi kwa ajli ya manufaa ya Taifa. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa John M. Cheyo aelewe hivyo na yeye kwa bahati nzuri tulisafiri naye mpaka Amerika, sijui safari ile angekisia gharama ni kiasi gani, lakini juu ya manufaa yake, bila shaka angelinganisha, hayafanani kabisa na gharama ambayo tulikuwa tumeitumia. *(Makofi)*

Pili, Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote pia, wachukulie ofisi hii kwamba, tofauti yake ni kubwa sana na ofisi nyingine, kwa sababu ndiyo inayoongoza na kusimamia nchi kwa ujumla wake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Lakini hilo Waziri pengine lingekuwa linaeleza ile shilingi bilioni 80, hili suala la *employment allowances* ndiyo tunahitaji maelezo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Suala la *employment allowances* katika Ofisi Rais – Ikulu, linahusu likizo, posho ya kuhama, matibatu, posho ya utalaam, posho ya nyumba, posho ya kujikimu, kazi ya ziada, posho ya mafunzo ya ndani, posho ya mafunzo nje, posho ya vikao ndani na nje ya nchi.

**MWENYEKITI:** Safi sana, naona limekaa vizuri.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* … … … … Sh. 706,135,000/=
Kif. 2001 - *Cabinet Secretariat* … … … … … Sh. 1,128,601,600/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

Kif. 1001 – *Administration and General* … … … Sh. 5,910,157,100/=

**MWENYEKITI:** Ninawaona Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa na Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, haya tutakwenda kwa utaratibu huo huo.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Program* namba 10, *subvote 1001*, kifungu 280800 *Transfers and Subsidy-Householda and Individuals.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2004, kifungu hicho kilikuwa na bajeti ya *shilling 2.8 billion* na mwaka 2005 ikawa ni *shilling 2.4 billion,* sasa hivi ni *shilling 4 billion*, tunataka tupate maelezo ni kwa matumizi gani yaliyofanywa hivyo. Tunataka maelezo haya kwa sababu kwa bahati mbaya, mfumo wetu wa bajeti unafunga funga mambo mengi sana, huwezi kujua hasa hiki kinakusudiwa nini na hilo ni tatizo moja ambalo tunalipata. Kwa hiyo, tunaomba hilo tupate ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo wakati Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, anajibu hoja alisema kwamba, imekuwa jumla jumla katika kutoa hoja zetu za rushwa, lakini tulikuwa *very specific* na bahati mbaya katika Kitabu hiki hakuna *department* ya Rushwa, yaani fungu peke yake la Mambo ya Rushwa halipo. Kwa hiyo, tunaona tutumie fungu hili hili, kuweza kupata majibu ya hilo, ametaja Wizara ya Elimu na TVT kwamba, ni maeneo ambayo *Public Accounts Committee* ilipendekeza kwamba, ni sehemu inayotakiwa kuchunguzwa na Idara ya Rushwa na taarifa hatujazipata lakini hakutoa maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hsante sana.

**MWENYEKITI:** Naomba urudie hapo.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwamba, katika kifungu 280800 *Transfers and Subsidy-Householda and Individuals*. Mwaka 2004 kulikuwa na bajeti ya *shilling 2.8 billion* halafu ikaja *shilling 2.4 billion* mwaka 2005, leo ni *shilling 4 billion.*

Tunataka uchambuzi wa hii *shilling 4 billion* imefikiaje? Kama nilivyosema kwamba, tatizo la bajeti yetu, mahesabu yetu yanakuwa makubwa ni tofauti na wenzetu wengine wanavyofanya kwamba, hata ziara za Rais unazijua ni ngapi kwa mwaka na kadhalika. Sisi hapa hatuna utaratibu, kwa hiyo, nilitaka ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sababu vilevile katika kitabu hiki, hakuna fungu maalum la Idara ya Kitengo cha Rushwa.

**MWENYEKITI:** Ndiyo lile lililopita la *shilling 8 billion* alilouliza Mheshimiwa John M. Cheyo, ndiyo hilo linajumlisha Usalama wa Taifa, hao wazito hao. Lakini endelea.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa hiyo, kwa sababu Waziri alisema tumemwuliza kwa jumla jumla wakati tumekuwa *very specific* katika masuala yetu, tumemwuliza Wizara ya Elimu ya Taifa ilipo *appear* kwenye *Public Accounts Committee,* baada ya kuwahoji kuleta *computer* ambazo zilikuwa mbovu, kulikuwa na *element* ya rushwa ndani yake, tuka-*report PCB* ichukue hatua, huu ni mwaka wa nne, hatujapata taarifa yoyote.

Kuna *TVT Public Accounts Committee,* vilevile ilifanya uchambuzi, ikatoa taarifa na ikataka ifanyiwe uchambuzi na *PCB* itoe taarifa, mpaka leo hakuna taarifa. Sasa siyo mambo ya jumla jumla, tumesema vitu *specific* na tungetegemea Serikali ingetujibu kwa yale ambayo tumeyasema kwa ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ninavyokumbuka ni kwamba, Mheshimiwa Waziri alijibu kwamba, kwa hayo *specific,* kulingana na muda asingeweza kuyajibu *orally* na kwamba, wanaandaa taarifa sasa kamili ya tuhuma za *PCB* na majibu yako, ambayo itasambazwa. Muda bado upo, baada ya kuipata hiyo, kama hatutaridhika, bado Bunge linaweza kuendelea kuhoji. Swali la kwanza Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki alichokizungumzia, kinawahusu wastaafu na sasa hivi nadhani wastaafu wanaongezeka kwa kuwa mwaka 2005, kuna Rais alistaafu, kuna Waziri Mkuu alistaafu, kwa hiyo na wao wanahudumiwa katika kifungu hicho. Kwa hiyo, kitakuwa kinaendelea mwaka hadi mwaka, kadri wastaafu wanavyoongezeka.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nifafanuliwe fungu hili na la *pension* linatofautianaje, kwa sababu kuna fungu la *pension*?

**MWENYEKITI:** Aah! Lakini Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, mbona hili linajieleza. Hawa wanaostaafu wanatunzwa, hii siyo *pension* ya kila mwezi, hii ni *households*, kwa utaratibu wetu Marais Wastaafu na Mawaziri Wakuu Wastaafu, wana haki zao chini ya Sheria, wanapata mambo hayo. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika programu ya 10, *subvote 1001,* baada ya kupitia kule nyuma na hapa kwa kuwa sikuona, nilikuwa napenda kutumia *subvote 100,1* kifungu kidogo cha 205100 kupata ufafanuzi kuhusu yafuatayo:-

La kwanza, kwa kuwa ndani ya Bunge hili, tulipitisha Sheria ya Usalama wa Taifa na Usalama wa Taifa ni moja kama yalivyo Majeshi yetu ya Ulinzi, kama Polisi tunajua kuna mambo yao ya siri, tunajua kuna utaratibu ambao tusingependa kuujadili, pia kwa sababu unahusu masuala labda ya usalama wa Taifa. Lakini masuala ya fedha, siyo masuala ya siri na kwa kuwa mishahara hasa ya watu inakuwa ni haki iweze kuonekana na Bunge hili, ili wale ambao wana malalamiko, wanapofika kwa Wabunge na Wabunge waweze kuangalia fungu lao labda liko wapi na kunapokuwa kuna sababu ya kufuatiliwa liweze kufuatiliwa.

Je, ni lini sasa Serikali kwa kuwa Sheria ilipitishwa na kwa kuwa zamani usalama ulikuwa kidogo siri na sasa si siri; ni lini basi kasma yao itawekwa wazi ili Bunge pia liweze kufuatilia na kujua fedha zinazotengwa kwa yao ziko ngapi na kwa ajili ya nini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kumbukumbu yangu ni kwamba, muda mfupi uliopita, tulishamaliza vifungu vinavyohusu anayoyaongelea Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, sasa anataka kulitumbukiza wapi suala hili, kwa sababu halihusiani kabisa na fungu lililopo mbele yetu kwa sasa?

**MWENYEKITI:** Nadhani ulikuwa na *points* mbili?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nina *points* mbili, lakini hata katika hili …

**MWENYEKITI:** Mimi nilikuwa nakusubiri umalize, lakini endelea sasa kabla sijatoa mwongozo wangu.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Ukitazama kichwa cha *vote* iliyotangulia ni *Cabinet Secretariat,* hakuna mahali popote inapoeleza kwamba, hapa ndipo pana usalama wa Taifa na kazi ya Bunge inapofuatilia ni kuona fungu la fedha ziko wapi na hapa tunapopitisha tunataka kujua ni kifungu gani hasa tunakipitisha.

Sasa Mheshimiwa Waziri, anapotuambia imepita ndiyo ni kweli kifungu kimepita, lakini kwa Wabunge ni nini kimepita, labda Kamati iliyojadili inaweza kujua lakini sisi ambao hatuko kwenye Kamati hatuwezi kujua? Ndiyo nilikuwa nauliza sasa, ni lini Serikali itatengeneza kasma maalum, kwa ajili ya Usalama wa Taifa ili iwe rahisi kwa Wabunge kufuatilia kama tunavyofuatilia kwa Jeshi la Wananchi, Polisi na *FFU,* kwa sababu suala la fedha si siri? Kazi yao ni siri na hatuhitaji kujadili kazi yao hapa ndani, lakini fedha tunahitaji kujua wana-*operate* vipi kwa sababu pia Wabunge tunafikiwa na malalamiko kwamba, kuna matatizo katika malipo yao. Sasa hilo tutaliona kama tuna

kasma yao, hilo lilikuwa ni swali la kwanza, ni lini italetwa, je, kuna utaratibu huo kama haupo pia tujulishwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika mchango wa maandishi, nilikuwa nimeomba na hili, sidhani kama kuna utata lakini linahitaji kupata ufafanuzi na maelezo, katika mchango wa maandishi nilieleza kwamba, wafanyakazi walio wengi, hasa katika Sekta Binafsi, kwa kweli kiwango chao cha mishahara, hakuna chombo rasmi kinachoratibu, japo kuna sheria. Sasa ni vitu viwili kuwa na sheria na sheria ile kufanya kazi. Nadhani tungeweza kujiuliza tu ni lini hicho kinachoitwa *Minimum Wage Board,* ilikutana mara ya mwisho, kwa kumbukumbu yangu ni zaidi ya miaka 15 iliyopita na tangu wakati huo haijakutana tena?

Sasa kama haijakutana, wafanyakazi walioko wengi nje, wengi zaidi kuliko hata wa Serikali Kuu tunaowazungumza, hata kuliko wa Halmashauri, kwa pamoja hao waliopo kwenye *Private Sector* ni pamoja na waliopo kwenye mahoteli na mashamba. Je, hawa haki zao sisi kama Wabunge tunazisimamia vipi?

Sisi Wabunge tunapata matatizo kwa sababu kwa mfano, mimi ukiniuliza kwangu kuna mashamba 45, nina wafanyakazi zaidi ya 20,000, lakini wanalipwa chini ya kiwango cha Serikali. Sasa nilitaka kujua, je, ni lini hawa watu tawawekea mfumo unaoeleweka? Najua ndani ya Bunge, tulitunga Sheria ya *Labour Laws* na *Labour Institutions,* lakini mpaka leo haijafanya kazi. Kwa hiyo, ilikuwa ni suala tu la kupata ufafanuzi kama je, ile *negotiating machinery,* kama *Minimum Wage Board* yenyewe itaanza tena au vipi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, umemaliza dakika zako. Mwongozo wa Mwenyekiti kuhusu hizi kasma ndogo.

Nadhani napenda niisihi Serikali, ikubali hoja kwamba, namna kasma hizi zilivyoandikwa, zinaleta ugumu sana wa kuweza kujadili. Kwa mfano, nimeuliza Sekretarieti sasa hivi ya TAKURU iko wapi? Haimo kabisa kwa hiyo, mtu akitaka kuzungumzia suala la rushwa, ataambiwa tena limepita.

Nadhani tukienda kwa *technical knockout*, hatuwezi kuutendea umma haki. Kwa hiyo, nimeruhusu hilo swali lijibiwe kwa sababu ni vizuri tujue na mimi nasema kama Mwenyekiti hapa, ni vizuri tuangalie tena vitabu hivi ili kweli ikijitokeza *vote* zilivyo na zoezi zima la kuidhinisha makadirio, liwe na maana kwa wananchi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa mwongozo wako. Bahati mbaya ndiyo Kanuni tunayoitumia, sasa mimi pia ningefurahi wakati ukifika kwamba, Kanuni zitatuongoza ili kufafanua mafungu yetu haya na kwa vile Kanuni ndiyo ilivyo, sasa tunafungwa lakini labda …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kaa chini. Wewe unafahamu kwamba, mwongozo wa Mwenyekiti ukishatoka, haiwezekani tena kuwa na mjadala. Hizo ndiyo Kanuni za Bunge, sasa nakushangaa unaendelea. Upo utaratibu wa kupinga mwongozo wa Mwenyekiti, unaweza kuutumia lakini mwongozo wangu ni huo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa mwongozo wako.

TAKURU ni sehemu ya Ofisi ya Rais, *Vote 30, President's Office and Cabinet Secretariat*. Watumishi wa TAKURU, Watumishi wa Usalama wa Taifa na Watumishi wengine wote wa Ikulu, wanachukuliwa kama Watumishi chini ya mwajiri mmoja.

**MWENYEKITI:** Bado la pili.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia kifungu cha 81, kinachoniruhusu kuomba ufafanuzi zaidi, sitaki kwenda kwenye kushika shilingi, lakini nadhani Waziri hajajibu.

Mimi niliuliza kwamba, sasa kwa sababu kazi ya Bunge iko wazi, ni kupitisha mafungu yaliyo wazi, Serikali haioni kwamba, wakati umefika wa kutengeneza kasma baada ya kupitisha Sheria ya Usalama wa Taifa, hatua ya pili iwe ni kuleta kasma iliyo wazi ili tunapozipitisha iwe wazi kwamba tunapisha nini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa wazi zaidi, naomba nimwelekeze Mheshimiwa Mbunge, kwenye kasma hiyo, kifungu kidogo cha 261100. Kifungu hiki kiko chini ya Fungu 30 - Ofisi ya Rais – Ikulu, kinahudumia TAKURU na Idara yetu ya usalama wa Taifa.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu 32 *subvote* 1001, Kifungu kidogo 250300. Mheshimiwa Waziri, alipokuwa anafafanua kwamba, kuna watumishi wengine ambao wanasomeshwa kwa fedha za Watanzania, wanafikia kupangiwa maeneo hawaendi kuripoti kwenye maeneo hayo. Sasa ninaomba Waziri, anifafanulie watu kama hao Serikali imewachukulia hatua gain, ukijua kwamba wamesomeshwa kwa fedha za Watanzania na wakati wanasomeshwa wanasema watafanya kazi mahali popote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo zaidi.

**WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa wale ambao wanakataa kwenda, baadhi ya maeneo ambayo wanapangiwa kwenda kufanya kazi, wanachukuliwa hatua lakini bado kama Serikali, tunachukua hatua za kuhakikisha kwamba, tunaboresha baadhi ya maeneo ambayo watumishi wanakataa kwenda kufanya kazi. Suala hilo ni mojawapo ambalo Tume ya Maslahi ya Mheshimiwa Rais iliyoundwa, imepewa kama hadidu za rejea kuangalia maeneo kama hayo, tuweke motisha za aina gani ili watu waende. Kwa sababu kuwapa adhabu ni namna moja, lakini watu kwenda ni aina nyingine. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* … … … … … … Sh. 144,053,600/=
Kif. 2001 - *Policy Develompment* … … … … … … Sh. 347,868,300/=
Kif. 2002 - *Management Services* … … … … … … Sh. 229,187,600/=
Kif. 2003 - *Establishment* … … … … … … .. … … Sh. 420,641,100/=
Kif. 2004 - *Ethics Division* … … … … … … .. … Sh. 128,731,800/=
Kif. 3001 - *Human Resource Development* … … …Sh. 412,921,100/=
Kif. 3002 - *Civil Service Training Centre* … … Sh 454,470,000/=
Kif. 3003 - *Tabora Secretarial College* … … … Sh. 252,499,500/=
Kif. 3004 - *Gender* … …… … … … … … … … … Sh. 60,194,000/=
Kif. 4002 - *Management Information System* … … Sh.179,834,500/=
Kif. 4003 - *National Achieves* … … … … … … … Sh.581,987,400/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 33 – Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi**

Kif. 1001 – *Administration and General* … … … …Sh. 1,249,076,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 94 – Tume ya Utumishi wa Umma**

Kif. 1001 – *Administration and General* … … … … Sh. 2,839,114,100/=
Kif. 2001 – *Civil Service* … … … … … … … … …Sh. 461,745,900/=
Kif. 2002 – *Local Government Service* … … … … Sh 518,187,200/=
Kif. 2003 – *Teachers' Service* … … … … … … ... . Sh.3,441,265,400/=
Kif. 2004 – *Fire and Immigration Service* . … … … Sh. 346,359,300/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2005 – *Health Service* ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh.322,654,100/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 30 – Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Kif. 1001 – *Administration and General* ... ... ... ... Sh. 34,785,840,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... Sh. 4,558,870,000/=
Kif. 2001 - *Policy Development* ... ... ... ... ... ... ...Sh. 3,900,429,200/=
Kif. 2002 - *Management Service* ... ... ... ... ... ... .. Sh. 25,495,560,000/=
Kif. 2003 - *Establishment* .... ... ... ... ... ... ..... .... Sh. 1,217,740,000/=
Kif. 2004 - *Ethics Division* . ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 762,546,400/=
Kif. 3001 - *Human Resources Development* ... ... ... Sh.3,024,026,700/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3002 – *Civil Service Training Centre* ... ... ... ... Sh. 1,300,000,000/=

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la kutaka ufafanuzi tu. Katika bajeti ya kawaida, *Tabora Secretarial College,* ilitajwa peke yake, katika bajeti ya maendeleo siioni, kwa maana ya maendeleo na ninavyofahamu ni kwamba, chuo kile kinahitaji matengenezo.

Je, fedha za matengenezo ya chuo hicho zipo katika fungu hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Chuo cha Uhazili Tabora kimetengewa fedha. Lile ni Tawi la Chuo cha Utumishi wa Umma cha Magogoni, kilichopo Dar es Salaam. Kwa hiyo, kimetengewa fedha na kitafanyiwa ukarabati.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3004 - *Gender*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 1,166,421,000/=
Kif. 4002 - *Management Information System* ... ... .. Sh. 4,651,574,000/=
Kif. 4003 - *National Archives* ... ... ... ... ... ... ... .. Sh. 3,230,391,200/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 94 – Tume ya Utumishi wa Umma**

Kif. 1001 – *Administration and General*... ... ... ... ... ...Sh. 139,998,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFI SI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati yako ya Matumizi baada ya kujadili taarifa ya Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imeyapitia makadirio ya matumizi ya fedha ya Ofisi ya Rais – Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma, kwa mwaka wa fedha 2006/2007, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, basi Bunge lako Tukufu liyakubali mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo. Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', anawaarifu Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii kwamba, kesho tarehe 14 Julai, 2006, kutakuwa na kikao cha Kamati saa tano asubuhi Chumba Na. 231.

Mnaombwa kwanza mpitie makabrasha yanayohusu mkutano huo kwenye *pigeon holes*, mtayakuta jioni hii hii, ili kesho saa tano muweze kukutana. Kwa hiyo, ni saa tano asubuhi Kamati ya Huduma za Jamii, Chumba Na. 231.

Nilikuwa nimewaarifu mmoja mmoja kwamba, Kamati ya Uongozi ingekutana kesho au Jumapili. Sasa kutokana na wengi kuwa na udhuru, tumeahirisha badala yake Kamati ya Uongozi, pamoja na Tume ya Huduma za Bunge, tutakutana wiki ijayo katika muda na siku ambayo itatangazwa, lakini wiki ijayo.

Baada ya kusema hayo, kwa sababu bado dakika saba kabla ya wakati wa kuahirisha Bunge, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, mambo ya Bunge aweze kutoa hoja tuweze kuahirisha shughuli za Bunge.

**KUAHIRISHA BUNGE KABLA YA WAKATI WAKE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako liahirishwe dakika kama saba hivi kabla ya muda wake kwa sababu shughuli za leo zimekwisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 01.40 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 14 Julai, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*